Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA TANO

**Kikao cha Nne – Tarehe 3 Novemba, 2006**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 41

**Wananchi ambao Hawakupata Nafasi ya Kupiga Kura**

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR** aliuliza:-

Kwa kuwa mara baada ya kumaliza uchaguzi mkuu wa mwaka 2005 kuna taarifa kuwa kuna baadhi ya wananchi wa Tanzania hawakupata nafasi ya kupiga kura kwa sababu wapo maeneo ya mbali na miji au wanaishi porini ambako Tume ya Uchaguzi ilishindwa kuwafikia:-

(a) Je, ni wananchi wangapi wanaokadiriwa kuwa hawakupata nafasi ya kupiga kura na zaidi ni kutoka Mikoa gani?

(b) Je, hivi ni kweli hadi sasa bado wapo Watanzania ambao bado wanajua kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni Mwalimu J.K. Nyerere, kama wapo Serikali ina mpango gani wa kuwatoa wananchi hao katika kiza hicho kinene?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, MAAFA NA KAMPENI DHIDI YA UKIMWI (MHE. DR. LUKA J. SIYAME)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir, Mbunge wa Dimani, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Ni kweli kwamba wakati wa uchaguzi Mkuu wa 2005 sio watu wote waliostahili walipiga kura. Kupiga kura kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 ni suala la hiari. Hivyo mtu kwa hiari yake anaweza kuamua asipige kura. Jumla ya wananchi 4,968,876 kati ya wananchi 16,407,318 waliojiandikisha kupiga kura hawakupiga kura. Mikoa yenye watu wengi ambao hawakupiga kura ni Dar es Salaam ukifuatiwa na Mkoa wa Mwanza.

(b) Mheshimiwa Spika, sio kweli kwamba bado wapo Watanzania wanaojua kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni Mwalimu J.K. Nyerere. Hayati Mwalimu J.K. Nyerere alikuwa Rais wa Awamu ya Kwanza ya Utawala wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aliongoza nchi yetu vizuri sana na kuitangaza ulimwenguni kote.

Hata hivyo, tuliendelea na uongozi wa Awamu ya Pili, Awamu ya Tatu na hivi sasa tupo katika Awamu ya Nne chini ya uongozi wa Rais Jakaya Mrisho Kikwete. Hakuna wananchi ambao wanahesabika kuwa katika kiza cha kutoelewa hilo hapa nchini.

Kama Mheshimiwa Mbunge anayo taarifa kuhusu wananchi walio katika kiza kinene anachokieleza, anaweza kuiwasilisha ili ifanyiwe kazi.

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR:** Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake lakini nina maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

(a) Katika maelezo yake, amezungumzia suala la kupiga kura ni hiari, swali langu lilikuwa linakwenda moja kwa moja kwa wale wananchi ambao wanapenda kupiga kura lakini hawakupewa nafasi ya kupiga kura kwa sababu sekta inayohusika na wananchi kuwafanya wapige kura haikufika katika maeneo yao wanakoishi. Sasa suala la kuwa la hiari na suala la kuwa na hamu ya mtu kupiga kura lakini hawakufikiwa ndio swali langu kubwa. Je, anaweza kuliambia Bunge hili idadi ya hawa na ni maeneo gani hasa? Ndio swali langu la msingi.

(b) Kuna baadhi ya wananchi bado wanafahamu kwamba Mwalimu Nyerere bado ni Rais wa Jamhuri.

Je, Serikali imefanya jitihada gani kuwaelimisha wananchi katika kufahamu kwamba hivi sasa tuko katika Awamu ya Nne na Rais wa Jamhuri ya Muungano ni Rais Jakaya Kikwete?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. JUMA J. AKUKWETI):** Mheshimiwa Spika, Tume ya Uchaguzi inahakikisha kwamba kila mahali katika nchi yetu inafikiwa na kila mmoja mwenye kutaka kupiga kura anapiga kura na vituo vinasambazwa nchi nzima.

Ni vigumu kuweka kituo kila nyumba lakini Tume ya Uchaguzi imejitahidi iwezevyo kuweka vituo karibu na makazi ya watu ili kila mmoja apate nafasi ya kupiga

kura. Kwa hiyo, ni imani ya Serikali kwamba kwa yule ambaye alikuwa na nia ya kutumia nafasi yake na haki yake ya kupiga kura alipata nafasi hiyo na alifanya hivyo.

Kwa niaba ya Serikali, nichukue nafasi hii kuwaomba Watanzania wote kwamba haki ya kupiga kura ni muhimu sana. Kuna nchi wanapigana, wanamwaga damu kuhakikisha kwamba anapata nafasi ya kupiga kura. Kwa hiyo, natoa wito kwamba kila mara inapotokea kupiga kura wote twende kupiga kura kwa sababu ndio njia halali na ya pekee ya kuhakikisha kwamba uongozi wa nchi unawekwa kwa matakwa ya wananchi wenyewe.

Mheshimiwa Spika, swali la pili kuhusu elimu. Nadhani Mheshimiwa Tahir anafahamu kwamba Serikali inajitahidi kwa kadri iwezavyo kutangaza matokeo ya nchi yetu na kwamba kila mara Rais anapoapishwa kuna matangazo ya redio, magazeti, televisheni na kadhalika.

Kwa hiyo, mimi naamini kwamba kwa jitihada ambazo zinafanywa na Serikali na jinsi Marais hawa wote toka Awamu ya Kwanza, Awamu ya Pili, Awamu ya Tatu na ya Nne ya Rais Jakaya Mrisho Kikwete, wanavyozunguka nchi nzima, nashindwa kuamini kwamba kuna mtu bado baada ya miaka hii yote anaamini kwamba Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere bado ni Rais wa nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hilo lipo tunachosema atupe maeneo hayo atueleze ili Serikali ifanye jitihada ya kuwafikia hao hata kwa mguu, hata kwa punda na kwa namna yoyote ili tuwaambie kwamba Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete. *(Makofi)*

Na. 42

**Kuweka Uzio Kwenye Hospitali ya Kiomboi**

**MHE. DIANA M. CHILOLO** aliuliza:-

Kwa kuwa Hospitali ya Kiomboi ya Wilaya ya Iramba haina uzio wa kudumu na wodi za watoto na wanawake zimechakaa sana:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga uzio wa kudumu na kukarabati majengo hayo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MISDTAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Diana M. Chilolo, Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, napenda nikubaliane na Mheshimiwa Mbunge kwamba Hospitali ya Wilaya ya Iramba haina uzio wa kudumu, paa katika wodi za watoto na wanawake linavuja na mfumo wa maji safi na maji taka sio mzuri. Uzio uliopo ni wa Senyenge ambao umekuwa ukiharibiwa na baadhi ya watu wasio waaminifu kwa kuukata hivyo kulazimu uwe unafanyiwa ukarabati wa mara kwa mara.

Mheshimiwa Spika, hospitali ya Kiomboi ina uwezo wa vitanda 180 na majengo yote muhimu kwa ajili ya kutoa huduma, yapo katika eneo moja (*under one roof)* hivyo endapo ukarabati utafanyika hauna budi kuhusisha majengo yote. Hata hivyo, kwa mara ya mwisho hsopitali hiyo ilifanyiwa ukarabati mkubwa mwaka 1997 kwa msaada wa Benki ya Dunia kupitia mradi wa afya na lishe na kugharimu Tsh.200,000,000/= ambapo majengo yote ya hospitali yalifanyiwa ukarabati ikiwa ni pamoja na wodi ya watoto na wanawake.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri kwa kutumia fedha za matumizi ya kawaida na gharama za uchangiaji huduma na *Basket Fund* imekuwa ikifanya ukarabati mdogo mdogo katika hospitali hiyo kuanzia mwaka 2000-2005 ambapo jumla ya Tshs.17,055,850/= zimetumika kwa mchanganuo ufuatayo:-

(i) Ujenzi wa vyoo vya wagonjwa ;
(ii) Ukarabati wa vitanda;
(iii) Ukarabati wa bomba la majitaka;
(iv) Uwekaji wa milango ofisi za Waganga; na ofisi nyinginezo;
(v) Ukarabati wa uzio;
(vi) Ukarabati wa stoo ya madawa;
(vii) Ukarabati wa wadi ya watoto; na
(viii) Ukarabati wa vifaa mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kwa kuona umuhimu wa uzio na ubovu wa wodi ya watoto na wanawake katika mwaka wa fedha 2007/2008, Halmashauri ya Kiomboi itatenga fedha kwa ajili ya kufanya ukarabati wa wodi hiyo ya watoto na pamoja na uzio huu.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

(i) Kwa kuwa hospitali ya Wilaya ya Kiomboi pamoja na ukarabati uliofanywa na Halmashauri kuhusu vyoo, mpaka sasa hivi vyoo hivyo havifanyi kazi. Je, Serikali inasema nini kuhusu hili tatizo ambalo linaweza kuzua magonjwa ya mlipuko kwa wagonjwa wanaotibiwa katika hospitali hiyo?

(ii) Kwa kuwa tatizo la hospitali ya Wilaya ya Iramba linafanana kabisa na hospitali ya Wilaya ya Manyoni na kwa kuwa hospitali ya Wilaya ya Manyoni haina chumba cha kupikia wagonjwa hasa wodi ya watoto na akina mama na ambapo wengi wao wanatoka vijijini hawana maeneo ya kupikia wanapolazwa wagonjwa wao. Je, Serikali inasema

nini kuhusu kusaidia hilo ambalo ni huduma muhimu ukizingatia Halmashauri zetu hazina pesa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MISDTAA** Mheshimiwa Spika, kwa hospitali ya Kiomboi ukarabati mdogo mdogo unaendelea kama kawaida kwa sababu kuna fedha za *basket fund* na fedha za matumizi ya kawaida. Iwapo tatizo hili ni sugu na gumu, tutaiagiza Halmashauri itengeneze vyoo hivyo kwa sababu ni jambo la muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hospitali ya Manyoni, ikumbukwe kwamba Serikali sasa hivi iko katika utekelezaji wa ukarabati wa vituo vya afya pamoja na Zahanati na kwa mwaka ujao 2007/2008, Serikali ina mkakati wa kutengeneza hospitali zote za Wilaya kwa awamu. Kwa hiyo, mradi huu utaanza hivi karibuni. Hivyo namwomba Mheshimiwa Mbunge awe na subira, iwapo mradi huo utatekelezwa hiyo hospitali ya Manyoni pia itaangaliwa.

**MHE. LAZARO S. NYALANDU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Tukiwa pale pale Mkoani Singida, hospitali yaKitinko imejengwa kwa gharama ya zaidi ya dola za Kimarekani milioni moja. Ina uzio, ni hospitali inayohudumia watu takriban laki mbili wa Jimbo la Singida Kaskazini, ni lini Serikali itakubali kuifanya hospitali ya Kitinko kuwa *District Designated Hospital* ili kuwasaidia wale ambao wanahitaji msaada?

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, uamuzi wa kuifanya hospitali kuwa teule unaanzia katika Wilaya husika na kupitishwa katika vikao vya *RCC* mpaka kufika Serikali Kuu. Ninavyojua ni kwamba Singida Vijijini ina hospitali mbili ikiwepo ya Makyungu wote wana azma hiyo ya kuifanya mojawapo iwe hospitali teule. Kwa hiyo, naomba hili suala lianzie kule, wakubaliane na kuleta mapendekezo halafu watafikiriwa pamoja na mengine.

Na. 43

**Tanzania Kuitwa Moja ya Nchi Maskini Sana Duniani**

**MHE. JUMA ABDALLAH NJWAYO** aliuliza:-

Kwa kuwa Tanzania inahesabika kuwa ni moja ya nchi maskini sana duniani:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kufuta neno hilo la aibu kuitwa nchi maskini duniani? (b)Je, umaskini wetu unatokana na nini wakati Tanzania ina kila aina ya utajiri kuanzia bahari, maziwa, mbuga za wanyama, mifugo, mazao mbalimbali, gesi, madini na kadhalika.

**NAIBU WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Juma Abdallah Njwayo, Mbunge wa Tandahimba, lenye sehemu (a) na (b) kama ifutavyo:-

(a) Tanzania kama sehemu ya jamii ya Kimataifa, inatekeleza Malengo ya Maendeleo ya Milenia *(Millennium Development Goals)*. Malengo haya ni vigezo muhimu ambavyo Mataifa yamejiwekea ili kupunguza umaskini ifikapo mwaka 2015. Tathmini ya hivi karibuni inaonyesha kuwa Tanzania itafikia vigezo vingi vya malengo haya.

Aidha, Serikali kwa kushirikiana na wadau wengine wa maendeleo inatekeleza Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kuondoa Umaskini (MKUKUTA) na kwa Zanzibar Mkakati wa Kukuza Uchumi Zanzibar (MKUZA). Lengo kuu la mikakati hiyo ni kuondoa umaskini na hivyo kufikia Malengo ya Muda Mrefu ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 na Dira ya Maendeleo ya Zanzibar 2020.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, Serikali peke yake haiwezi kufanikiwa katika vita vya kuondoa umaskini. Jitihada za kuondokana na umaskini zinahitaji ziungwe mkono na wananchi wote, mashiriki yasiyo ya Kiserikali, makampuni binafsi, taasisi na asasi mbalimbali.

(b) Mheshimiwa Spika, sababu za umaskini wa Tanzania zimeinishwa katika tathmini nyingi. Aidha, umaskini una sura nyingi, hivyo si rahisi kuwa na sababu zinazofanana sehemu zote. Hata hivyo, sababu za jumla zinazoleta umaskini zimegawanyika katika makundi mawili yaani sababu za ndani na zile za nje.

- Baadhi ya sababu za ndani ni pamoja na:-

- Kutokuwepo na mitaji ya kutosha kuwekeza katika miundombinu kama vile barabara, reli, njia za mawasiliano, nishati na maji;

- Teknolojia duni inayotumika katika uzalishaji na utoaji wa huduma;
- Uzalishaji mdogo wa mazao ya chakula na biashara unaotokana na huduma zisizotosheleza katika sekta ya kilimo;

- Uwekezaji usiotosheleza katika sekta mbalimbali zikiwemo kilimo, viwanda vidogo vidogo vya kati na vikubwa;

- Viwango vidogo vya elimu katika fani mbalimbali;

- Idadi kubwa ya wategemezi katika kaya na tabia ya uzembe na uvivu;

- Urasimu usio na lazima katika asasi za umma na zile za sekta binafsi; na

- Athari mbalimbali zitokanazo na maradhi pamoja na majanga mbalimbali kama vile ukame, athari za UKIMWI na kadhalika.

Aidha, baadhi ya sababu kubwa za nje ni pamoja na:-

- Deni la Taifa ambalo ni kubwa na linatumia rasilimali nyingi ili kulilipa;

- Kupanda kwa bei ya mafuta ambayo imekuwa ikiathiri shughuli za uzalishaji mali na usafirishaji; na

- Bei duni kwa bidhaa ghafi tunazouza katika soko la dunia ikilinganishwa na bei za bidhaa tunazonunua hivyo kusababisha urari mbaya katika biashara ya Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kubainisha vikwazo vya ndani na nje vinavyoleta umaskini, Serikali imejipanga kuhakikisha kuwa Tanzania inaondokana na umaskini kwa kuboresha sekta ya kilimo, miundombinu, elimu, afya na uwezeshaji wa wananchi kiuchumi kwa kuwapatia mitaji yenye riba nafuu na kuboresha mazingira ya uwekezaji. Aidha, kupitia Ilani ya Uchaguzi ya CCM, Serikali imejizatiti kuhakikisha kuwa inajenga maisha bora kwa kila Mtanzania.Kupitia Bunge lako Tukufu, napenda kuwahimiza Watanzania wenzangu, wake kwa waume, kujituma na kushiriki kikamilifu katika shughuli za uzalishaji za kiuchumi ili kuungana na Serikali katika jitihada za kupambana na umaskini.

**MHE. JUMA ABDALLAH NJWAYO:** Mheshimiwa Spika, napenda nichukue nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu ya kutosheleza lakini hata hivyo nina maswali madogo ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa katika hali ya sasa imejionyesha dhahiri kwamba mazao ya biashara yamekuwa yakisaidia kupunguza umaskini hapa nina maana mazao kama korosho, pamba, kahawa na kadhalika na katika hali iliyopo sasa kwamba tume-*liberalized* mno biashara ya mazao haya kiasi cha kuwafanya wanunuzi wakiamua ku-*curtail* inaleta matatizo sana kwa wazalishaji wa mazao ya biashara kama ilivyojitokeza hivi karibuni kwenye zao la korosho. Je, Serikali ina mpango wowote wa kuvisaidia vyama vya ushirika kwa dharura kuwapa mitaji ili waondoe tatizo la umaskini na hasa linalotokana na ujanja ujanja unaofanywa na wafanyabiashara?

(b) Kwa kuwa tulibinafsisha viwanda vyetu na hasa vile vya korosho kwa wafanyabiashara Wazalendo wa Kitanzania na kwa kuwa ukarabati unaofanywa unaenda pole pole na moja ya mambo yanayoonyesha ukarabati huo kwenda pole pole ni kukosa pesa za kutosha kufanya ukarabati huo. Je, Serikali ina mpango gani wa dharura kuwasaidia wazalendo hao ili waweze kukamilisha ukarabati ule na hivyo wanunue mazao ya wakulima kama vile korosho ili kuondoa umaskini walionao na hivyo kuongeza tija na uchumi kwa wananchi hao wa Tanzania?

**NAIBU WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Spika, kwanza, suala la uwezeshaji wa vyama vya ushirika ili viweze kushiriki katika kununua mazao mbalimbali ikiwemo zao la korosho ni suala la muhimu sana. Sisi kama Serikali tunatambua kwamba mashirika binafsi yana mchango mkubwa sana katika kuondoa umaskini. Mchango wao unatokana na kwanza kuongeza tija katika bidhaa zao lakini vile vile kutoa ajira. Kwa hiyo, sasa hivi kuna mkakati mkubwa wa kuweza ku-*modernize* na kubadilisha mfumo mzima wa ushirika. Lakini vile vile tunatambua kwamba wanunuzi na makampuni yanayofanya shughuli za ununuzi wa korosho wameanzisha mfumo wa *curtail*. Hilo linafahamika na sasa hivi Serikali inafanya jitihada za makusudi kabisa katika kuona kwamba hawatumii nafasi hiyo ya kiujanja ili kuweza kuwafanya wananchi wa maeneo wanayozalisha korosho wabaki kuwa na umaskini. Ni lazima makampuni binafsi yatambue kwamba wao kama sehemu ya nchi hii na sehemu ya jamii, yana mchango mkubwa katika kuondoa umaskini. Tarehe 17 mwezi uliopita, China ilitoa zawadi katika makampuni makubwa manne kwa ajili ya mchango wao katika kuondoa umaskini. Sisi kupitia Wizara yetu ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, tutahakikisha kwamba tunafuatilia ili kuona kwamba makampuni haya yanayonunua korosho hayatumii fursa hii ya utandawazi kuweza kuwadhulumu na kuwanyanyasa wakulima wa zao la korosho.

Mheshimiwa Spika, swali la pili ameuliza kuhusu jitihada za kusaidia viwanda vilivyobinafsishwa ili viweze kuwa na mchango wao katika kubangua korosho. Sisi tunafahamu kwamba katika lengo la kusaidia wazawa tumebinafsisha viwanda na viwanda vingi vimenunuliwa na Watanzania wazalendo wenzetu. Sisi tunachoweza kusema kama Serikali ni kuhamasisha waende katika mabenki wakachukue mkopo kwa sababu kuna tabia ya kuogopa mikopo. Mimi nadhani tuthubutu twende tukachukue mikopo kwa sababu mikopo ipo katika taasisi za biashara. Napenda nimalizie kwa kumpongeza Mheshimiwa Mbunge Abdallah Njwayo kwa mchango wake mkubwa wa kuhamasisha masuala ya *sulphur* kwa ajili ya zao korosho na maendeleo ya Mtwara kwa ujumla.

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa mjadala huu, Mheshimiwa Naibu Waziri amezungumzia juu ya suala hili la korosho na kwa kuwa kwa sasa hivi hali ya ununuzi wa korosho katika Mikoa ya Kusini ni mbaya sana sana, hiyo *curtail* aliyoizungumzia Mheshimiwa Waziri hasa hasa inawaumiza wakulima. Je, Serikali inatoa tamko gani kuhusu bei ya korosho? Je, inunuliwe kwa Sh.600 au Sh.500 kwa kilo wanazokazania hao wana-*curtail*?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mipango na Uwezeshaji kwa majibu yake mazuri sana. Pili, nikubaliane na Mheshimiwa Njwayo na Mheshimiwa Mrope kwamba lipo tatizo kubwa la ununuzi wa korosho katika Mikoa ya Lindi na Mtwara. Serikali inalifahamu suala hili na Waheshimiwa Wabunge wanajua tumekuwa na vikao vya majadiliano. Lakini kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri ni kweli kwamba wanunuzi wa korosho wameweka utaratibu wa *curtail* wa kuwaumiza wakulima. Hatukubaliani na *curtail* hiyo na Serikali inaahidi kuchukua hatua zinazopaswa  Bei ambayo wamekubaliana wale wanunuzi na wakulima ni Sh.600 kwa kilo ndio msimamo wa Serikali na maamuzi hayo yaheshimiwe na hao wanaotaka kununua korosho. *(Makofi)*

Na. 44

**Ahadi ya Kujenga Madaraja na Barabara**

**MHE. HASSAN CHANDE KIGWALILO** aliuliza:-

Kwa kuwa wakati wa kampeni za uchaguzi mkuu wa mwaka 2005, Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Nne aliwaahidi wananchi wa Liwale kuwa Serikali itajenga daraja la Mto Ruhuhu kwenye barabara ya Liwale kwenda Lilombe hadi Tunduru na kuboresha barabara ya Nangurukuru kwenda Liwale hadi Nachingwea ili ziweze kutumika wakati wote.

(a) Je, ni lini ahadi hizo zitaanza kutekelezwa?

(b) Je, isingekuwa vema kwa Serikali kuweka makambi ya ujenzi katika barabara korofi nchini ikiwemo ya Nangurukuru – Liwale – Nachingwea kwa lengo la kurekebisha sehemu korofi papo kwa papo ili barabara hizo ziweze kupitika wakati wote.

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Miundombinu, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Hassan Chande Kigwalilo, Mbunge wa Liwale, lenye sehemu (a) na (b), napenda kutoa maelezo yafuatayo:-

Barabara ya Liwale – Lilombe yenye urefu wa kilometa 64 inahudumiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Liwale.

Aidha, Wizara yangu inatambua umuhimu wa barabara ya Nangurukuru – Liwale (km.231) na Liwale – Nachingwea (km.136) kwa ajili ya maendeleo ya Wilaya ya Liwale na kwa kuzingatia umuhimu huu, Wizara yangu kupitia Ofisi ya Wakala wa Barabara *(TANROADS)* Mkoa wa Lindi imekuwa ikizifanyia ukarabati barabara hizi katika maeneo korofi kulingana na upatikanaji wa fedha kama ifuatavyo:-

(i) Barabara ya Nangurukuru – Liwale, kati ya mwaka 2002/2003 hadi 2005/2006 jumla ya Sh. 417.7m/= zimetumika katika ukarabati na matengenezo ya sehemu korofi zenye jumla ya urefu wa kilomita 40.4. Aidha, jumla ya Sh.113m/= zimetumika kukarabati madaraja ya Njinjo, Zinga Kibaoni, Kilongo, Kimambi na Nangale.

Katika mwaka wa fedha wa 2006/2007, Sh. 131.287m/= zimetengwa kwa ajili ya kufanyia matengenezo sehemu korofi yenye urefu wa kilomita 9.4 katika barabara hii.

Vile vile, barabara hii itaendelea kufanyiwa matengenezo ya kawaida katika urefu wake wote.

(ii) Barabara ya Nachingwea – Liwale. Kuanzia mwaka 2000/2001 na mwaka 2003/2004 jumla ya shilingi 193 milioni zilitumika kufanyia matengenezo sehemu korofi zenye jumla ya kilometa 22 za barabara hii na shilingi 30 milioni zilitumika kwa ajili ya matengenezo ya daraja la Kibutuka.

Aidha, barabara hii ni kati ya barabara zinazokarabatiwa kwa kiwango cha changarawe (*engineered gravel standard*) katika mradi maalum wa kukarabati barabara za Mkoa wa Lindi zenye urefu wa kilomita 114 chini ya ufadhili wa *OPEC* na Serikali ya Tanzania.

Chini ya mradi huu kipande chenye urefu wa kilomita 13 kati ya Liwale na Mikunya kitajengwa kwa kiwango cha changarawe katika mwaka huu wa fedha. Mkandarasi wa kufanya kazi hiyo ameshapatikana na yupo katika maandalizi ya kuanza kazi (*site-mobilization*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo hayo, sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hassan Chande Kigwalilo, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwa kuwa barabara ya Liwale – Lilombe, inahudumiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Liwale ambayo Mheshimiwa Mbunge ni mjumbe wa Baraza la Madiwani, nashauri Halmashauri iangalie uwezekano wa kutumia sehemu ya mgao wa fedha za Mfuko wa Barabara (*Roads Fund*) wanayopata ili kutimiza ahadi ya Mheshimiwa Rais. Kuhusu barabara zinazohudumiwa na Wizara yangu, ukarabati na matengenezo yamekuwa yakifanyika kama nilivyosema kwenye maelezo ya utangulizi hapo juu.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali haina mpango wa kuweka makambi ya ujenzi katika barabara korofi nchini kwa kuwa kazi za barabara kwa sasa zinafanyika kwa kuwatumia wakandarasi ambao hujenga makambi ya muda wakati wa utekelezaji wa mradi husika.

Hata hivyo, kuna mkakati unaandaliwa wa kutoa kandarasi za muda mrefu kwa mkandarasi kufanyia matengenezo ya barabara husika kwa kipindi kirefu (mfano miaka mitano). Kwa hali kama hii, Mkandarasi ataweza kuona umuhimu wa kujenga kambi

kwenye baadhi ya maeneo hasa yasiyokaliwa na watu ili kumrahisishia kazi, hususan katika kupunguza gharama za kusafirisha vibarua na hivyo kujiongezea tija.

**MHE. HASSAN C. KIGWALILO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri yaliyotolewa na Naibu Waziri. Naibu Waziri haoni kwamba tayari katika Awamu ya Tatu tulishapitisha katika *RC*C ya Mkoa wa Lindi kwamba barabara inayotoka Liwale kuelekea Tunduru kupitia Mto huo Ruhuhu iko katika ngazi ya Mkoa? Sasa hivi jibu lake linadhihirisha kwamba hakuna mawasiliano yoyote yaliyofanywa kati ya Awamu ya Tatu na Awamu ya Nne, suala hili mimi kwangu naliona gumu naomba Serikali ifuatilie vizuri katika ofisi zake kuona jibu linapatikana kwa ajili ya utatuzi wa daraja la Mto Ruhuhu kwa barabara inayokwenda Tunduru.

La pili, maelezo yanayohusu barabara kutoka Liwale kwenda Nachingwea. Pamoja kwamba majibu haya ni mazuri je, Serikali inaelewa hadi hivi leo hakuna kitu chochote kinachofanyika katika kutengeneza kilomita tisa au kumi na tatu ambazo zimepangwa kutengenezwa katika kipindi hiki katika sehemu ile ya mchanga katika barabara ya kutoka Liwale kwenda Nachingwea na hawa makandarasi wanaozungumziwa kusema kweli wamepeleka magreda yao na kila kitu Nachingwea huu ni mwezi wa pili na hakuna kinachoendelea?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, kuhusu mapendekezo ya *RCC* ya kupandisha daraja barabara ya Liwale hadi Lilombe kwamba iwe ni ya Mkoa badala ya kuhudumiwa na Halmashauri ni kwamba maombi kama haya yapo mengi sana katika Wizara na ule mchakato wa kuamua sasa ni barabara zipi zipandishwe daraja haujakamilika. Mimi nadhani Mheshimiwa Mbunge angesubiri kama ambavyo tumekuwa tukijibu kwamba tutakapoleta Sheria ya Barabara ndipo tutakapoona ni barabara zipi zimekubalika zipande na zipi zimekubalika zishuke. Kwa sasa hivi kwa mujibu wa sheria iliyopo barabara ile bado inahudumiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Liwale.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili la kipande cha kilomita kumi na tatu ambacho nimesema kwamba maandalizi yapo mbioni nimweleze Mheshimiwa Mbunge tu kwamba, kwa taarifa ambazo nimezipata mpaka jana hii kazi ya *site mobilization* imeanza na hao makandarasi hivi karibuni wataanza hiyo kazi. Lakini kwa sababu Mheshimiwa Mbunge amelalamika tutafuatilia tena tuhakikishe kwamba kweli hii kazi inaanza upesi iwezekanavyo.

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi naomba niongeze swali la nyongeza kama ifuatavyo. Kwa vile swali la msingi liligusia kivuko cha mto Ruhuhu na kwa vile kati ya Wilaya ya Mbinga na Ludewa kuna kivuko ambacho kiliwekwa mwaka jana. Kivuko hiki kinafanya kazi kwa shida sana na kinashindwa kuwahudumia wananchi wale wa Ludewa na wananchi wa Mbinga na licha ya kwamba kivuko cha awali kilichozama pale kwenye Mto Ruhuhu hakijaibuliwa mpaka leo kinaoza pale chini. Je, Wizara hii itatueleza ni lini itahakikishwa kwamba kivuko cha Mto Ruhuhu kati ya Mbinga na Ludewa kinafanya kazi kwa ufasaha kuwawezesha wananchi kuvuka mahali hapo kwa usalama? Ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kivuko kile pale Mto Ruhuhu kati ya Wilaya ya Mbinga na Ludewa kipo katika hali mbaya na mimi mwaka huu nilitumia kivuko kile tukiwa na Mheshimiwa Komba na Mheshimiwa Kayombo na tuliona jinsi ambavyo kweli ni shida kwa sababu kinatumia nguvu za binadamu kwa kuvuta kamba. Lakini kama ambavyo tumeshawahi kujibu katika Bunge hili kivuko katika Mto ule kiko katika mpango wa kununuliwa. Kwa hiyo, suala ni kwamba sasa tuharakishe tu ununuzi wa kivuko kile kama ambavyo imeahidiwa kwenye bajeti.

Na. 45

**Usafiri wa Ndege Dodoma**

**MHE. MARTHA M. MLATA** aliuliza:-

Kwa kuwa Dodoma ni Makao Makuu ya Serikali pamoja na Makao Makuu ya nchi na kwa kuwa mahitaji ya usafiri wa ndege yanaongezeka hasa wakati wa vikao vya Bunge na kwa kuwa kwa sasa hakuna usafiri wa uhakika wa ndege toka Dodoma kwenda Dar es Salaam na sehemu nyingine nchini zenye usafiri wa ndege:-

(a) Je, Serikali ina mikakati gani ya kuwezesha upatikanaji wa usafiri wa uhakika wa ndege kwa wakazi wa Dodoma?

(b) Je, ndege za Serikali zilizoko chini ya Wakala wa Ndege za Serikali zinaweza kutoa huduma ya usafiri kwa kushirikiana na ndege za Mashirika binafsi?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Martha Moses Mlata, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Wizara ya Miundombinu kupitia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania *(TAA)* ina mkakati wa kujenga Kiwanja kipya cha ndege kitakachowezesha Dodoma kupata usafiri wa ndege wa uhakika.

Wizara ya Miundombinu kwa kushirikiana na Mamlaka mbalimbali za Mkoani Dodoma, imeshapata eneo litakalokidhi ujenzi wa kiwanja hicho, eneo la Msalato nje kidogo ya Manispaa ya Dodoma.

Mwezi Juni, 2006, Serikali ya Tanzania ilipata msaada wa fedha kutoka Benki ya Mandeleo ya Kiarabu *(BADEA)* kiasi cha Dola za Kimarekani 440,000 kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu na usanifu kwa ajili ya ujenzi wa kiwanja kipya cha ndege cha Dodoma sehemu ya Msalato. Kiwanja hiki kitakuwa na miundombinu yenye kukidhi matumizi ya ndege kubwa aina ya *Boeing* 737.

Zabuni za upembuzi yakinifu na usanifu wa kiwanja hicho kipya, tayari zimetumwa kwa makampuni ya usanifu tangu 13 Oktoba, 2006 na zitarejeshwa ifikapo Desemba 1, 2006. Lengo ni kupata kampuni yenye utaalamu wa kufanya kazi hiyo. Aidha, Benki ya Maendeleo ya Kiarabu *(BADEA)* imeonyesha nia ya kutoa mkopo wenye riba nafuu kwa ajili ya ujenzi wa kiwanja hicho mara baada ya kukamilika kwa upembuzi yakinifu na usanifu. Matumaini ya Wizara ni kuwa baada ya kukamilika kwa ujenzi wa kiwanja kipya cha ndege, wakazi wa Dodoma watakuwa na uhakika wa huduma ya usafiri wa ndege.

Aidha, wakati mchakato wa ujenzi wa kiwanja kipya unaendelea, Wizara ya Miundombinu kupitia Mamlaka ya viwanja vya Ndege, itafanya matengenezo ya miundombinu ya kiwanja cha sasa ikiwa ni pamoja na kuweka taa za kuongoza ndege ili kuwezesha ndege kuruka na kutua salama hata nyakati za usiku. Kiwanja cha Ndege cha Dodoma kina uwezo wa kuruhusu ndege aina ya *Fokker* au *ATR* zinazobeba wastani wa abiria 50 kutua. Wizara kupitia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege itaendelea kufanya matengenezo ya mara kwa mara ili huduma za ndege katika kiwanja ziendelee kuwa za usalama.

(b) Mheshimiwa Spika, kimsingi, ndege za Wakala wa Ndege za Serikali, zinaweza kutoa huduma za usafiri wa anga pale ambapo nafasi kama hiyo inatokea. Huduma kama hizo zinaweza kutolewa na Wakala yenyewe au kwa kushirikiana na sekta binafsi.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwanza kabisa namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa jibu lake zuri na nina maswali mawili madogo ya nyongeza. Swali la kwanza, pamoja na kwamba amesema kuna mipango ya kujenga kiwanja kipya cha ndege hapa Dodoma lakini inavyoonyesha kiwanja hicho kitakuwa na ndege za hapa nchini. Sasa nataka kumwuliza Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba, je, Serikali sasa haioni umuhimu wa kujenga kiwanja kikubwa zaidi cha Kimataifa ili kuufanya Mkoa wa Dodoma kuwa na hadhi ya Makao Makuu ya Nchi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, swali la pili, je, ni kwa nini Serikali ilipopanga kuufanya Mkoa wa Dodoma kuwa Makao Makuu ya Nchi Wizara haikuona umuhimu wa kuweka mpango madhubuti wa kujenga kiwanja cha Kimataifa hapa Dodoma kwa kuzingatia hadhi ya Makao Makuu ya nchi mpaka ikumbushwe? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, kwamba kiwanja kinachojengwa hicho kiwe cha Kimataifa ni kwamba nimesema katika jibu la msingi kwamba kiwanja hicho kitakuwa ni kikubwa, kitakuwa na uwezo wa kuhudumia ndege za *Boeing* 737. Kwa maana hiyo kitakuwa ni kiwanja kikubwa. Kwamba sasa kiwe ni cha Kimataifa itategemea na mazingira ambayo kiwanja kile na miundombinu mingine ambayo ipo katika kiwanja hicho kipya kukidhi matakwa ya kiwanja kuwa cha Kimataifa lakini kitakuwa ni kikubwa ambacho kinaweza kuhudumia ndege kubwa kama *Boieng* 737.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kwamba Serikali kwa nini haikupanga mipango hii toka awali. Kama tunavyoelewa uamuzi wa kuweka Makao Makuu ya Serikali Dodoma unakwenda kwa awamu. Kwa hiyo, si kwamba Serikali ndiyo imekumbushwa sasa kuhusu suala la uwanja wa ndege, mipango mingine yote imekwenda kwa awamu na wala siyo suala la uwanja tu ambalo halijatekelezwa katika suala zima la kuhakikisha kwamba Dodoma inakuwa Makao Makuu, kuna mambo mengi ambayo yanakwenda kwa awamu kutegemea na fedha na uwezo wa Serikali kufanya hivyo.

Na. 46

**Ujenzi wa Gati za Kisasa Kigoma**

*(Swali lililotajwa hapo juu liliondolewa kwa idhini ya mwuliza swali kwa sababu lilijibiwa katika mkutano uliopita)*

Na. 47

**Muda wa Askari wa Kukaa katika Kituo Kimoja cha Kazi**

**MHE. DR. HAJI MWITA HAJI** aliuliza:-

Kwa kuwa Sheria, Kanuni au Taratibu za Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ni kwamba, Wanajeshi wanapopangiwa kazi katika kambi fulani wanatakiwa kuwepo katika vituo hivyo kwa muda wa miaka mitano mitano na kuhamishiwa sehemu nyingine ili wapate uzoefu fulani, lakini baadhi ya Askari hao hubakia katika kambi moja hadi miaka kumi (10) au zaidi bila kuhamishwa:-

(a) Je, ni sababu gani zinazowafanya Askari kubakia katika kambi kwa muda mrefu bila ya kuhamishiwa sehemu nyingine muda ulipofika?

(b) Je, kumweka Askari, katika sehemu moja kwa muda mrefu kituoni kunaweza kumfanya Askari azoee sana mazingira kiasi cha kutojali utendaji mzuri wa kazi zake?

(c) Je, kuna mpango gani wa kutekeleza mpango huo wa uhamisho kama utaratibu au kanuni za kijeshi zinavyotaka?

**NAIBU WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Haji Mwita, Mbunge wa Jimbo la Muyuni, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa sheria na kanuni za Jeshi la Wananchi wa Tanzania, hakuna muda maalum uliowekwa kwa wanajeshi kuishi sehemu moja. Aidha,

wanajeshi wanaweza kuishi sehemu moja kwa muda mrefu. Hali hii inatokana na majukumu pamoja na muundo wa vikosi walipo. Kwa mfano, vikosi vya kiufundi (ndege, wanamaji, vifaru, karakana na kadhalika), wanajeshi wake hawawezi kuhamishwa kwenda kwenye vikosi vingine kutokana na utaalam walionao. Wanaweza kupelekwa vyuoni ili kuwa wakufunzi wa utaalam wao.

(b) Mheshimiwa Spika, askari kukaa sehemu moja kwa muda mrefu ni moja kati ya misingi mikubwa katika maisha ya wanajeshi. Kukaa kwake katika kituo kimoja kwa muda mrefu, kunamfanya apate mafunzo ya mara kwa mara yanayolingana na majukumu yake ambayo yanasaidia katika kuleta uelewano na ufanisi katika utekelezaji wa majukumu. Aidha, wanajeshi wanapoishi pamoja kwa muda mrefu wanapata nafasi ya kuelewa uwezo wa kila mmoja wao, hivyo ni rahisi kusaidiana.

(c) Mheshimiwa Spika, utaratibu uliopo wa kuhamishwa kwa wanajeshi na ambao unafuatwa ni ule unaotokana na mahitaji ya kuziba mapengo baada ya wanajeshi wa sehemu moja kustaafu, kufa au kujaza muundo wa kikosi.

Mheshimiwa Spika, ni vema ikaeleweka kuwa, kuwahamisha wanajeshi mara kwa mara kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine nako kuna gharama zake. Jeshi lazima liwe na fedha za kutosha.

**MHE. DR. HAJI MWITA HAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Kwa mujibu wa maelekezo ya Mheshimiwa Waziri nimefahamu vizuri. Sasa ikiwa kama imetokea kwa dharura. Je, mwanajeshi anaweza kupewa ruhusa ya kuomba yeye mwenyewe kwa sababu maalum na anaweza kupata uhamisho huo? Ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, mwanajeshi akiwa anaumwa na kuumwa kwake kunatokana na mazingira ya eneo alipo mwanajeshi huyo anaweza kuomba ruhusa na akahamishiwa katika kambi ambayo ipo katika eneo lingine, lakini vinginevyo mwanajeshi huyo ataendelea kukaa katika kikosi hicho alipo.

**MHE. FAIDA MOHAMMED BAKAR:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa katika mpango wa kuhamisha askari kutoka kituo kimoja kwenda kingine ni mzuri lakini umetawaliwa na usumbufu wa malipo ya uhamisho wa askari husika. Je, Serikali haioni kwamba huko ni kusababisha usumbufu kwa askari hao?

**NAIBU WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, askari yeyote anayehamishwa kwenda katika kikosi kilichoko sehemu nyingine anastahili posho zake kulipwa na inapotokea kwamba amechelewa kulipwa siyo kwamba hatalipwa, hapana, atalipwa kwa sababu hiyo ni haki yake na kama kunakuwa na usumbufu basi tunawaomba radhi wanajeshi hao.

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali. Katika miaka ya 70 na 80 askari wengi wanajeshi wazalendo walipelekwa kutetea nchi yetu pamoja na kupigania uhuru wa nchi jirani kama vile Msumbiji, Afrika Kusini, Angola na hata Sychelles na Uganda. Askari wengi kati ya hao pia hawakurudi nyumbani na mpaka leo wanasubiriwa na familia zao na inahofiwa kwamba pengine walipoteza maisha yao. Je, Serikali ina mpango gani wa kutangaza hao askari mashujaa ili wafahamike na Taifa kwamba basi endapo walipoteza maisha yao walizikwa wapi na kama hawakuzikwa basi majina yao yatajengewa mnara wapi ili waendelee kufahamika kama watu mashujaa waliotumikia nchi yetu? Hilo linakwenda sambamba na kuwalipa familia zao fidia ya maisha yao. Pia Serikali yetu ina mpango gani wa ku............

**SPIKA:** Mheshimiwa Wangwe nimekuvumilia tu kwanza swali ni *out of order*, swali la nyongeza halihusiani kabisa na swali la msingi ambalo linahusu askari kukaa katika vituo kwa muda mrefu na uhamisho wao. Wewe unauliza waliokufa vitani ambacho ni kitu kingine tofauti. Tunaendelea Waheshimiwa Wabunge na Wizara hiyo hiyo. Mheshimiwa Col. Saleh Ali Farrah, Mbunge wa Raha Leo.

Na. 48

**Malipo kwa Wazabuni Wanaohudumia Vikosini**

**MHE. COL. SALEH ALI FARRAH** aliuliza:-

Kwa kuwa Wizara ya Fedha inakasimia Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ambapo fedha huombwa kwa matumizi ya kawaida kama mishahara na chakula kwa Askari wote na kwa kuwa vikosi huingia Mikataba na wazabuni walio na uwezo wa kulisha vikosi kulingana na viwango vya ubora wa lishe jeshini:-

(a) Je, kwa nini vikosi husika havilipi wazabuni wao hata baada ya kupokea huduma toka kwa wazabuni pamoja na wazabuni hao kuwa na hati safi za madai yao?

(b) Je, ni lini wazabuni hawa wafuatao *Al-Amin Gerneral Traders, Nassor Traders, Kikwajuni Store, Mahusiano Store, Unguja Ukuu Store* watalipwa madai yao yenye jumla ya Tshs. 39,981,000/= kama kweli hayana udanganyifu wowote?

(c) Je, kama mzabuni atashindwa kutoa huduma ya chakula kwa Askari kutokana na kucheleweshewa malipo yake ni nani atalaumiwa katika kadhia hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, napenda kujibu swali la Mheshimiwa col. Saleh Ali Farrah, Mbunge wa Jimbo la Raha Leo lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli Jeshi la Wananchi wa Tanzania lina madeni ya wazabuni, lakini madeni hayo ni yale yaliyokuwepo kabla ya mwaka wa fedha

2001/2002 ambayo yalitokana na utaratibu wa zamani wa utoaji huduma Jeshini ambao ulikuwa ni kununua vyakula vibichi kutoka kwa wazabuni na Jeshi kujipikia wenyewe. Tokea mwaka 2001 tuliapoanzisha utaratibu ambao unaendelea sasa wa utoaji huduma kwa kuponi, hakuna deni linalodaiwa na wazabuni. Tulishindwa kulilipa deni la nyuma lote kutokana na ufinyu wa bajeti. Hata hivyo, sehemu ndogo ya deni hilo tunaendelea kuilipa kwa awamu.

(b) Mheshimiwa Spika, Wizara inaendelea kuwasiliana na Wizara ya Fedha ili madeni ya Wazabuni yaliyotajwa na Mheshimiwa Mbunge amewataja ni sehemu ya deni la Tshs. 185,468,112.30 kwa Kanda ya Zanzibar pamoja na madeni mengine yaweze kulipwa katika muda mfupi ujao. Pia Wizara inaangalia uwezekano wa kulimaliza deni hilo kutoka katika bajeti ya mwaka huu endapo hali ya fedha itaruhusu.

(c) Mheshimiwa Spika, wazabuni wote wanaotoa huduma kwa utaratibu wa kuponi kuanzia Julai, 2001 wamekuwa wakilipwa mara baada ya kutoa huduma na kuwasilisha Ankara za madai. Kama nilivyotangulia kusema kwamba, tangu utaratibu wa utoaji huduma kwa kuponi ulipoanza, hakuna mzabuni yeyote anayelidai jeshi, madeni yaliyopo ni ya nyuma, kabla ya mwaka 2001. Aidha, napenda nisisitize kwamba, Jeshi litajitahidi kuhakikisha kuwa hakuna mzabuni yeyote atakayeshindwa kutoa huduma Jeshini kutokana na kutolipwa fedha zake.

Na. 49

**Upimaji wa Mashamba ya Wananchi**

**MHE. AHMED ALLY SALUM** aliuliza:-

Kwa kuwa moja kati ya mipango ya kuwawezesha wananchi kiuchumi ni kurasilimisha mali zisizokuwa rasmi ili ziweze kutambulika kisheria hasa kwa wakulima wa Vijijini ili waweze kupata hati za mashamba zitakazowawezesha kupata mikopo ya kuwasaidia katika shughuli zao za kilimo kwa lengo la kuinua kipato chao na pato la Taifa kwa ujumla:-

(a) Je, Serikali haioni umuhimu wa kutoa kipaumbele katika upimaji wa mashamba ya wakulima kwanza ili wakulima waweze kukopa kwa lengo la kukuza kilimo cha kisasa chenye tija?

(b) Je, Serikali itafanya mikakati gani ya kuvifanya vyombo vya fedha kutoa mikopo kwa masharti nafuu?

(c) Je, mikakati ya kupima mashamba ya wakulima katika Jimbo la Solwa itaanza lini?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ahmed, Mbunge wa Solwa, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali imeweka kipaumbele katika upimaji wa ardhi Mijini na Vijijini ikiwa ni kanuni ya msingi ya kurasimisha ardhi ili itambulike kisheria na kuwanufaisha wananchi walio wengi. Jukumu hili ni utekelezaji wa Sheria ya Ardhi Na. 4 ya mwaka 1999 na Sheria ya Ardhi ya Vijiji Na. 5 ya mwaka 1999. Serikali imetoa mamlaka kwa Halmashauri za Miji na Wilaya kupima viwanja na mashamba. Vile vile kazi hiyo inafanywa na wapimaji binafsi wanaotambulika kisheria. Aidha, Serikali za Vijiji zimepewa mamlaka ya kutoa hati za haki miliki za kimila. Utaratibu huu unasogeza huduma kwa wananchi badala ya kuifuata Makao Makuu ya Wizara, Mkoa au Wilaya. Serikali inajenga uwezo wa kutekeleza kazi hizo katika ngazi za Vijiji ili wanavijiji kwa kushirikiana na wataalam wa Halmashauri za Miji na Wilaya zao waweze kupima Vijiji na mashamba yao.

(b) Mheshimiwa Spika, vyombo vya fedha, huendesha shughuli zake kibiashara kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu zilizowekwa. Serikali imeweka mazingira bora kwa pande zote (mkopaji na mkopeshaji) ili kuhakikisha haki inatendeka. Mikakati iliyoandaliwa ni pamoja na kupitishwa kwa Sheria ya Mabenki ya Mwaka 2006, kuruhusu kuanzishwa kwa mabenki mengi na taasisi za fedha kufanya shughuli za kibenki na juhudi zinaendelea kupunguza riba kwa wakopaji. Aidha, kwa mujibu wa Sera ya Mikopo midogo midogo (*Micro-finance Policy*) ya mwaka 2000 inahimiza wananchi kujiunga katika vikundi vidogo vidogo vya *SACCOS* ili waweze kupata huduma mbalimbali za kifedha ikiwemo mikopo iliyo nafuu.

(c) Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri za Miji na Wilaya zinaendelea na upimaji wa Vijiji na mashamba ya wanavijiji nchini. Kazi hii inafanyika kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha. Wizara ilichagua Wilaya za mfano ili Wilaya zingine ziweze kuiga. Kazi nzuri ilifanyika katika Wilaya za Mbozi na Iringa Vijijini ambazo zilichaguliwa kuwa za mfano. Katika Wilaya hizo elimu kuhusu matakwa ya sera na Sheria za Ardhi ilitolewa, masijala za ardhi zilijengwa na utoaji wa Hati za Hakimiliki za kimila ulifanyika.Kazi ya kurasimisha ardhi ya Mijini na Vijijini na hatimaye kuyapima maeneo yote ili wananchi walio wengi waweze kukopesheka haiwezi kufanywa na Wizara peke yake. Hivyo, Halmashauri kupitia Wilaya za mifano zinatakiwa kuhamasika na kuifanya kazi hiyo wenyewe. Ni vema Mheshimiwa Mbunge akashirikiana na Halmashauri ya Wilaya yake katika kuwahamasisha wananchi kutekeleza jukumu hilo.

**MHE. AHMED A. SALUM:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Kwa kuwa hati hizi za mila hupimwa na Halmashauri na mara nyingi hati hizi si rahisi kutambulika na mabenki binafsi katika utoaji wa mikopo katika suala zima la MKURABITA. Je, Serikali inalijua hilo na kama inalijua hilo imelifanyia kazi vipi hili hizi hati za mila ziweze kutambulika na wananchi waweze kupata mikopo?

Swali la pili, kwa kuwa taarifa ambazo nimezipata hivi karibuni ni kwamba Mkoa mzima wa Shinyanga ni Vijiji 150 tu vitakavyopimwa. Jimbo la Solwa lina Vijiji 116 na ili kwenda sambamba na kasi hii mpya ya MKURABITA ili sasa MKUKUTA uweze kufanya kazi yake vizuri na kwa kuwa *SACCOS* peke yake si rahisi kukidhi mahitaji ya wananchi wengi wenye kuhitaji mikopo kwa nini isiongeze kasi mpya ili upimaji wa Vijiji na rasilimali ya wananchi wa Jimbo la Solwa na wananchi wa Tanzania nzima kwa ujumla ufanyike ili wananchi wapate mikopo haraka? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli Serikali imegundua kwamba mabenki mengi hayakubali kutoa mikopo na hii imewapa wasiwasi wananchi wengi ambao wameishapimiwa mashamba yao. Tulilifuatilia hili suala katika Wilaya ya Mbozi na tumeongea na mabenki kadhaa ikiwemo *EXIM Bank* na tayari imeishakubali na imewapa mikopo kwa kutumia hatimiliki za kimila wakulima watatu na tayari wamekwishaanza kazi zao. Bado Serikali inaendelea kufanya mazungumzo na Benki ya *CRDB* na *NMB* ili kuhakikisha kwamba wanatambua hati hizi.

Mheshimiwa Spika, vilevile Serikali itajaribu kupima vijiji kwa kasi inavyowezekana na katika mwaka huu wa fedha tumesema tutapima vijiji 3,104 vikiwemo vijiji vya Mkoa wa Shinyanga 150 na hapo hapo tuliwahi kupima katika Mkoa wa Shinyanga vijiji 208.

Mheshimiwa Spika, ningeomba Mheshimiwa Mbunge akubaliane na Serikali kwamba kupima kijiji kimoja ni fedha nyingi yapata bilioni moja na laki tano. Kwa hiyo, Serikali inajaribu kupima kwa kasi kutokana na uwezo ambao Serikali inao.

Na. 50

**Upimaji na Utoaji wa Hati Miliki ya Nyumba**

**MHE. JAMES P. MUSALIKA** aliuliza:-

Kwa kuwa Ilani ya Uchaguzi ya CCM 2005/2010 inaeleza kuwa kutakuwa na utekelezaji wa mkakati wa kurasimisha Rasilimali na Biashara Tanzania (MKURABITA) kwa lengo la kuwawezesha Watanzania kurasimisha ardhi na nyumba zao ili waweze kuzitumia kupata mikopo kutoka Benki na kwenye Mifuko mingine ya fedha inayokopesha na kwamba Benki hizo zitaandaliwa ipasavyo ili zitambue rasilimali hizo katika kutoa mikopo hiyo:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kupima na kutoa hati miliki ya ardhi kwa wananchi wa Kata za Busolwa, Shabaka, Nyang'hwale, Mwingiro, Kakora, Nyungwa, Kharumwa, Kafita na Bukwimba ambao wanasubiri kwa shauku kubwa mpango huo?
(b) Kwa kuwa Mikoa ya Mwanza, Shinyanga, Mara, Kigoma, Tabora, Singida, Dodoma, Lindi, Mtwara na Rukwa iko nyuma kimaendeleo na watu wake ni maskini

sana ila wanayo ardhi na nyumba pia: Je, Serikali ina mpango gani wa makusudi wa kuanza kutekeleza mpango wa upimaji ardhi katika maeneo hayo ili kuleta usawa?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa James Musalika, Mbunge wa Nyang'hwale, lenye sehemu (a) na (b) napenda kutoa maelezo mafupi kama yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa maelezo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 kifungu cha 42(a), Serikali inaelekezwa kutekeleza Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA). Mpango huu ni mkubwa na unahitaji ushirikishwaji wa wadau wengi. Serikali imemaliza utafiti wa kutambua matatizo dhidi ya urasimishaji wa rasilimali zilizokuwa kwenye mfumo usio rasmi wa kiuchumi. Kwa sasa Serikali inafanya tathmini ya matatizo na kutayarisha mapendekezo juu ya mfumo unaofaa kwa ajili ya urasimishaji. Mara kazi hii itakapokamilika Serikali itatekeleza mapendekezo yatakayokuwa yameainishwa.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu ni msimamizi wa Sera ya Taifa ya Ardhi ya mwaka 1995 , Sera ya Maendeleo ya Makazi ya Mwaka 2000, Mdhibiti Mkuu wa Upimaji Ardhi na utayarishaji wa Ramani na utayarishaji wa Mipango na Matumizi mbalimbali ya Ardhi Kitaifa Mijini na Vijijini. Lakini jukumu la kupanga matumizi ya upimaji ardhi liko chini ya Mamlaka ya Halmashauri za Jiji, Manispaa, Miji na Wilaya chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Aidha, Sheria ya Ardhi ya Vijiji Na. 5 ya 1999, inavipa Vijiji Mamlaka ya kusimamia ardhi yake na kuwawezesha wananchi au wanakijiji kupata hati za kimila.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo ya jumla sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, vijiji vyote alivyovitaja Mheshimiwa Mbunge vimepimwa. Katika mwaka 1999, Wizara iliweza kupima vijiji vyote katika Kata za Busolwa, Shabaka, Nyang'hwale, Mwingiro, Kakora, Nyungwa, Kharumwa, Kafita na Bukwimba, Wilayani Geita Mkoani Mwanza. Hivyo, ni jukumu la Halmashauri husika kutumia Sheria Na.5 ya Ardhi ya Vijiji katika kuhakikisha vijiji vilivyokwishapimwa vinapata Vyeti au Hati za kimila.

Aidha, sina takwimu zinazoonyesha kuwa wakazi wa Mikoa ya Mwanza, Shinyanga, Mara, Kigoma, Tabora, Singida, Dodoma, Lindi, Mtwara na Rukwa ni maskini sana kama alivyobainisha Mbunge. Mikoa iliyotajwa inayo mazao makuu ya kibiashara kama pamba, mifugo, samaki, mawese, tumbaku, karanga na kadhalika ambayo inawapatia wananchi fedha. Hata hivyo, suala la upimaji ardhi katika maeneo hayo litazingatiwa kulingana na upatikanaji wa fedha.

**MHE. JAMES P. MUSALIKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Namshukuru Naibu Waziri kwa majibu yake. Lakini napenda niulize maswali mawili madogo ya nyongeza kama ifuatavyo:-

La kwanza, kwa kuwa, wakati akijibu kifungu (a) amesema vijiji vyote katika Kata za Busolwa, Shabaka, Nyang'hwale, Mwingiro, Kakora, Nyungwa, Kharumwa, Kafita na Bukwimba vimepimwa; na kwa kuwa swali la msingi lilikuwa linahusu kurasimisha mashamba; na kwa kuwa mabenki yanatambua hatimiliki za ardhi na mashamba wala siyo hatimiliki za vijiji kama alivyojibu. Je, sasa anaweza akajibu swali langu la kupima ardhi na nyumba. Anaweza akajibu hilo sasa.

La pili, kwa kuwa wakati akijibu swali Namba 49 amesema kwamba benki ya *EXIM* imeishakubali utaratibu wa kukopesha wananchi kufuatana na Hatimiliki za ardhi zao. Je, katika Wilaya ya Geita ambako kuna benki ya *NMB* iko tayari sasa hivi kukopesha wananchi wakulima ambao watakuwa na hati za nyumba zao na mashamba? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, katika jibu la msingi nimesema kuwa tumepima vijiji vyote katika Wilaya ya Solwa na nimevitaja na mwisho nikasema kwamba Halmashauri ihakikishie kwamba inawapatia Hatimiliki za kimila. Labda nifafanue ili kumwelewesha Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Spika, tunapima vijiji na tunawapa vyeti, kijiji kina mashamba mengi na wananchi au wakazi wengi. Wale wakazi kila mmoja anahitaji kupimiwa shamba lake. Tukishawapimia sisi kama Wizara tunataka Halmashauri zijenge masjala za vijiji na katika masjala hizo ndiko ambako watashughulika sasa kuhakikisha kwamba wanawapimia wananchi mashamba. Labda Mheshimiwa Mbunge nimpe utaratibu ambao unaotakiwa kutumika wakati mwananchi anatakiwa kupata hatimiliki ya kimila. Anatakiwa kwenda kwa Mtendaji wa kijiji kuchukua fomu na alipie shilingi 500/= halafu kikao kitakaa cha kijiji kizima ambacho kitaamua kama kweli hilo shamba ni la huyo mwananchi au siyo. Hatimaye atajaza fomu 44 ambayo inapatikana kule kule Wilayani kwake na kuiwasilisha kwenye Halmashauri ya Kijiji na mapendekezo yatakayatolewa na Mkutano Mkuu wa kijiji ndipo hatimiliki itatolewa ambayo itasainiwa na wanavijiji na itakwenda kule Wilayani pia kusainiwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo ndipo wanaweza kupata hizo hati na kuweza kuzitumia. Lakini tatizo ambalo tumeliona katika Wilaya nyingi ambazo tumekwishapima vijiji ni kwamba wananchi hata zile fedha ambazo zinakisiwa kufikia shilingi 2000/= ili walipe wapimiwe mashamba yao wanakuwa hawana. Ningemwomba Mheshimiwa Mbunge awahamasishe Halmashauri wawasaidie wananchi zile fedha ndogo za kupima mashamba yao ili waweze kupata hatimiliki za kimila.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili, ni kweli NMB sasa tumeanza mazungumzo nao na Serikali inajitahidi kuwaonyesha umuhimu wa hatimiliki za kimila ili waweze kutusaidia kutoa mikopo. Japo kuna benki zingine zinasema umbali wa lile shamba na ile benki uwe umbali ambao wanaweza kufika kama kudai fedha zao

zikipotea. Lakini mazungumzo yanaendelea, tutajitahidi kusaidia ili zoezi la MKURABITA liweze kufanikiwa.

**MHE. MOHAMED R. ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa suala la MKURABITA limepewa kipaumbele katika Ilani ya Uchaguzi na sharti kubwa la Mpango mzima wa MKURABITA ni kwamba shamba lile lipimwe na hatimaye wananchi wapate hatimiliki ili hatimaye waweze kukopeshwa waendeleze maeneo yao. Tatizo ni kwamba katika Wilaya zetu hakuna vifaa vya kupimia *at least destromat* zipatikane ili kuharakisha utaratibu wa MKURABITA. Je, atakubaliana na mimi na hatua gani zitachukuliwa?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli suala la MKURABITA limepewa kipaumbele na tumeweka katika bajeti ya mwaka huu utekelezaji ambao unatakiwa kufanywa na kama mtakumbuka katika jibu langu la jana nilieleza kwamba vifaa havipo na ni vya gharama kubwa. Tunajitahidi sana Serikali kwa kupitia Wizara zake Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi pamoja na TAMISEMI tuweze kushirikiana kuweza kupata ruzuku ya kuweza kununua hivyo vifaa. Wizara yetu ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi imekwisha kuwasiliana na Wizara ya TAMISEMI na kuwaandikia kwamba tunawaomba wawapatie ruzuku Idara za Ardhi ili waweze kupata vifaa ili kuwezesha kupima ardhi kwa haraka iwezekanavyo.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Sauti haitoki kwa sababu ya raha ya jana ya kupata kura nyingi sana. Nawashukuru sana wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu jambo linalozungumziwa hapa kubwa ni MKURABITA na kwamba ardhi ichukuliwe kama mali ya mtu; na kwa kuwa wale wanaokopesha ni lazima wawe na uhakika ili mali iwe inabaki na yule mtu na isiwe ya wasiwasi; na kwa kuwa kumekuwa na matamshi ya Serikali mara nyingi juu ya kunyang'anya watu mashamba yao pamoja na viwanja vyao. Ni lini basi Serikali itaaacha matamshi hayo ili ardhi kweli itumike kama rasilimali ya kudumu kwa wakulima ambao ni maskini wanataka kuondoshwa katika janga hili la umaskini? Nataka jibu.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, na mimi nikimpongeza sana kwa furaha aliyokuwa nayo na ambayo kwa kweli imechangiwa sana na Chama cha Mapinduzi. Katika kutekeleza swali lake la nyongeza kuhusu hatua zinazochukuliwa na Serikali kuhusu MKURABITA.

Mheshimiwa Spika, ni kweli ninakubaliana na Mheshimiwa John Cheyo kwamba lengo kubwa la Sheria ya Ardhi Namba 4 ya mwaka 1999 na Sheria ya Ardhi, Namba 5 ya mwaka 1999 ilikuwa ni kuhakikisha kwamba ardhi inatambulika kama mali.

Katika hatua ambazo zimeanza kuchukuliwa na Serikali baada ya kupitisha hizo Sheria ni pamoja na kuhakikisha kwamba katika bajeti ya mwaka huu zaidi ya vijiji 3,104 vinapimwa katika nchi nzima na katika Mikoa ambayo kwa bahati mbaya vilikuwa havijapimwa kabisa ukiwemo Mkoa wa Tanga na Shinyanga vijiji 150 na vijiji vyote vilivyoko katika Mkoa wa Mbeya na sehemu zingine.

Mheshimiwa Spika, lakini katika kutambua hilo pia tumeanzisha kwa mujibu wa sheria hiyo Namba 5 ya vijiji kuhakikisha kwamba panapatikana Hati za kimila katika vijiji. Tumeanza na vijiji vya mfano, katika majibu mazuri sana yaliyojibiwa na Naibu Waziri, tumeanza na Iringa Vijijini, tuko Mbozi na tuko Handeni. Kwa hiyo, ningependa kutoa wito kwa Halmashauri ambazo zingependa kutoa hatimiliki kwa mashamba ya vijiji ili Hati zile ziweze kutumika waweze kwenda kujifunza kwenye Wilaya hizi tatu za mfano ili wajue ni namna gani Hati zinaweza zikatolewa katika mashamba na maeneo mbalimbali.

Kuhusu suala la kunyang'anya viwanja hilo ni suala la sheria na sisi sote tupo hapa kwa ajili ya kufuata sheria. Kwa hiyo, tutahakikisha sheria zinafuatwa, lakini katika kuzingatia haki za wananchi walio wengi.

Na. 51

**Upungufu wa Nafasi za Vyuo Vikuu**

**MHE. MZEE NGWALI ZUBEIR** aliuliza:-

Kwa kuwa, idadi ya wanafunzi wanaomaliza kidato cha sita na wenye sifa za kujiunga na Vyuo Vikuu kwa mwaka 2005/2006 inakadiriwa kuwa 28,000 huku uwezo wa Serikali wa kudahili ni wanafunzi 11,000.

(a) Je, Serikali ina mkakati gani wa kuziba mwanya huo wa upungufu?

(b) Je, pengo hilo la upungufu linaleta athari kiasi gani?

(c) Je, tatizo hilo litaisha lini?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU YA JUU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir, Mbunge wa Mkwajuni, naomba kufanya marekebisho kidogo ya kitakwimu. Kwa mwaka masomo wa 2005/2006 idadi ya wahitimu wa kidato cha sita ilikuwa ni 21,126 na siyo 28,000 kama ilivyoelezwa katika swali. Vilevile, uwezo wa Vyuo Vikuu wa kudahili kwa mwaka huo ilikuwa ni wanafunzi 19,296 na siyo 11,000.

Mheshimiwa Spika, baada ya kufanya marekebisho hayo ya kitakwimu, naomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir, Mbunge wa Kikwajuni, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kuwa tatizo la upungufu wa nafasi za kujiunga na Vyuo Vikuu huenda litaendelea kujitokeza kwa kipindi cha miaka ijayo ikizingatiwa kuwa chini ya Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Msingi (MMEM) na Sekondari (MMES), wananchi wamehamasika sana kujenga shule nyingi ili kudahili wanafunzi wengi.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, napenda kumhakikishia kwamba Mheshimiwa Mbunge kwa Wizara yangu itaendelea na mikakati ya kupanua na kujenga Vyuo Vikuu vipya kutegemea na uwezo wa Serikali kifedha; na wakati huo huo kuhimiza taasisi binafsi kuanzisha Vyuo Vikuu na vya kati chini ya usimamizi wa Tume ya Taifa ya Vyuo Vikuu *(TCU)* na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi *(NACTE).*

(b) Mheshimiwa Spika, athari za pengo la upungufu wa wasomi wa Chuo Kikuu nchini ni pamoja na nchi kuendelea kuwa na wataalam wachache, kukosa ushindani katika ajira ndani ya dhama hizi za utandawazi, na hasa ikizingatiwa ya kwamba tuko katika karne ya Sayansi na Teknolojia.

(c) Uwezo wa Vyuo Vikuu kudahili katika mwaka huo ilikuwa ni wanafunzi 19,296 kama nilivyoeleza hapo awali. Uwezo huu ulizidi idadi ya wahitimu wa kidato cha sita waliokuwa na sifa ya kujiunga na Vyuo Vikuu katika mwaka huo 2005/2006 ambapo idadi yao ilikuwa ni 18,295 kati ya wanafunzi 21,126 waliokuwa wamehitimu kidato cha sita.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, pamoja na mambo mengine Wizara yangu imefanya na itaendelea kufanya yafuatayo kama mikakati ya kupanua nafasi ya masomo ya Elimu ya Juu ukizingatia ya kwamba wahitimu wa kidato cha sita wanazidi kuongezeka mwaka hadi mwaka.

Kwanza, ni kupanua nafasi za Elimu ya Juu kama ilivyofanywa kwa kuanzia Vyuo Vikuu Vishiriki vya *DUCE, MUCE, MUCCOBS* na kampasi mbili za Chuo Kikuu cha Mzumbe za DSM na Mbeya.

Pili, ni upanuzi wa miundombinu katika Vyuo Vikuu vya *DSM, SUA* na Chuo Kikuu cha Mzumbe.

Tatu, ni kuwavutia wawekezaji katika kuanzisha Vyuo Vikuu binafsi ambapo mpaka sasa kuna Vyuo Vikuu binafsi 13 na Vyuo Vikuu Vishiriki 6.

Nne, ni Chuo Kikuu Huria ambacho kimeanzishwa katika kila Mkoa na hivyo kutoa fursa kwa wanafunzi wengi kujiunga na Elimu ya Juu.

Tano, ni kupeleka na kusomesha wanafunzi katika nchi rafiki na zenye gharama nafuu kama vile India, Russia, China, Algeria na Afrika ya Kusini.

Sita, kuanzishwa kwa Bodi ya Mikopo ili kutoa mikopo kwa wanafunzi wanaosoma katika Vyuo vyote vya Elimu ya Juu. Hivyo hata wanafunzi wasio na uwezo watanufaika na mkopo utolewao na Bodi hii.

Aidha, ujenzi wa Vyuo Vikuu vipya, kama Chuo Kikuu Dodoma kitakachokuwa na uwezo wa kuchukua wanafunzi 40,000 kitakapokamilika.

Mheshimiwa Spika, aidha, napenda kuwaomba Waheshimiwa Wabunge wahamasishe wadau mbalimbali katika kuanzisha Vyuo Vikuu katika Mikoa yao.

**MHE. MZEE NGWALI ZUBEIR:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipatia nafasi hii kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Kutokana na majibu mazuri ya Naibu Waziri. Lakini taarifa hizi nimezipata katika taarifa ya Kamati ambapo wenyewe Wizara wamezitoa hizi taarifa. Kwa hiyo, kama ni takwimu inaonyesha Maafisa wake wamedanganya Kamati wakati ambapo wanatoa taarifa hiyo. Je, hili atalishughulikiaje wakati ambapo taarifa hizi tumezipata kwenye Kamati. Lingine ni kuwa tatizo kubwa ambalo linaukabili huu usajili au kuongeza wanafunzi katika Vyuo Vikuu vyetu ni matatizo ya mikopo ambapo wanakopeshwa ni wanafunzi. Hili ni tatizo kubwa ambalo linawakabili wanafunzi wakati wa kuingia kwenye Vyuo Vikuu na hili linaleta mgogoro mara zote wakati ambapo wanafunzi wanaochukuliwa ni *division one* ambapo ni wachache ambao wanaingia katika Vyuo Vikuu. Je, kuna mkakati gani wa kuongeza *division* ambapo wataingia wengi zaidi kuachana na hao wachache ambao wanapata *division one* na kuchukua waliopata *division two* na kuingia katika Vyuo Vikuu. Hili litachukuliwaje katika kuhakikisha kwamba wanafunzi wengi zaidi wanaingia katika Vyuo Vikuu ikilinganishwa na idadi ya sasa iliyopo.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU YA JUU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, lile la kwanza halikuwa swali. Kuhusiana na swali la kuongeza mikopo kwa *division* nyingine ili kuongeza udahili.

Mheshimiwa Spika, kama Mheshimiwa Mbunge angeweza kuvumilia swali linalofuata linazungumzia zaidi mikopo na nafikiri hapo angeweza kupata majibu sahihi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Kwa hiyo basi, tuendelee na swali hilo linalofuata kwa sababu yanahusiana.

Na. 52

**Mikopo kwa Wanafunzi wa Vyuo vya Elimu ya Juu**

**MHE. CHARLES N. KEENJA** aliuliza:-

Kwa kuwa, katika miaka ya hivi karibuni, Serikali imeamua kupanua utaratibu wa kutoa mikopo kwa wanafunzi wa Vyuo Vikuu ili kujumuisha wale wa Vyuo visivyokuwa vya Serikali lakini utekelezaji wa uamuzi huo umeghubikwa na matatizo mengi, malalamiko ya wadau, uchelewashaji wa mikopo na wanafunzi kupoteza muda mwingi kufuatilia mikopo hiyo na matamko yanayopingana yamezidi kusababisha malalamiko:-

(a) Je, mikopo hiyo ilikusudiwa kwa wanafunzi gani na ni maelekezo gani yaliyotolewa juu ya mikopo hiyo?

(b) Je, utaratibu wa kutoa mikopo hiyo unakabiliwa na matatizo gani, yanayotokana na nini na yameshughulikiwa namna gani?

(c) Je, Serikali imekuwa ikitenga kiasi gani cha fedha kila mwaka na kiasi hicho kinawatosha wanafunzi wangapi na wanafunzi hao ni asilimia gani ya wanafunzi walioko kwenye Vyuo vinavyohusika?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU YA JUU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Charles Keenja, Mbunge wa Ubungo, naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Serikali ilianza utaratibu wa uchangiaji gharama za Elimu ya Juu kwa njia ya mikopo ya wanafunzi kuanzia mwaka 1994/1995. Kuanzia kipindi hicho Serikali imekuwa ikitoa mikopo kwa wanafunzi wanaosoma Vyuo vya Elimu ya Juu vya Umma kwa ajili ya chakula na malazi. Mikopo hiyo ilikuwa ikisimamiwa moja kwa moja na Wizara ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia. Ili kuongeza ufanisi katika utoaji mikopo na kupanua wigo wa elimu ya juu kwa wanafunzi wengi zaidi, Bodi ya Mikopo ya wanafunzi wa Elimu ya Juu ilianzishwa kwa Sheria Na.9 ya 2004 na kuanza rasmi shughuli mwezi Julai, 2005. Majukumu ya Bodi hiyo ni kusimamia utoaji na urejeshwaji wa mikopo kwa wanafunzi wa Elimu ya Juu ikiwa ni pamoja na mikopo iliyotolewa na Serikali kuanzia mwaka 1994/1995.

Mheshimiwa Spika, baada ya utangulizi huo naomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa Charles Keenja, Mbunge wa Ubungo, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mikopo itolewayo na Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu imekusudiwa kwa wanafunzi wa Elimu ya Juu. Maelekezo yaliyotolewa juu ya mikopo hiyo yapo katika:-

(i) Sheria Namba 9 ya mwaka 2004 iliyoanzisha Bodi hiyo;
(ii) Kanuni *(Regulations);* na
(iii) Tamko la Serikali.

(b) Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kutoa mikopo hiyo wakati Bodi imeundwa umekabiliwa na matatizo yafuatayo:-

(i) Ufinyu wa bajeti;

(ii) Upungufu wa watumishi;

(iii) Uchache na uduni wa vitendea kazi; na

(iv) Baadhi ya wanafunzi kutokuwa waaminifu wakati wanapojaza fomu. Hata hivyo, katika kushughulikia matatizo hayo Serikali imefanya yafuatavyo:-

(i) Imeidhamini Bodi ya Mikopo kukopa fedha ili wanafunzi wengi zaidi wapate kunufaika na mikopo hiyo. Ongezeko hilo la mahitaji ya fedha limetokana na:-

- (i) Ongezeko la posho ya chakula na malazi;
- (ii) Ongezeko la muda wa mafunzo kwa vitendo kwa baadhi ya mitaala kutoka wiki sita kwenda wiki tisa;
- (iii) Idadi kubwa ya waombaji wenye sifa;

(ii) Bodi ya Mikopo sasa hivi ina watumishi 41 wenye uzoefu na masuala ya mikopo kutoka watumishi 7 walioanzisha Bodi hiyo na imepata kibali cha kuajiri watumishi wengine; na

(iii) Bodi sasa ina vifaa na vitendea kazi vya kisasa.

(c) Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa masomo wa 2005/2006 Bunge lako Tukufu liliidhinisha kiasi cha shilingi bilioni.32.5 b kwa Bodi ya Mikopo. Kiasi hiki hakikukidhi mahitaji ya wanafunzi wote waliotimiza masharti ya kupewa mikopo. Serikali ililazimika kuidhamini Bodi ili ikope kiasi cha shilingi bilioni 31 zaidi kutoka *PSPF* na hivyo kufanya mahitaji kufikia jumla ya shilingi bilioni 63.5 kwa mwaka wa masomo 2005/2006. Fedha hii ilikidhi mahitaji ya wanafunzi 42,729 sawa na asilimia 82.72 ya wanafunzi wote 51,657 waliokuwa katika Vyuo vyote vya Elimu ya Juu.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa masomo wa 2006/2007 Bunge lako Tukufu lilipitisha kiasi cha shilingi bilioni 63.5 ambapo kiasi hiki kilishindwa kukidhi mahitaji ya wanafunzi wote. Kwa mara nyingine Serikali imeidhamini Bodi ya Mikopo ili ikope shilingi bilioni 47.8. Hii imefanya mahitaji kufikia kiasi cha shilingi bilioni 111.3. Fedha hii itakidhi mahitaji ya wanafunzi 51,064 ambayo ni sawa na asilimia 75.07 ya wanafunzi wote 68,029 wanaosoma katika Vyuo vya Elimu ya Juu nchini.

**MHE. CHARLES N. KEENJA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuuliza maswali mawili madogo baada ya maelezo mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Wakati wa Kikao cha Bajeti hapa Bungeni Waziri alieleza kwamba kigezo kimoja cha kuwapa

wanafunzi mikopo ni kufaulu katika daraja la kwanza kwa wanaume na daraja la kwanza na pili kwa wanawake. Kwa viwango vyovyote duniani mwanafunzi anayefaulu kwa kiwango cha daraja la pili amefaulu vizuri inakuwaje asipewe mkopo wa kumwezesha aendelee na masomo yake? Je, Naibu Waziri anatambua kwamba wanaothirika zaidi ni watoto wa maskini ambao hawawezi kujilipia wenyewe? Hilo swali la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili, inaonekana kwamba tatizo letu ni fedha, lakini inanipa matatizo kidogo. Mara nyingi nafikiri kinachokosekana ni nia. Kwa mfano, kama Serikali ingebadilisha aina na wingi wa magari peke yake tungeokoa kiasi kikubwa sana cha fedha ambacho tungeweza kukielekeza kwenye Elimu ya juu. Kuna baadhi ya kodi zimesamehewa hapa ambazo zingeweza kutupa fedha tukazielekeza Elimu ya Juu. Je, sasa Mheshimiwa Waziri anakubali na mimi kwamba katika bajeti ijayo sasa hapo uwepo mpango mkubwa wa kufundisha vijana wengi ili tuweze kuwa na wasomi katika Taifa letu ili tushindane vizuri na nchi za jirani? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU YA JUU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nafikiri anakubaliana na Serikali kwamba tatizo kubwa katika Bodi hii ya mikopo ya wanafunzi wa Elimu ya Juu ni ufinyu wa bajeti. Pamoja na nia nzuri sana ya Serikali ya kuhakikisha kwamba wanafunzi wote wanaofaulu iwe ni daraja la kwanza, daraja la pili na daraja la tatu wanakopeshwa lakini fedha haitoshelezi kufanya hivyo na wanafunzi wanaongezeka mwaka hadi mwaka.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa mwaka huu wa fedha Serikali iliamua kwamba hiyo fedha iliyopo itumike vizuri, iliyoidhinishwa hapa itumike vizuri na tukaona kigezo kiwe ni kuwakopesha vijana wetu waliofaulu vizuri zaidi. *Division Two* amefaulu nakubali, lakini *Division One* amefaulu vizuri zaidi. Kwa hiyo, tukaamua tuwakopeshe *Division One* na *Two* ili tuweze kuwaandaa Watanzania wenye uwezo mzuri zaidi, hii ndiyo *cream* ya nchi.

Mheshimiwa Spika, lakini pia Serikali iangalie uhitaji wa makundi maalum, *professison* maalum katika kuwakopesha vijana wetu. Hamna anayebisha kwamba katika nchi hii tuna uhaba mkubwa wa Walimu hasa baada ya kuhamasika wananchi kujenga shule nyingi, kwa hiyo, Walimu ikaonekana wakopeshwe hata kama alikuwa na *Division Three*. Pia tuna uhaba wa Wahandisi, Madaktari na wataalamu wa Kilimo. Hii ilikuwa ni matumizi mazuri ya fedha hii kulingana na fedha iliyokuwepo.

Mheshimiwa Spika, ninachoweza kusema ni kwamba ndugu zetu ambao walikopeshwa katika ile awamu ya kwanza mwaka 1994/1995 waanze sasa kurejesha fedha hii. Tumeshawaandikia waajiri, Makatibu Wakuu kwa Serikali Kuu, tumeshawaandikia Serikali za Mitaa kwa maana ya Ma-*DED* wa-*identify* wale ambao wana mikopo waanze kurejesha ili tuanze kutunisha Mfuko wa Bodi ya Mikopo na hivi tusiwe na tatizo la kukopesha mpaka *Division Three*. Lakini nakubaliana *Division Two* wamefaulu lakini utamkopesha *Division Two* na *Three* na kuacha *Division One* hiyo utakuwa humtendei haki huyo mwanafunzi.

Mheshimiwa Spika, swali la pili nafikiri Mheshimiwa Mbunge alikuwa anatoa ushauri kwamba Serikali iweze kuweka mikakati. Mkakati mojawapo ndiyo huo wa urejeshwaji wa mikopo na ningependa Waheshimiwa Wabunge mnaohusika na hii mikopo wengine mko humu muwe wa kwanza kuanza kuirejesha. Spika ameshaletewa barua aweze kutusaidia katika ofisi yake lakini pia ninyi wenyewe Wabunge ambao mnadaiwa ile fedha ambayo siyo nyingi na tumewapa *soft way* ya kuweza kuilipa muanze kuilipia, huo ni mkakati mojawapo wa Serikali. Kila mara Serikali itakapokuwa na fedha hii fedha itaongezwa pia katika bajeti. *(Kicheko)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge muda wa maswali umekwisha. Tunayo matangazo. Kwanza ni wageni, tunao wageni kutoka nchi za nje Makao Makuu Nairobi wa *Amani Forum,* Mheshimiwa Mwitila Crispin Shumina kutoka Zambia, yule pale. *Welcome to Parliament. Thank you. (Makofi)*

Tunaye Bibi Salome Katia kutoka Kenya, karibu sana. Naomba kwa nafasi hii niwatangazie Waheshimiwa Wabunge wote waliojisali kuwa wanachama wa *Amani Forum* ambao ndio wageni wetu wamekuja kushughulikia basi watakutana leo katika ukumbi wa Mheshimiwa Msekwa saa 5.00 asubuhi wote wanaotaka kujiunga na *Amani Forum.* Saa 5.00 asubuhi na itakuwa ni fursa pia ya kukutana na wageni wetu kutoka Kenya na Zambia.

Wageni wengine waliopo kwenye *gallery* nadhani ni upande wa kulia ni vijana 15 wa kikundi kinaitwa Mulika cha Mjini Dodoma. Sielewi kikundi hiki kinafanya nini lakini kinaitwa Mulika, wale pale. Karibuni sana vijana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Mgana Msindai, Juma Killimbah, Diana Chilolo na Martha Mlata, wanao wageni wao ambao nao wako kwenye *gallery* kule. Wa kwanza Bwana Hamisi Jumanne Mtali, Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Iramba, yule pale anapunga mkono. Karibu sana. Amefuatana na Wajumbe wa Kamati ya Siasa ya Wilaya Chama cha Mapinduzi. Wajumbe wote wasimame tafadhali ili Wabunge wawaone. Ahsanteni sana na karibuni sana. *(Makofi)*

Kuna matangazo kuhusu vikao na mikutano. Mwenyekiti wa *CPA* Tawi la Tanzania, Mheshimiwa Dr. Raphael Chegeni anaomba Wajumbe wa Kamati ya Utendaji ya *CPA,* Tanzania wakutane leo saa 6.00 mchana katika ukumbi namba 428 jengo la Utawala. *CPA Executive Committee* saa 6.00 mchana huu chumba namba 428.

Mheshimiwa Gideon Cheyo, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Kilimo na Ardhi ameniomba nitangaze kuwa kutakuwa na Kikao cha Kamati hiyo ya Kilimo na Ardhi leo saa 7.00 mchana mara baada ya kusitisha shughuli za Bunge kwa asubuhi na ukumbi wa Mkutano utakuwa ni namba 133 Jengo la Utawala.

Waheshimiwa Wabunge ile semina iliyopangwa kwa ajili ya kesho kwa ghafla waandaaji wametuletea taarifa kwamba hawataifanya. Lakini Semina ya Jumapili tarehe 5 Novemba, 2006 saa 5.00 asubuhi ambayo inahusu Upembuzi Yakinifu wa Mifumo ya Sheria na Udhibiti *(Regulatory Impact Assessment)* itakayotolewa na Wizara ya

Mipango, Uchumi na Uwezeshaji itakuwepo katika Ukumbi wa Pius Msekwa saa 5.00 asubuhi kesho kutwa Jumapili. Waheshimiwa Wabunge wote mnakaribishwa.

Waheshimiwa Wabunge, Ofisi ya Bunge imeitikia wito wenu wa kupatiwa mara kwa mara *official gazette* la Serikali. Nafurahi kusema sasa kwa ajili ya miezi ya Agosti, Septemba na Oktoba mwaka huu machapisho haya yameshanunuliwa na Ofisi ya Bunge na yanapatikana karibu na *Cash Office* pale katika Jengo la Utawala, ni mazito.

Waheshimiwa Wabunge, huu ndio mzigo ambao huko pale kwa jina kwa kila Mheshimiwa Mbunge. Lakini ni muhimu kwa sababu usipojua Sheria Ndogo na ni muhimu mzisome kwa sababu tuna wajibu sisi Wabunge kulinganisha Sheria Ndogo, *regulations* na sheria zilizotungwa ili kujua kwamba tunaendelea na makusudio yale yale kama tulivyopitisha.

Lakini pia kuna mambo mengi tu humu ambayo yanachapishwa ambayo ni muhimu sana Waheshimiwa Wabunge myafahamu. Kwa hiyo, tutawaomba kuanzia sasa yatakuwepo pale kwenye Ofisi ya Majarida karibu na *Cash Office*.

Nimeombwa na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Usalama wa Raia kwa masikitiko sana kutangaza kifo cha Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kagera, Kamanda Gregory Puka amefariki jana usiku.

Hii hasa taarifa kwa Waheshimiwa Wabunge wa Mkoa wa Kagera ili kama kawaida yetu, ushiriki wetu katika mambo kama haya kwa namna moja au nyingine hata kutuma salaam za rambirambi iweze kufanyika. Ndugu wa Marehemu walikwishaarifiwa ndiyo maana nimeruhusiwa nisome tangazo hili. Amefia *Bugando Hospital* kwa operesheni sio ajali.

Baada ya matangazo haya ninakabiliwa na shughuli za wageni na za kiofisi kwa hiyo nitamwomba sasa Mwenyekiti *(Presiding Officer)* Mheshimiwa Jenista Mhagama, aweze kuja kuchukua kiti ili kuendeleza shughuli zilizopo.

*Hapa (Mwenyekiti Mhe. Jenista J. Mhagama) Alikalia kiti)*

**MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

**Muswada wa Sheria ya Mfuko wa Pensheni wa Serikali za Mitaa wa Mwaka 2006 *(The Local Authorities Pensions Fund Bill, 2006)***

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria wa Mfuko wa Pensheni wa Serikali za Mitaa *(The Local Authorities Pensions Fund Act)* 2006 pamoja na marekebisho kwa mujibu wa orodha ya mabadiliko iliyoambatanishwa kwenye Orodha ya Shughuli za leo sasa usomwe kwa mara ya pili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Muswada huu unasomwa baada ya kifo na maziko ya aliyekuwa Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Iringa, Marehemu Peter Siyovelwa, napenda niungane na familia yake katika majonzi yanayotokana na msiba huo mzito. Marehemu Peter Siyovelwa aliwahi kushika nyadhifa mbalimbali za Kitaifa na Kimataifa zikiwemo za Rais wa Shirikisho la Serikali za Mitaa Afrika Mashariki, Mwenyekiti wa *ALAT* Taifa na Mjumbe wa Bodi za Mashirika mbalimbali nchini. Marehemu amewahi kutumikia Taifa katika ngazi ya Waziri, Mkuu wa Mkoa na Mkuu wa Wilaya katika Serikali ya awamu ya kwanza. Kama wengi mtakavyokumbuka marehemu alikuwa muumini mzuri wa Sera ya Ugatuaji wa Madaraka ya Serikali kwa Wananchi.

Aidha, marehemu alikuwa ni kitabu kizuri cha rejea na kamusi ya masuala ya Serikali za Mitaa. Kila mara alihakikisha kwamba uboreshaji wa mfumo wa Serikali za Mitaa unafanikiwa vema. Marehemu alitumia muda wake mwingi na uwezo wake mkubwa kuhakikisha kuwa masuala yaliyoamuliwa katika vikao vya *ALAT* yanapata nafasi ya kufikiriwa na Serikali katika maamuzi yake mbalimbali. Kazi hii inayofanywa leo ni sehemu ya mchango wake katika jitihada za kuwanufaisha wafanyakazi wa Serikali za Mitaa. Nachukua nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuongoza ujumbe wa Serikali kwenye maziko ya marehemu.

Shukrani za pekee zimwendee pia Mheshimiwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mawaziri, Waheshimiwa Wabunge wa Iringa na Waheshimiwa Wabunge wengine waliopata nafasi ya kujumuika katika maziko hayo. Shukrani pia ziwaendee wawakilishi wa Shirikisho la Serikali za Mitaa la Afrika Mashariki kutoka Kenya na Uganda na wananchi wengine wa Halmashauri na Wilaya ya Iringa ambao wameguswa sana na msiba huo. Marehemu atakumbukwa kwa uadilifu na uongozi wake mahiri na kwa mchango wake mkubwa kwa Taifa letu. Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nichukue fursa hii kuishukuru Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa kwa kuujadili kwa kina na kwa umahiri mkubwa Muswada huu na kutoa ushauri. Napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba ushauri wa Kamati hiyo umesaidia sana katika kuboresha Muswada huo. Pia nachukua nafasi hii kuwashukuru wawakilishi na wafanyakazi wa Serikali za Mitaa kupitia chama chao cha *TAWLGU,* Jumuiya ya Tawala za Mitaa Tanzania *(ALAT),* Taasisi mbalimbali za kifedha, Bima na Hifadhi ya Jamii nchini na wadau wengine ambao kutokana na michango yao Muswada huu uliweza kukamilishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko wa Akiba ya Wafanyakazi wa Serikali la Mitaa *(LAPF)* ulianzishwa mwaka 1944 ili kulipa mafao kwa Watumishi wa Serikali za Mitaa. Tangu kuundwa kwake Mfuko umeendelea kufanyiwa maboresho mbalimbali ambapo ilipofikia mwaka 2000 ilitungiwa sheria ijulikanayo kama *The Local Authorities Provident Fund Act* namba 6 ya mwaka 2000 ili kuimarisha utendaji wake chini ya uongozi na usimamizi wa Bodi ya Wadhamini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu kutungwa kwa sheria hiyo Mfuko umeendelea kukua kutoka mtaji wa shilingi bilioni 26.6 mwaka 2000 hadi kufikia shilingi bilioni 102 mwezi Juni, 2006 ikiwa ni ongezeko la zaidi ya mara tatu katika kipindi hicho. Aidha, idadi ya wanachama imeongezeka kutoka wanachama 34,143 mwezi Juni, 2000 hadi kufikia wanachama 65,809 mwezi Juni, 2006. Idadi hiyo inatarajiwa kuendelea kuongezeka kutegemeana na ajira mpya katika Serikali za Mitaa na wengine watakaojiandikisha katika Mfuko huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko ulifanyiwa tathmini mwaka 2005 na kuonekana kwamba unaweza kubadilishwa na kuanza kutoa mafao ya pensheni. Kwa kuwa lengo ni kuhakikisha kwamba wale wote waliokuwa wanachama wa Mfuko wa sasa kuanzia tarehe 1 Julai, 2005 wanapata malipo ya pensheni katika kipindi chote cha ajira zao Serikali imekubali kutoa ruzuku ya shilingi 107.3 bilioni ili kuwezesha Mfuko utakaoanzishwa kubeba jukumu hilo na kubaki kuwa endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo wa akiba ni utaratibu ambao mwanachama na mwajiri wake huchangia kiwango fulani cha mshahara wa mwanachama kilichokubaliwa. Mwanachama anapostaafu, kuacha kazi au kufariki dunia hulipwa kwa mkupuo mmoja kiasi kilichochangwa pamoja na riba iliyopatikana kutoka katika vitega uchumi. Kwa upande mwingine Mfuko wa Pensheni ni utaratibu ambao mwanachama anapostaafu hulipwa malipo ya mkupuo *(Commuted Pension)* na malipo ya pensheni kila mwezi hadi anapofariki dunia. Malipo haya hayategemei kiasi alichochanga mwanachama bali kanuni maalum za hesabu zinazomwezesha kupata mafao bora zaidi na ya muda mrefu kwa kuzingatia mabadiliko ya kiuchumi na hali ya maisha.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwelekeo wa dunia katika sekta ya hifadhi ya jamii hivi sasa ni kubadili mifumo ya malipo ya akiba kuwa ya pensheni inayotoa mafao mengi na bora zaidi. Mifano ya baadhi ya nchi ambazo zimefanikiwa kubadiliki mifumo ya akiba kuwa ya pensheni ni pamoja na Ghana, Zambia, Mauritius na Tanzania kwa upande wa *NSSF*. Mwelekeo huo wa kidunia unawiana na matakwa ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Ibara ya 11(1) inayoeleza pamoja na mambo mengine haki ya mwananchi kupata hifadhi ya jamii wakati wa uzee, ugojwa na ulemavu. Pamoja na maelekezo hayo ya Kikatiba, Sera ya Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Ajira ya mwaka 1999 inaelekeza kuwepo kwa uwiano wa maslahi na mafao kwa Watumishi wa Umma wakiwemo Watumishi wa Serikali Kuu na wale wa Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu nyingine ya kuandaliwa kwa Muswada huu ni kutekeleza Sera ya Taifa ya Hifadhi ya Jamii ya mwaka 2003 inayotoa mwongozo wa jinsi ya kuendeleza sekta ya hifadhi ya jamii nchini. Pia hatua hii ni utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 – 2010 aya ya 105(b) inayoelekeza kuwepo kwa maandalizi madhubuti kabla mfanyakazi kustaafu. Ni dhahiri kutokana na mwelekeo huo Muswada huu umeletwa kwa wakati muafaka kwani unakidhi mahitaji halisi ya hifadhi ya jamii nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, madhumuni ya Muswada huu ni kupendekeza kutungwa kwa Sheria ya Mfuko wa Pensheni kwa Serikali za Mitaa wa Mwaka 2006 ambayo itaanza kutumika kuanzia Julai, 2005 na kufuta Sheria ya Mfuko wa Akiba ya Watumishi wa Serikali za Mitaa ya mwaka 2000 sura 407. Sheria mpya inakusudia kuubadili mpango wa akiba unaoendeshwa kwa ajili ya Wafanyakazi wa Serikali za Mitaa, Taasisi zinazohusiana nazo na wachangiaji wengine kuwa Mfumo wa Pensheni kwa ajili ya walengwa hao na wengine watakaopenda kuchangia Mfuko kwa mujibu wa maelekezo ya sheria itakayotungwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu umegawanyika katika sehemu 11. Sehemu ya kwanza inahusu mambo ya utangulizi ambayo ni jina la sheria inayotungwa, tarehe ya kuanza kutumika na tafsiri za maneno mbalimbali kama yanavyokusudiwa kutumika kwenye sheria husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya pili inaanzisha Mfuko wa Pensheni wa Serikali za Mitaa na kuelezea malengo yake. Inatamka kuhamishwa kwa Mfuko wa Akiba ya Wafanyakazi wa Serikali za Mitaa kwenda kwenye Mfuko unaoundwa wa Pensheni. Inaelezea pia uendeshaji wa Mfuko huo mpya na nafasi na shughuli za Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko huo. Sehemu ya tatu inaanzisha Bodi ya Wadhamini wa Mfuko wa Pensheni wa Serikali za Mitaa na kutamka shughuli zake. Sehemu hii inatamka pia madaraka ya Bodi na namna na kiwango cha kuyakasimu kwa watu na vyombo mbalimbali. *(Makofi)*

Sehemu ya nne inatoa utaratibu wa uandikishaji wa wanachama wa Mfuko na waajiri wao, wote wakiwa wachangiaji wa Mfuko. Sehemu hii pia inatoa wajibu wa mwajiri wa kutoa marejesho ya michango yao. Sehemu ya tano ina vifungu vinavyotoa kiwango cha uchangiaji kwa mwajiriwa na mwajiri na inaelekeza namna ya kuweka kumbukumbu na kutunza michango inayohusiana na Mfuko. Sehemu hii pia inatoa haki kwa mwanachama kupata na wajibu wa mfuko kutoa mafao kwa mwanachama anayestahili kutokana na uchangiaji wake na inaipa Bodi jukumu la kusimamia kufanyika mara kwa mara tathmini ya mali za Mfuko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya sita inatoa orodha ya mafao yatakayotolewa na Mfuko. Inatamka pia matakwa na mazingira ambamo mafao mbalimbali yanastahili kutolewa. Katika mwelekeo huo sehemu hiyo inatoa viwango vya miaka ya kustaafu kwa hiari na kwa lazima. Kanuni itakayotumika huko kukokotoa viwango vya pensheni na kiinua mgongo. Sehemu hii pia inaelezea mazingira mbalimbali ya kipekee ambamo mafao yanaweza kutolewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya saba ina vifungu vinavyoelezea vyanzo mbalimbali vya fedha za mfuko na utumiaji wake. Inatoa maelekezo ya utengenezaji wa bajeti ya mwaka, uandaaji wa hesabu za mfuko na kuziwasilisha kwa Waziri mwenye dhamana. Pia inaelekeza hesabu za mfuko kukaguliwa na Mkaguzi Mkuu wa Serikali kila mwaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya nane inaelezea utaratibu wa Mfuko kupeleka na kuendesha kesi Mahakamani dhidi ya wachangiaji wanaokataa kuwasilisha michango kwenye mfuko kwa wakati. Sehemu ya tisa inaunda makosa mbalimbali ya jinai na adhabu zake kuhusiana na vitendo vinavyoweza kutendwa kwa nia ya kuzuia au kuudanganya mfuko katika ukusanyaji wa michango. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya kumi inatoa maelekezo ya jumla na maswali ya mpito, inaelekeza uhamishaji wa madaraka, haki, wajibu na mali, uendeleaji wa mikataba, ajira za watumishi vilivyomo katika mfumo wa sasa kwenda na kuendelea katika mfumo mpya wa pensheni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya 11 inapendekezwa kufutwa kwa Sheria ya Mfuko wa Akiba wa Wafanyakazi wa Serikali za Mitaa ya mwaka 2000 sura 407. Sehemu hii pia inalinda na kubakiza stahili na vitu vyote vilivyokuwa vinafanyika kihalali kupitia sheria inayofutwa ili viendelee kutambulika na kufanyika chini ya sheria mpya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumalizia kwa kueleza kwamba katika mabadiliko tuliyokwisha kuyasambaza nitawaomba Waheshimiwa Wabunge wasizingatie ile sehemu (e) ambayo imo katika orodha ya mabadiliko tuliyokuwa tumewasilisha pamoja na Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo haya naomba sasa Bunge lako Tukufu liujadili Muswada huu na hatimaye likubali kuupitisha kuwa sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MHE. CHARLES N. KEENJA (k.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi naomba nichukue nafasi hii kutoa salaam za rambirambi kwa familia, ndugu na marafiki wa Marehemu Peter Siyovelwa ambaye kama alivyosema Mheshimiwa Waziri atakumbukwa kwa mchango wake kwa mambo mengi sana aliyoifanyia nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala Mheshimiwa George Malima Lubeleje, kwa niaba ya Kamati na kwa mujibu wa Kanuni ya 70(2) ya Kanuni za Bunge Toleo la mwaka 2004 naomba kuwasilisha maoni ya Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu Muswada wa Sheria ya Mfuko wa Pensheni wa Serikali za Mitaa ya mwaka 2006 *(The Local Authorities Pensions Fund Bill, 2006).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kuanza kwa Mkutano huu wa Bunge Mheshimiwa Spika alituma kwenye Kamati Miswada miwili wa kwanza ni ule wa Kurekebisha Sheria Mbalimbali wa mwaka 2006 *(The Written Laws Miscellanous Amendment Bill, 2006)* na wa pili ni Muswada wa Kurekebisha Sheria Mbalimbali za Serikali za Mitaa wa mwaka 2006 *(The Local Government Miscellanous Amendment Bill, 2006)* ambao unajumuisha Muswada huu wa Mfuko wa Pensheni wa Serikali za Mitaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Kamati yangu iliifanyia kazi Muswada huu tarehe 18 Oktoba, 2006 katika Ofisi yetu Ndogo ya Dar es Salaam kwa kupokea maelezo ya Serikali yaliyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa Mheshimiwa Mizengo Pinda na kuridhika sana na maelezo tuliyopewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo ya Serikali na ufafanuzi uliotolewa kwenye Kamati yangu juu ya Muswada huu tuna masuala machache yaliyojitokeza kwenye Muswada huu. Kimsingi Kamati inaafikiana na mapendekezo yaliyotolewa kwenye Muswada hasa kwa kuzingatia kuwa Muswada huu utaboresha maslahi na maisha ya wanaohusika na Mfuko huu. Hata hivyo pamoja na kuunga mkono Muswada huu yapo maeneo machache ambayo Kamati yangu inapenda kuyatolea maoni na mapendekezo kwa madhumuni ya kuzidi kuboresha Muswada huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ibara ya pili ya Muswada huu inaainisha aina za watumishi wanastahili kulipwa Pensheni na Mfuko huu wakiwemo watumishi kutoka kwenye Serikali za Mitaa, Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa, Mfuko wa Pensheni wa Serikali za Mitaa, Asasi zilizo chini ya Serikali za Mitaa na kadhalika. Kwa kutambua nafasi muhimu waliyonayo Madiwani katika Serikali za Mitaa, Kamati inashauri kuwa Serikali iweke utaratibu maalum wa kuwawezesha Madiwani waingizwe katika Mfuko huu ili nao waweze kupata mafao wakati wanapostaafu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 49 ya Muswada inaipa mamlaka Bodi ya Mfuko wa Udhamini kuwekeza fedha kwa kuingia ubia na chombo chochote itakachoona kwamba itapata manufaa ya kiuchumi au ya kibiashara. Kamati inaafikiana na utaratibu huu. Hata hivyo kutokana na uzoefu uliopatikana siku zilizopita kuhusu matumizi mabaya ya mifuko mingine ya akiba za wafanyakazi, Kamati ilitahadharisha kuwa Mfuko huu ujiepushe na matumizi mabaya ya fedha yanayoweza kuuletea kashfa.

Aidha, mbali na madaraka iliyopewa Bodi, Kamati inashauri pia kuwe na chombo kingine mahsusi ama Wizara yenyewe ama chombo kingine chochote kitakachowekwa, kitakachodhibiti yaani kuangalia madaraka hayo ya Bodi ili yasiweze kutumiwa vibaya. Nafurahi kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa ushauri huu umezingatiwa na Serikali katika marekebisho yaliyowasilishwa mbele ya Bunge hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 65 ya Muswada huu inaweka utaratibu wa kupata michango yaani *recovery of contributions* na kumpa madaraka ya kufungua mashtaka ya jinai Mkurugenzi Mkuu Mkaguzi yaani Inspekta au afisa aliyeidhinishwa *(a person authorised)* na Mfuko kufanya hivyo kwa niaba yake.

Kamati inaona kuwa afisa aliyeidhinishwa au *person authorised* kwa maana iliyotumika kwenye Muswada haitoi picha halisi ya afisa ambaye amekusudiwa katika ibara hii na hivyo inaleta utata. Kwa sababu hiyo Kamati inashauri kuwa ni vyema kuwe na tafsiri mwanzoni mwa Muswada ya afisa huyo ili aweze kufahamika vizuri zaidi.

Kama nilivyoeleza hapo mwanzo Ibara hii pia inampa mamlaka Mkaguzi yaani *Inspector* kufungua Mashtaka ya Jinai. Pamoja na kupewa mamlaka hayo Kamati ilibaini kuwa sifa za Mkaguzi huyo hazikuwekwa bayana. Kwa kutambua kuwa uendeshaji wa mashtaka ni kazi inayohitaji ujuzi, utaalamu na uzoefu maalum Kamati ilishauri kuwa Mkaguzi huyo awe na sifa zinazostahili. Ushauri huu pia umezingatiwa na Serikali kama inavyoonekana katika jedwali la marekebisho lililowasilishwa mbele ya Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine linahusu kifungu cha kwanza sehemu ya kwanza cha jedwali la kwanza la Muswada huu ambacho kinaonyesha kuwepo kwa wawakilishi mbalimbali wanaounda Bodi ya Udhamini ya Mfuko wa Pensheni wa Serikali za Mitaa. *(Makofi)*

Kuhusu Bodi ya Udhamini ya Mfuko wa Pensheni wa Serikali za Mitaa, pamoja na kuwepo kwa wawakilishi wa Serikali na asasi nyingine, Kamati ilitafakari kwa kina nafasi aliyonayo Mwenyekiti wa Taifa wa *ALAT* na kuona kuwa kuna umuhimu mkubwa kwa Mwenyekiti huyo kutajwa moja kwa moja katika kifungu hiki kutokana na ukweli kuwa anawakilisha maslahi ya wafanyakazi wote.

Aidha, Kamati pia ilishauri kuwa ni vema katika uwakilishi huo suala la jinsia likazingatiwa. Serikali ilipokea ushauri huu na kuufanyia kazi kama inavyoonekana katika marekebisho yaliyowasilishwa mbele ya Bunge hili Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyotangulia kusema Muswada huu ni mzuri na unaletwa kwa wakati muafaka. Kutokana na maelezo mazuri yaliyotolewa na Serikali maeneo ambayo Kamati yangu haikuyatolea maoni, yalipatiwa ufafanuzi wa kina na mengine iliyachukua na kuahidi kuyafanyia kazi. Jedwali la marekebisho ya Muswada huu lililowasilishwa Bungeni ni matokeo ya kazi nzuri iliyofanywa na Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo napenda nikushukuru kwa kunipatia nafasi hii ya kuwasilisha maoni ya Kamati mbele ya Bunge hili Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, napenda nimshukuru Mheshimiwa Mizengo Pinda, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Dr. Luka Siyame, Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ushirikiano mkubwa sana walioipa Kamati katika kufanya shughuli zake.

Vile vile napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati hii kwa kazi nzuri waliyofanya ya kuuchambua Muswada huu na kuuboresha kufikia hatua inayoonekana hivi sasa. Napenda niwatambue Wajumbe wa Kamati kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa George Lubeleje, Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa *Hajat* Tatu Ntimizi, Makamu Mwenyekiti, Wajumbe wengine ni Mheshimiwa Pindi Chana, Mheshimiwa Stephen Galinoma, Mheshimiwa Athumani Janguo, Mheshimiwa Rajab Ahmad Juma, Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Mheshimiwa Salim Yussuf Mohamed, Mheshimiwa John Paul Lwanji, Mheshimiwa Fatma Maghimbi, Mheshimiwa Ramadhan Maneno, Mheshimiwa Halima Mdee, Mheshimiwa Nimrod Mkono, Mheshimiwa Abbas Mtemvu, Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa na mimi ninayesoma maoni haya, Charles Keenja.

Vile vile nawashukuru Makatibu wa Kamati hii Ndugu Emmanuel Mpanda, Ernest Zulu, Nenelwa Mwihambi na Charles Mloka kwa kuihudumia Kamati na kutayarisha maoni haya ya Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naomba nitamke kwamba Kamati inaunga mkono Muswada huu. *(Makofi)*

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA - MWENYEKITI:** Ahsante sana, Waheshimiwa Wabunge kabla sijamwita Msemaji wa Kambi ya Upinzani naomba niwataje wale ambao wamekwisha kuomba kuchangia hoja hii kusudi kama wako nje waweze kurudi ukumbini na kufanya maandalizi. Tutaanza na Mheshimiwa Philemon Ndesamburo, atafuatiwa na Mheshimiwa William Shellukindo, Mheshimiwa Dr. Mzeru Nibuka, Mheshimiwa Ezekiel Maige na Mheshimiwa Lekule Laizer. Kwa hiyo, kama kuna mtu hayuko ndani basi naomba aingie.

Baada ya kusema hayo sasa namwomba nimwite msemaji wa Kambi ya Upinzani kwenye Wizara hii ili aweze kuja kutoa taarifa ya Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa. *(Makofi)*

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA - MSEMAJI WA KAMBI YA UPINZANI OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, ninapenda kuchukua nafasi hii kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge Toleo la mwaka 2004, kifungu cha 43(5)(b)(c) na kusomwa kwa pamoja na kifungu cha 70(2) kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Muswada wa Sheria ya Mfuko wa Pensheni wa Serikali za Mitaa yaani *The Local Authorities Pension Fund Act,2006,* ambao pia unalenga kufutwa kwa Sheria ya Mfuko wa Akiba wa Serikali za Mitaa ya mwaka 2000 sura ya 407. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijasema hayo naomba niungane na wenzangu kwa kuwa tukio hili linatokea baada ya msiba ambao sisi wote nadhani unatugusa kwa namna moja au nyingine wa Baba yetu, Ndugu yetu Hayati Peter Siyovelwa, Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Mizengo Pinda, Mbunge na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Celine Kombani, Naibu wake, Ndugu Tarishi, Katibu Mkuu, Mwanasheria Mkuu wa Serikali na timu yao yote ya wataalamu kwa maandalizi ya Muswada huu muhimu kwa maslahi ya watumishi wetu wa Serikali za Mitaa. *(Makofi)*

Kambi ya Upinzani pia inawakilishwa katika Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala. Hivyo, napenda kueleza kuwa Kambi ya Upinzani kimsingi inakubaliana na kuunga mkono maoni ya Kamati. Hata hivyo, pamoja na maoni hayo, Kambi ya Upinzani inapenda kujielekeza katika maeneo kadhaa mahususi katika Muswada huu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni katika mambo ya jumla, ushirikishwaji wa wadau. Kambi ya Upinzani kwa dhati kabisa inaamini kuwa Muswada huu haukuwa shirikishi kwa kiasi cha kutosha. Mfuko huu unaanzishwa kwa fedha za wafanyakazi tena wa vyeo na ngazi mbalimbali. Hapakuwa na ushirikishwaji wa kutosha wa makundi mbalimbali hasa katika hatua ya *Public Hearing* yaani wakati Muswada ulipokuwa ukijadiliwa na Kamati ya Bunge. Maoni ya wadau ni muhimu sana kuhusu mambo yanayowahusu hasa mambo yanayohusu maslahi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaamini hii si hali nzuri kuwaacha nje ya mchakato wa kutunga sheria kundi muhimu la wafanyakazi na hata waajiri wao ambapo kila mmoja hukatwa kila mwezi kutoka mshahara wake kiasi cha asilimia tano kwa wafanyakazi na kumi na tano kwa waajiri ambao ni Halmashauri za Miji, Manispa na Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inadhani hii ni dosari kubwa na ni vema ikarekebishwa katika Miswada ijayo. Ni muhimu kuelewa ya kuwa kitu chochote kinachohusu kukatwa kwa jasho la mfanyakazi maridhiano baina ya pande husika ni muhimu kabla ya sheria kutungwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Makao au Ofisi Kuu za Mfuko, kwa ujumla Kambi ya Upinzani ina mashaka na mambo kadhaa katika eneo hili:-

(a) Sheria haielezi chochote kuhusu Makao au Ofisi za Mfuko huu. Uzoefu unaonyesha kuwa wakati Ofisi ya Mfuko wa Akiba wa Serikali za Mitaa ulikuwa Dodoma yaani ile Sheria tunayoifuta leo. Shughuli nyingi za Mfuko zimekuwa zikifanyika Dar es Salaam, jambo linalofanya viongozi wa mfuko huu kusafiri kila kukicha kati ya Dar es Salaam na Dodoma. Mfuko umeendelea kujenga majengo mazuri na makubwa Dar es Salaam badala ya Dodoma ambapo ofisi zipo, jambo ambalo limeendelea kuwa kichocheo cha kufanya kazi Dar es Salaam badala ya Dodoma. Safari ni gharama, tena hugharimiwa na makato toka mishahara ya wafanyakazi ambao hali yao si nzuri. Inawezekana tukawalaumu Maofisa wa Mfuko kwa kuuingizia mfuko gharama hizo. Lakini Kambi ya Upinzani haiamini kuwa hiyo inafanyika kwa makusudi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahiri, watumishi wa Mfuko hawana njia tukizingatia historia ya mfuko huu. Huu ni mfuko wa fedha na kimsingi ni lazima ushirikiane katika kutekeleza majukumu yake na mifuko mingine ya aina hii au na Taasisi nyingine za fedha. Hali halisi inaonyesha kuwa taasisi karibu zote zinazoshughulikia mambo ya fedha makao yao makuu yako Dar es Salaam. Hazina yenyewe ambayo ni mhimili mkuu wa Taasisi za fedha ipo Dar es Salaam, Benki Kuu ipo Dar es Salaam. Hivyo ni dhahiri shughuli nyingi za mfuko lazima zifanyike Dar es Salaam. Ni vema sasa tukaokoa fedha hizo za safari na kuzielekeza katika kuboresha maisha ya wafanyikazi tunaowakata mishahara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tungependa Mheshimiwa Waziri alieleze Bunge hili ni wapi hasa itakapokuwa Makao makuu au Ofisi Kuu ya Mfuko, na ni kwa nini iwapo Makao Makuu hayo yatakuwa ni Dodoma, shughuli nyingi za Mfuko ikiwa ni pamoja na mikutano, semina na kadhalika ziendelee kufanyika Dar es Salaam? Kambi ya Upinzani ingeshauri kwa dhati kabisa Makao Makuu ya mfuko yawe Dar es Salaam kwa sababu tulizotaja hapo juu ikizingatiwa kuwa Dar es Salaam ni pia Mji wa biashara, Taasisi nyingi za Serikali, Ofisi nyingi za Serikali ziko Dar es Salaam kwa lengo la kurahisisha shughuli za mfuko na mawasiliano na vyombo vingine vya aina yake.

(b) Kambi ya Upinzani imetafakari kwa makini Kifungu cha 81, kinachotoa mamlaka kwa Waziri kutunga Kanuni. Kwa bahati mbaya hakuna kipengele chochote kinachoeleza jinsi utoaji huduma utakavyoratibiwa. Wengi wa wafanyakazi wa mfuko huu ni walimu, waganga na manesi, wafanyakazi wa kilimo na mifugo na hata mtu mmoja mmoja kama ilivyotajwa wakiwemo Madiwani japo Mheshimiwa Waziri amesema tusiangalie tena kipengele (a) cha marekebisho na baadaye tutamwomba atufafanulie kama Madiwani watakuwemo tena au hawatakuwemo. Hili limetokea hapa hapa kwa hiyo sikuweza kuliingiza katika hotuba. Lakini kwa msingi huo basi asilimia 85 ya watumishi watakao husika na mfuko huu wako vijijini ambako hakuna hospitali, kituo cha afya au zahanati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vema Waziri atuhakikishie wakati wa majumisho atahakikisha vipi watumishi hawa wasipate adha kama ile ya Bima ya Afya ambapo watu wanakatwa fedha lakini upatikanaji wa huduma unakuwa wa taabu kutokana na huduma nyingi kutopatikana vijijini. Je isingefaa utaratibu huo ukaratibiwa kupitia Kanuni atakazotunga Waziri? Na kwa kuwa hasemi chochote katika kipengele kile cha Kanuni kuhusu mambo atakayoyatungia basi tungependa atupatie ufafanuzi wa kina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala zima la uboreshaji wa mafao kupitia ushindani.Tuko kwenye ulimwengu wa mtandao au wa sayansi na teknolojia. Muda wa kufanya mambo kwa mazoea sasa umeisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi nyingi zinafungua milango kuboresha maslahi ya wafanyikazi wake. Nchi hizo haziweki tena mifuko ya lazima na narudia neno lazima na kuzitungia Sheria kulazimisha uanachama Mheshimiwa Waziri nashukuru hapa ametumia neno mfano wa nchi kadhaa ikiwemo ya Ghana ambako wanachofanya ni

kutunga Sheria na kuruhusu ushindani wa Mashirika au hata watu binafsi wanaotaka kufungua mifuko ya aina hiyo na kwa kuwa misingi ni ushindani, kila mfuko unafanya kila jitihada kutoa maslahi yaliyobora zaidi na kupunguza *premium* kadri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inavyowezekana ili walala hoi waweze nao pia kuingia kwenye aina moja au nyingine ya mafao hayo mtindo wetu wa kulazimisha watu kuwa mwanachama wa mfuko fulani anakofanya kazi umepitwa na wakati na una hatari ya kutokuwa na manufaa ya ushindani yaani *benefit of competition.* Mifano hai ni Afrika ya Kusini na Ghana ambako wanachofanya ni kutenga sheria na kuruhusu ushindani wa mashirika au hata watu binafsi wanaotaka kufungua mifuko ya aina hiyo na kwa kuwa msingi ni ushindani kila mfuko unafanya kila jitihada kutoa maslahi yaliyo bora zaidi na kupunguza *premium* kadri inavyowezekana ili walalahoi waweze nao pia kuingia kwenye aina moja au nyingine ya mafao. Mtindo wetu wa kutunga sheria ya kuwalazamisha watu kuwa mwanachama wa mfuko anakofanya kazi umepitwa na wakati na una hatari ya kutokuwa na manufaa ya ushindani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya Serikali inapaswa kufungua milango, kutengeneza mazingira mazuri na kuhakikisha hakuna utapeli wa aina yoyote. Watu wanatakiwa kutafiti, kupima na kuchagua wenyewe wapi kuna unafuu wa michango na wapi kuna mafao makubwa zaidi. Kwa mfano wakati mfuko huo unalenga kumkata mfanyakazi kila mwezi asilimia tano ya mshahara wake, kuna mifuko inakata asilimia tatu tu na mafao karibu yanalingana, mwanachama akipewa uhuru wa kuchagua ni dhahiri atachagua kule kwenye asilimia tano ya kukatwa mshahara kuliko kwenye asilimia tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inadhani wakati umefika sasa wa kufungua milango, ili mifuko hii ishindane kupata wanachama kutokana na ubora wa huduma wanazotoa, mafao yaliyobora, kiwango cha makato chenye tija zaidi na vigezo vingine vya aina hiyo. Sheria ilinde misingi ya ushindani huo kuliko kuwalazimisha watu kuwa mwanachama wa mfuko anakofanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mtandao unaoaminika wa huduma. Kifungu cha 26(1) kinafafanua kwa kina aina ya mafao yatakayotolewa na mfuko huu. Pamoja na mafao mengine, mfuko unalenga kuwapa wanachama wake Mafao ya Uzazi yaani *maternity benefits*, Mafao ya ugonjwa *Sickness benefits* japo hayafafanuliwi kwa kina, Huduma ya mazishi *funeral grant* na Huduma ya Elimu *(Education grant),* haya ni mafao mazuri na yanamgusa mfanyakazi wa ngazi za chini kabisa kwa hiyo ni lengo kwa kweli la kuungwa mkono. Pamoja na nia njema ya Mfuko huu, sheria haijaweka bayana mfumo au muundo wa utoaji huduma utakaowahakikishia wanachama wake huduma bora, ndiyo maana tunapenda sana Waziri katika Kanuni atakazotunga aweze kujielekeza kwenye eneo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tuna uzoefu wa Bima ya Afya ambako bado wanachama wana malalamiko mengi. Wakati wanakatwa hela kila mwezi wanashindwa kupata huduma kwa vile wanakoishi vijijini mara nyingi huduma hazipatikani. Isitoshe taratibu za kiutawala ili kupata huduma hizo kwa maeneo mengi ni kikwazo kikubwa. Baada ya uzoefu huu, tunapaswa kuwa na majibu ya matatizo hayo tunapotunga leo

sheria inayofanana na hiyo bila ya kuweka vipengele ambavyo vinatoa suluhisho jinsi ya kukabiliana na matatizo yanayo lalamikiwa katika sheria rafiki zinazofanana na hii tunadhani tutaingia kwenye matatizo yale yale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tulivyosema hapo awali, mfuko huu unalenga kutoa huduma kwa watumishi wa Serikali za mitaa wakiwemo walimu, manesi na waganga, watumishi wa kilimo na mifugo na watu mmoja mmoja. Hili ni kundi kubwa sana, tena limetapakaa nchi nzima, na mara nyingi vijijini ndani kabisa ambako Zahanati ziko mbali, vituo vya afya viko mbali na kadhalika. Sheria haisemi chochote kuhusu mfumo wa utendaji kazi wa Mfuko na Bodi. Haisemi kama kutakuwa na mtandao wa ofisi za bodi kwenye maeneo mbalimbali. Sheria ikitazamwa kwa makini inatia msisitizo sana katika upande wa makusanyo ya michango ya wanachama, lakini haisemi kitu kabisa kwa upande wa udhibiti wa ubora wa Huduma zitakazotolewa Sheria inayokosa balance ya aina hii ni hatana ni tatizo tungependa upande wa pili pia utazamwe sana wa utoaji huduma kuliko kukazania tu ukusanyaji wa mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaona jambo hili ni hatari kabisa kwani watu watakatwa fedha zao asilimia tano na kisha wakaishia bila huduma zinazolingana na fedha zao *(value for money)* au kukosa huduma kabisa. Tungependa Waziri alihakikishie Bunge hili udhibiti wa ubora wa huduma utafanyika vipi, muundo gani wa mtandao wa Bodi utatumika kuhakikisha wafanyakazi hawapati usumbufu usiokuwa na sababu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafungu mengineyo tunayodhani yanahitaji kuboreshwa, Kambi ya Upinzani, licha ya mambo hayo ya jumla imetafakari kwa kina sana Muswada huu wa Sheria na kubaini maeneo kadhaa yenye kuhitaji kuboresha au kurekebishwa kwa lengo la kuufanya mfuko huu ufanye kazi zake kwa ufanisi. Maeneo haya ni kama ifuatavyo:-

(i) Kifungu cha 10(1) Kambi ya Upinzani inadhani kwa vile Serikali yetu imekwisha kuridhia maamuzi ya kuwa na Idadi ya Wanawake katika maeneo yote ya uamuzi isiwe chini ya asilimia thelathini, basi katika Kifungu cha 10(1) na hasa kwenye Jedwali la Kwanza *(First Schedule),* idadi ya wanawake itajwe wazi hasa pale panapotakiwa kuingia watu wawili kwenye Bodi angalau mmoja awe mwanamke, nashukuru kwamba kwenye *schedule of amendiment* tuliyopata leo asubuhi Serikali imetekeleza moja lakini bado kuna mahali pengine ambapo bado panataja wawili lakini hapo hakutajwa mwanamke. Hii siyo tu kukuza demokrasia lakini pia kupata hisia za wanawake katika chombo kikubwa kama hiki kinachogusa moja kwa moja maslahi ya watu wengi.

(ii) Kifungu cha 10(2) Kambi ya Upinzani bado ina tatizo la msingi na Kifungu hiki kinachompa mamlaka Waziri kwa kushauriana na Bodi, kurekebisha, kubadilisha, au kufuta kipengele chochote kilichoko katika Jedwali hili. Hii ina maana ya kwamba hakuna kinachomzuia Waziri kama hataki wawakilishi wa wafanyikazi katika Bodi hii au wawakilishi hao wanakuwa kikwazo kwake na kwa Bodi yake kufanya wanalotaka kwa kubadilisha yeyote kati ya wajumbe wa Bodi au kuwafuta wote kabisa na kuwaweka

wengine. Hii ni hali ya hatari kuweka chombo kama hiki chini ya huruma ya mtu mmoja au kundi la watu. Inawezekana leo tuna Waziri mzuri na sina mashaka na ndugu zangu waliokaa kwenye mstari ule, lakini sheria haitungwi kwa ajili ya kumtazama mtu fulani. *(Makofi)*

Kambi ya Upinzani inapendekeza kipengele hiki kifutwe kabisa kwa vile kinaenda kinyume na dhana nzima ya mamlaka ya chombo hiki mamlaka ambayo inaotokana na uwakilishi wa uhakika unaolindwa na kwa mamlaka ya Sheria. Ikumbukwe kuwa Waziri ana mamlaka ya kutunga kanuni wakati wowote bila kupitia Bungeni na au kubadili jedwali bila kupitia Bungeni na mara nyingi kanuni haziji Bungeni.

(iii) Kifungu cha 41 kinazungumzia mazingira ambapo mfanyakazi mwanachama wa mfuko ameachishwa kazi katika mazingira ambapo mwajiri hamhitaji tena au ofisi yake imefutwa katika muundo wa ajira, haki zake katika Mfuko zitaamuliwa na Rais kama ataona inafaa. Huyu ni mwanachama aliyechangia kutokana na mshahara wake. Hatuoni kwa nini Rais apewe mamlaka ya kama ataona inafaa. Mtumishi huyu tayari ameshaumizwa na uamuzi wa kuachishwa kazi. Bado tunatia pilipili kwenye kidonda kwa kumtaka afuatilie haki zake hadi ofisini kwa Rais, ajieleze, Rais amwelewe ndipo aone kama inafaa. Ni dhahiri haya yatakuwa mateso ya ziada kwa mtu anayetoka Mutukula, Rukwa au Kyela au Masasi au kona yoyote mbali ya nchi hii ambapo usafiri wenyewe kwanza ni taabu pia atatumia hela zake za mfukoni atamaliza hata hizo anazofuatilia kwa ajili ya usafiri kumfuata Rais hadi Dar es Salaam kufuatilia jambo ambalo kimsingi ni haki yake. Tunadhani iwapo kuna sababu basi aambiwe katika Barua ya kumwachisha kazi kuwa anastahili au hastahili haki zozote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria ni lazima kwanza ilinde haki zake za Kikatiba za malipo halali na ya haki ndipo kwa msingi wa barua hiyo, ikiwa lazima Rais aingie basi iwe ni kama mamlaka ya rufaa lakini si vinginevyo. Watu wengi watapata usumbufu usio na kifani bila sababu iwapo sheria itabakia kama inavyopendekezwa katika Muswada. Leo tuna ushahidi wa wazee wetu wameifanyia nchi hii kazi na wanafuata kwa gharama kubwa haki zao za ustaafu kule Dar es Salaam na bado hawazipati wanakaa miezi na miezi wanatumia hela, wanauza mifugo, wanatafuta haki na hazipatikani. Tunaomba tusiwaingize watu wetu katika hali hiyo kwa kutunga sheria.

(iv) Kifungu cha 49 kimefanyiwa marekebisho kwa kuitaka Bodi kupata kibali cha Waziri kabla ya kuwekeza fedha katika mradi wowote ule. Hata hivyo, wakati Kambi ya Upinzani inakubaliana na sharti hili kwa lengo la kulinda fedha za wanachama zisiingie katika biashara isiyo na tija au yenye wasiwasi, ni vema Bodi pia ikawa na maamuzi ya kuwekeza fedha katika Dhamana za Serikali *(Government Securities and bonds/Treasury Bonds)* ambazo kimsingi ni za muda mfupi na ni za uhakika kwa kuwa ziko mikononi mwa Serikali yenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kusubiri maamuzi ya Waziri kwa jambo lililo wazi kama hili linaweza kufanya Mfuko usiwe shindani katika ulimwengu wa sasa na ukashindwa kufanya biashara au faida kwa njia ambazo ziko wazi. Hivyo,

tunapendekeza, Bodi ipate kibali cha Waziri kwa uwekezaji mkubwa ambao fedha zitarudi baada ya muda mrefu kama kujenga majumba na kadhalika lakini si kwa *government securities* wala *bonds.*

(v) Kwenye Jedwali la Kwanza *(First Schedule),* kwenye marekebisho imependekezwa (b): *"A Permanent Secretary to the Ministry of Finance or his representative."* Tunapendekeza kuwa kutokana na umuhimu wa mfuko huu na matatizo ambayo hivi karibuni yameikumba mifuko yetu na hasa kwa kuingia katika biashara au uwekezaji ambao unalalamikiwa sana ni vema, Jedwali liweke wazi kuwa: *"A Permanent Secretary to the Ministry of Finance or his representative* hilo tunakubaliana lakini tunaongeza *but in any case, not below the rank of Deputy Secretary."* Hii itarahisisha maamuzi, lakini pia kuwa na ufuatiliaji wa karibu wa mwenendo wa Mfuko huu katika Ofisi ya Katibu Mkuu. Kuwa na *or his representative,* kwa uzoefu tumeona kila mwanya huu unapotolewa kuna kuwa na tatizo kwa vile siyo mtu huyo huyo anatumwa kila mara na hivyo kukosa mtiririko, lakini pia wanaotumwa huwa maofisa wa chini kiasi cha kukosa maamuzi mazito.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kumlimbikizia Mamlaka Waziri, Pamoja na nia njema ya kudhibiti na hivyo kumpa mamlaka mengi Waziri, kwenye Muswada huu, Mheshimiwa Waziri amepewa mamlaka makubwa isivyolazima. Mathalani, Kifungu cha 10(2) Waziri ana uwezo wa kufuta kabisa Bodi ambayo ina uwiano ambao Bunge limeuthibitisha kutokana na umuhimu wake. Lakini Waziri anaweza siyo tu kubadilisha, bali anaufuta kabisa na hivyo kuwa na uwezekano mkubwa wa kubadili nia na madhumuni ya Bunge katika kuuweka uwiano huo. Waziri huyo, huyo na siyo Bodi, ndiye mwenye Mamlaka ya kutangaza masharti ambayo mtu anakuwa *insured person* yaani kuwa mwanachama. Haya yanatakiwa kuwa mamlaka ya Bodi, na ikiwa lazima Waziri athibitishe lakini si Waziri afanyekazi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii pia inaiondolea Bodi uwezo wa kuwa *efficient and Competitive* kwa vile ni lazima imsubiri Waziri. Wakati wenzao wanatafuta wananchama kwa udi na uvumba, wao wanamgonjea Waziri. Kifungu cha 19 Bunge linapanga kuwa mchango wa wafanyikazi uwe asilimia tano ya mshahara wa mfanyikazi na tajiri ambaye ni Halmashauri ya Jiji, Miji au Manispaa ichangie asilimia 15 kila mwezi ya mshahara wa mfanyakazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Waziri kwa kutangaza kwenye Gazeti la Serikali anapewa mamlaka ya kuongeza michango hiyo au kuipunguza anavyotaka tunaona jambo hilo ni la hatari. Jambo linalolifanya Bunge lisiwe na maana kabisa. Vivyo hivyo kifungu cha 24, 26 na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashauri tuwe na Bodi yenye nguvu na mamlaka ya kutosha kuiwezesha kufanya kazi zake katika kipindi hiki cha ushindani na utandawazi bila mlolongo wa umangimeza *(Bureaucracy).* Waziri awe na mamlaka ya kumtosha kuingilia pale anapoona mambo yanaenda kombo tu. Wenzetu wengi siku hizi wanatumia mfumo wa *eyes on and hands off.* Nasi hatuna budi kuelekea huko iwapo tunapenda kuingia kwenye ushindani wenye manufaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapenda kutoa tahadhari ya Jumla kuhusu matumizi ya mfuko huu. Kuna malalamiko mengi kuhusu matumizi ya fedha katika mifuko mingine iliyoundwa na Bunge lako Tukufu. Wanachama wanalalamikia kucheleweshewa mafao yao, kupata usumbufu katika kuyafuata na hata kiwango kisichoridhisha cha mafao hayo ikilinganishwa na uwekezaji *(investment)* mkubwa unayofanywa na mifuko hiyo. Isitoshe, pale kunapotokea matatizo hata Serikali kutoonekana kuwa na meno ya kutosha kulinda maslahi ya wanachama wake kama ilivyo kwenye mifuko iliyolalamikiwa na wadau wengi na hivi karibuni kulalamikiwa sana kwenye kwenye vyombo vingi vya habari. Ni imani yetu kuwa mfuko huu utaanza vema na utaweka misingi imara ya matumizi thabiti ya fedha za wanachama wa mfuko, lakini pia kodi za wananchi ambao huchangia kwa kupitia kwa waajiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, narudia tena kukushukuru kwa niaba ya Kambi ya Upinzani kwa kunipa nafasi ya kutoa maoni haya. *(Makofi)*

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA - MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dr. Slaa, nakushukuru sana kwa kutoa maelezo ya Kambi ya Upinzani. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa tutaanza mjadala wa pamoja na nitamwita kwanza Mheshimiwa Ndesamburo, atafutiwa na Mheshimiwa William Shellukindo. *(Makofi)*

**MHE. PHILEMON NDESAMBURO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kwanza kuwa mchangiaji wa kwanza leo asubuhi katika Muswada ulio mbele yetu. Kwanza kabla sijasema na mimi nitoe rambirambi kwa kifo cha Mzee wetu Peter Siyovelwa, kilichotokea Dar es Salaam na mazishi yakafanywa Iringa, nawapa pole sana familia ya Marehemu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nina mchango mdogo sana lakini mchango wangu unahusiana hasa na wanachama wa mifuko hii. Mifuko hii inawaangalia wanachama kuwapa *pension* mwishoni, mazishi na mambo mengine madogo madogo. Lakini mimi najihusisha hasa na elimu ya wafanyakazi wa Serikali za Mitaa. Ili nchi yetu iweze kuendelea tunahitaji wasomi, ili tuweze kuleta maendeleo tunahitaji watalaam ambao ndiyo wako vijijini ambao ndiyo wanaendesha Serikali za Mitaa. Wengi wao hawana kisomo cha kutosha na ndiyo mara nyingi wakati Mkaguzi Mkuu anapoangalia mahesabu yao wanakuwa na *certificate* chafu na kumekuwepo na malalamiko mengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninachosema hapa ni kwamba wale wafanyakazi wa Serikali za mitaa waweze kupewa mikopo ya kusoma wakati wakiwa bado wako kazini na wakiweza kupewa mikopo ya kwenda kusoma zaidi ili waje kufanya kazi vizuri zaidi sio tu watauongezee mfuko pesa nyingi zaidi kwa sababu wakihitimu vizuri mishahara itapanda *contribution* yao itakuwa kubwa na kazi ya ufanisi itaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna nchi yoyote inayoendelea bila kuwekeza katika elimu. Mifuko yetu mingi inaangalia kuwekeza katika vitega uchumi lakini kitega

uchumi kizito kuliko vyote ni elimu na sisi hatutaki kuwekeza katika elimu hawa vijana au hawa wafanyakazi wa hii mifuko wanapesa zao katika hii mifuko. Mifuko hii itumike katika kifungu cha 48, matumizi ya pesa hizi za mifuko. Ningeomba Waziri aongeze pale mikopo kwa ajili ya wafanyakazi ambao ndiyo wadau wanaochangia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna tatizo hapa tunasema, Mfuko wa Serikali wa kutoa Mikopo kwa Wasomi wa Vyuo vya Juu, hautoshi. Hii ni sehemu moja ambayo ingeweza kupunguza matatizo ya Serikali kwa hao waliotayari katika kazi wakaweza kujiendeleza kwa kutumia Mfuko huu huu wa Pensheni, hii *Fund*. Badala ya kuwekeza katika majumba na kufaidisha matajiri na watu wengine, hawa wenye Mfuko wao wangefaidi kwanza. Ndio wangefaidishwa kwanza, waweze kupata masomo na warudi walete ufanisi katika kazi zao katika vijiji na sehemu wanazofanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimejaribu kuangalia katika hii, sijaona kama kweli kuna *emphasis* katika kujaribu kuwasaidia wenye mfuko wao. Huu Mfuko una wenyewe, lakini hawana maamuzi katika Mfuko wao. Pesa nyingi katika Mfuko huu zinatumika katika kuwekeza kwa watu wengine na wao hawafaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ningeomba sana, wafanyakazi katika Serikali za Mitaa ili waweze kujiendeleza, Mfuko huu uwe wazi ya kuwa wanaweza kupewa mikopo, wakajiendeleza na wakaweza kuja kurudi kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili katika *section* ya 49, mimi sikubaliani katika sehemu hii kumfanya Waziri aingilie Bodi wakati wakitaka kutoa mikopo au wakitaka kutoa miradi yoyote. Huu ni ukiritimba ambao utachelewesha maendeleo katika ku-*make decision*. Kuna mambo mengine ambayo utaweza kungojea Waziri labda kwa mwezi mzima hajatia saini, ambapo hata kama ni mradi walitaka kufanya, unachelewa.

Mimi sioni kama kuna haja ya kumwambia Waziri aingilie Bodi. Bodi tumeiunda na ina madaraka, ipewe madaraka yake na ifanye kazi yake. Kwa nini tunaleta ukiritimba wa kumweka Waziri pale aje akaangalie tena, ndiye aje akasimamie! Mimi sioni sababu! Ni ukiritimba wa kuchelewesha na haya mambo ndio matatizo. Hii Mifuko mingine tunayo. Sijui wanachama wa hii Mifuko wamefaidi nini? Wanafaidi tu kununuliwa masanduku wakati wa kuzikwa lakini hawana faida yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo yangu yalikuwa ni machache hayo. Naweka *emphasis* ya kuwa Mfuko huu uwafaidishe wenye Mfuko wao kwa kuelimishwa ili waweze kuja kuchangia vizuri katika maendeleo ya Taifa letu. Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA - MWENYEKITI:** Mheshimiwa Philemon Ndesamburo, ahsante sana kwa mchango wako. Sasa naomba nimwite Mheshimiwa William Shellukindo na Mheshimiwa Dr. Omar Nibuka, naomba ajiandae.

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili na mimi nitoe mchango wangu kidogo kuhusu

Muswada huu wa Kuanzisha Sheria ya Mfuko wa Pensheni wa Serikali za Mitaa badala ya Mfuko wa Akiba ambao ulikuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa napenda kuipongeza Ofisi ya Waziri Mkuu, Waziri Mheshimiwa Mizengo K. P. Pinda, pamoja na wasaidizi wake kwa kupitia Sheria iliyokuwepo kwa makini kabisa na kutoa mapendekezo ambayo yanakwenda na wakati. Nawashukuru sana kwa hilo na naunga mkono Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kabla ya hapo, napenda sana kutoa rambirambi zangu kwa familia na jamaa wa Marehemu Peter Siyovelwa, kwa msiba mkubwa waliopata. Namwomba Mwenyezi Mungu aiweke roho ya Marehemu mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitapenda kutoa kile nasema…huu Muswada unanihusu sana. Unanihusu sana kwa nini! Nimekuwa Mwenyekiti wa Mfuko wa Akiba kwa muda wa miaka minne wakati nikiwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu. Kwa hiyo, yanayoelezwa yananifariji sana kwamba Mfuko unaendelea. Nimeona katika miaka hii kumi, kazi nzuri sana imefanywa na Bodi pamoja na wataalam wa Mfuko huu na ndiyo iliyofanya Serikali kwa kweli kukubali kuubadilishia Mfumo wake, badala ya kuwa wa Akiba, uwe ni Mfuko wa Pensheni. Napenda kuwapongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa vilevile ningependa kumtaja Mheshimiwa Anna Abdallah, ambaye wakati ule ndiyo alikuwa Waziri anayehusika na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Ilikuwa ni vigumu sana wakati ule kuishauri Serikali ikakubali kuwekeza na uwekezaji mkubwa zaidi ni kwenye Ofisi za Bunge hizo pamoja na ule Ukumbi wa Msekwa sasa hivi, ndio uwekezaji wa kwanza kabisa umefanywa na tunashukuru kwamba Serikali ilinunua majengo hayo, ikiwa na maana kwamba wale wanaosema kwamba kuwekeza huko ni kupoteza fedha, hawaelewi kwamba fedha zikikaa kwenye benki kule, zinanufaisha wafanyabiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko unapata asilimia ndogo sana ya faida ambayo inapatikana kwa kuweka fedha benki. Lakini kuziweka kwenye vitega uchumi, wanafaidika zaidi kuliko zikikaa kwenye benki. Huo ndio mwelekeo nadhani tunakokwenda huko na ni mabadiliko kwa kweli. Hii Mifuko kwa wale *economists* wangesema kwa kiingereza ina fedha nzuri, inaitwa *liquidity.* Iiko *liquid*, kwa sababu Jengo hili la Bunge na Ukumbi ule haukujengwa na mkopo, ulijengwa na fedha za Mfuko wa Akiba. *(Makofi)*

Kwa hiyo, zimepata thamani zaidi kuliko kama zingekaa benki na kupewa kale ka-asilimia kadogo ka- benki. Kwa hiyo, mimi sidhani kama uwekezaji huo ni kupoteza hizo fedha, fedha zimetumika vizuri zaidi. Kwa hiyo, kazi nzuri imefanywa na Bodi hiyo. Kwa hiyo, mimi napenda kuipongeza kabisa na kwamba waendelee kuwekeza kwenye vitega uchumi ambavyo vitawanufaisha wenye Mfuko huo au wachangiaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kukubaliana na Serikali kabisa kwamba, kwa sababu ni uwekezaji huu, ni vizuri kila mara tathmini ifanyike ili hata wachangiaji wale wajue Mfuko wao sasa una thamani kiasi gani au una *asset* kiasi gani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tatizo sugu ambalo sisi Waheshimiwa Wabunge linatupata, suala la kuchangia. Wafanyakazi wamekatwa mishahara yao, fedha ziko kwenye Halmashauri, lakini hazifikishwi kwenye Mfuko. Ni tatizo sugu kabisa, mimi kama Mbunge nimeshashughulikia wafanyakazi wengi ambao wamestaafu, wengine wamekuja Dodoma hapa na nashukuru sana kwamba wakati nilipowapeleka kule, wamehudumiwa vizuri sana.

Lakini sasa utakuta fedha ambazo zipo ni zile ambazo zimefika tu kwenye Mfuko. Fedha nyingine hazikufikishwa, kwa hiyo, inabidi warudi tena waende wakadaiane na Wakurugenzi wa Halmashauri za Wilaya. Sasa, nadhani hii kasi mpya na nguvu mpya ibadilike. Kama mtu amechangia katika mwezi huu, mwezi unaokuja, fedha zake lazima zipelekwe kwenye mfuko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwamba vimewekwa vifungu vya adhabu ya kutowasilisha michango hii. Lakini hizi adhabu, kwa kweli za faini, mimi nadhani faini isitumike sana. Hii itatusaidia kama Mkurugenzi mmoja atafungwa ile miaka miwili, itakuwa ni fundisho kubwa sana. Wanacheza cheza sana na hizi faini. Kwa hiyo, tutumie njia ambayo kwa kweli itabadilisha hali ilivyo sasa.

Wataalam katika utawala ambao wanahusika na udhibiti wa nidhamu wanasema hivi nitasema kwa kiingereza: *punishment if properly administered, should work as a deterrent memento* yaani mtu akikaa, anakumbuka akisema mwenzangu alikula miaka miwili, sitaki kwenda jela. Itakuwa ni fundisho. Hili la faini kwa kweli tungewashauri, japokuwa hatutaki kuigilia kazi za Mahakama, lakini tungeshauri kwamba hiyo haijasaidia. Tumtoe muhanga mmoja akatumikie kifungo, halafu hiyo itakuwa ni fundisho na hakuna mtu ambaye ataleta mchezo mchezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii nazungumza kwa sababu inasumbua sana, hata inaweza kuwa katika wale wastaafu ambao wanahusika, wengi ni wa Halmashauri za Wilaya, kwa sababu michango yao haijafika kwenye mfuko mpaka Waziri Mkuu anasema nileteeni sasa orodha yeye ashughulikie. Nadhani hili suala katika Sheria mpya liwekewe *full stop*, lisitokee tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu ni mzuri sana kwa sababu katika kifungu cha 17(4), inatoa fursa kwa mchangiaji naye aongeze mchango wake. Nadhani hili ni badiliko zuri sana. Lakini, linahitaji kutolewa maelezo na elimu, kwa sababu katika jamii yetu suala la kuweka akiba na kukopa ni kitu watu wanakiogopa sana. Suala la kuweka akiba na kukopa si kitu cha kawaida. Sasa lakini kwa mfanyakazi ambaye hana muda wa kwenda kuwekeza mahali pengine, pengine mahali pa kuwekeza kwake zaidi ni hapa kwa sababu akikatwa zile fedha zinaingia kwenye Mfuko wa pensheni.

Kwa hiyo, mimi nadhani hili lingetolewa maelezo vizuri na hata pengine kuanzisha kipindi cha kutoa maelezo kwa mchangiaji kwamba atapata faida. Kwa hiyo, kile kiwango kilichowekwa kisheria kiachwe hivyo. Lakini yeyote yule aweze kuchangia zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa muono huu, ndio maana nikasema Waziri, Mheshimiwa Mizengo K. P. Pinda na *staff* wake, wataalam wake pamoja na taasisi zake, wamekaa, wamefikiri sana. Watu wale ambao ni wataalam wa mambo ya sera, wanasema, unapotunga sera uhakikishe kwamba umefikiria mpaka kichwa kimeuma *(think until it hurts)*. Usikae tu … Kwa hiyo, Muswada huu umekuwa mpana vizuri sana.

Eneo lingine ambalo limenifurahisha ni hili la utoaji taarifa kwa wachangiaji. Ni jambo muhimu sana, nadhani hilo litasaidia hata kusukuma watu wengine waweze kuchangia zaidi ya kile kiwango kilichowekwa kisheria kwamba anapewa akaunti yake kwamba sasa mchango wako ni kiasi hiki na hii itasaidia vile vile kudhibiti wakurugenzi ambao ni wavivu wa kuwasilisha michango ya wachangiaji kwenye mfuko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuhusu faida ya vitega uchumi. Hili nalo, nadhani lingetolewa maelezo kwamba vitega uchumi hivi siyo vya Serikali, hivi ni vya wachangiaji.

Kwa hiyo, wajue kwamba kuna vitega uchumi vyao, vitajwe na waviheshimu. Itasaidia vile vile kuona kama kuna watu wanavichezea chezea, wao wenyewe kuwadhibiti. Vijulikane vitega uchumi, tena wamewekeza vizuri sana. Lile jengo lililoko Kijitonyama Dar es Salaam, kwa kweli ni zuri sana. Ukimwambia mtu yeyote kwamba limewekezwa na Mfuko wa Akiba wa Wafanyakazi, atashituka! Maana yake tumezoea kuona watu wakubwa wakubwa hawa kibiashara ndio waliokuwa wakiwekeza kwa namna hiyo na taasisi hizi kwa kweli Serikali ingeendelea kuzitumia ili isaidiwe kuwekeza. Kwa mfano, jengo hili la Bunge jipya limejengwa na muungano wa Mifuko hii. Ni heshima kubwa sana. Kwa hiyo, Mfuko huu mimi naupenda sana. Uendelee na sheria inavyokwenda hivi kama kuna mahali pa kuibadili, basi wakati wowote iletwe, sisi tutaliunga mkono hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine nadhani ni hili la kinga. Mara nyingi wafanyakazi wanakuwa na wasiwasi wakiona majengo yanajengwa na *LAPF* wanadhani fedha zao sasa hazipo. Lakini Serikali katika kile kifungu cha 53 cha kuweka kinga kwamba kama kutatokea dharura, basi fedha za mchangiaji ziko salama maana Serikali imeweka kinga ya kuweza kusaidia Mfuko na Mfuko huu kwa kuwa umetungiwa sheria mpya, basi hiyo inasaidia vile vile kwamba katika wakati huu kusiwe na mtu yeyote ambaye atakuwa na wasi wasi kwamba pengine hakutakuwa na fedha wakati anastaafu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine katika kubadili mifumo hii, ni ajira. Nashukuru sana Serikali kwamba imeweka wazi kwamba ajira zilizoko zitalindwa. Hii ni muhimu kwa sababu katika mabadiliko haya, kama wafanyakazi hawana uhakika kama watakuwepo, basi, hata utekelezaji wake unakuwa ni legelege. Lakini ni katika hali hii kwamba ajira zinalindwa isipokuwa tu pale ambapo mtu kaenda kinyume na kanuni au na sheria zilizopo. Lakini katika mabadiliko hakuna mtu ambaye anapoteza ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni lile jedwali. Nakubaliana kabisa na *amendment* iliyoletwa na Mheshimiwa Waziri ya kuongeza wajumbe watatu wa Chama

cha Wafanyakazi wa Serikali za Mitaa. Nadhani hili ni hatua nzuri sana, maana hao ndio wenyewe na ndio wangeweza kusaidia kutoa maelezo ya kuhusu Mfuko unavyokwenda na unavyofikiriwa na wale wachangiaji.

Mheshimiwa Menyekiti, isipokuwa nina tatizo, Mheshimiwa Mizengo K. P. Pinda, yeye ni Mwanasheria, nilikuwa tu natazama, hii miaka mitatu kwa *Institution building* au kujenga taasisi, ni michache sana. Miaka mitatu haitoshi kabisa kujenga taasisi. Nilikuwa nadhani, hebu tungeangalia kwa nini isiwe miaka minne au mitano, na kwa kuwa iko kwenye kanuni, haina matatizo, siyo sheria yenyewe kubwa. Kwa sababu naona sasa hii imekuwa *standard* katika kuunda taasisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naizungumza hii kwa sababu mimi nimepata tatizo kidogo. Iliundwa Tume ya Pamoja ya Fedha ya Muungano, lakini wajumbe wake wamepewa miaka mitano. Kwa hiyo, miaka mitatu ilikuwa kujenga Tume maana ilikuwa haipo. Katika mwaka wa nne, ndio Tume imeweza kukaa chini na kutulia na kufanya kazi. Kwa hiyo, huu muda utazamwe huu usiwe *standard* na tungeishauri Serikali sasa kwamba huu muda wa Bodi za Mashirika iangaliwe ili kukkidhii mahitaji ya Shirika lenyewe. Kwa sababu unapokuwa na watu kwa muda wa kutosha, unapata uelewa wa kutosha kabisa. Kwa mfano Bodi inayopendekezwa hapa, iko na wawakilishi wa aina nane. Lakini wa aina sita, wote wanaingia kwa nyadhifa zao.

Kwa hiyo ambao wanaingia kwa kuteuliwa mtu mmoja mmoja ni yule wa aina ya saba na ile ya nane ambayo Mheshimiwa Waziri ameleta *amendment* yake ya wawakilishi watatu. Sasa watu kama wale wakikaa miaka mitano au minne, watakuwa wanafaida zaidi kwa sababu wale wanaoingia kwa nyadhifa zao wanaweza kubadilika hata kila baada ya mwaka mmoja. Kwa hiyo, uzoefu unakuwepo pale na kuweza kuhakikisha kwamba taasisi hii kwa kweli inajengeka vizuri sana. *(Makofi)*

Mimi huu ndio mchango wangu, lakini zaidi ni kuimarisha na naunga mkono kabisa na kwamba sheria hii kwa kweli isicheleweshwe na tunamuomba Mheshimiwa Waziri Mkuu ahakikishe kwamba inapelekwa, inaidhinishwa mapema ili kasi iwe nzuri katika kuleta mabadiliko ya mfumo huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana!

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA - MWENYEKITI:** Mheshimiwa William H. Shellukindo, ahsante sana kwa mchango wako.

Waheshimiwa Wabunge, naomba sasa nimwite Mheshimiwa Dr. Omar Nibuka na Mheshimiwa Ezekiel Maige naye ajiandae.

**MHE. DR. OMAR M. NIBUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia katika Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijachangia, kwanza ningeomba nitoe rambirambi zangu za dhati kwa kifo cha Daktari mwenzangu, Dr. Kanyika ambaye ni

miongoni mwa Madaktari waliofariki kule Nigeria na habari nilizozipata ni kwamba huenda mwili wake ukaletwa kesho Dar es Salaam na baadae ukapelekwa Morogoro kwa ajili ya mazishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuwapa rambirambi ndugu wa marehemu Dr. Kanyika, lakini pia naomba nichukue nafasi hii kutoa rambirambi kwa wananchi wote wa Manispaa ya Morogoro, kwa sababu Dr. Kanyika alikuwa akifanya kazi kwenye Hospitali ya Mkoa wa Morogoro na alikuwa akitoa huduma kwa wananchi wote wa Manispaa ya Morogoro. Naomba Mwenyezi Mungu ailaze mahali pema roho yake peponi, *Amini.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa bahati mbaya Madaktari wote wawili waliofariki Nigeria, mimi nilisoma nao akiwepo pamoja na Dr. Kanyika. Kwa kweli nina uchungu mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nataka kuchukua nafasi hii kutoa rambirambi zangu kwa Mzee wetu Peter Siyovelwa ambaye alizikwa jana kwa heshimia kubwa. Kwa hiyo, naomba nitoe rambirambi zangu kwa ndugu zangu wa Mkoa wa Iringa kwa msiba mkubwa ambao umewapata lakini pamoja na nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba niende kwenye kuchangia Muswada. Kwanza, naomba nimpongeze Waziri mwenye dhamana kwa jinsi alivyouwasilisha huu Muswada na pia naomba niipongeze Kamati ambayo iliongozwa na kaka yangu Mheshimiwa Charles Keenja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu ni Muswada muhimu hasa kwa wafanyakazi wa Serikali za Mitaa kwa maana ya kuboresha maisha yao. Lakini kitu ambacho nilitaka kupata wasi wasi kidogo ni kwamba, sina uhakika kama wafanyakazi hawa wameshirikishwa kiasi gani katika dhima nzima ya kuuleta Muswada huu. Lakini kama hawajashirikishwa, bado nafasi tunayo. Ningeomba basi wafanyakazi hawa wapate elimu ya kutosha kwa njia ya warsha au semina ili waweze kuelewa na wao wakachangia katika jambo ambalo wao ndio wadau wakuu na wao ndio wanahusika zaidi na Muswada huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba nichukue nafasi hii kwamba wafanyakazi hawa wa Serikali za Mitaa ni kama walivyo wafanyakazi wa Serikali Kuu, ni wafanyakazi ambao wanafanya kazi katika mazingira magumu, katika hali ngumu kwa maana ya mafao duni. Kwa hiyo, ningeomba Serikali iwaboreshee mafao yao kwa maana ya huduma zao hasa katika suala la matibabu. Matibabu kwa maana ya wafanyakazi wenyewe na familia zao, aidha, kwa kupitia Mfuko wa Bima ya Afya au kwa namna yoyote ile. Hasa hapa ni pamoja na kuboresha sehemu zinazotolewa huduma kwa maana ya hospitali na kuwe na vifaa vya kutosha vya matibabu lakini na dawa ambazo zingeweza kuwasaidia, kwa sababu vinginevyo watakuwa hawana njia nyingine kubwa na nzuri ya kuweza kuwasaidia katika sehemu hii ya matibabu. Lakini pia wafanyakazi hawa wana matatizo mengi tu ikiwemo pamoja na mishahara licha ya kuwa duni, lakini mishahara hii pia hawapati kwa wakati muafaka na hawana uhakika wa kujua kwamba mshahara wake mtumishi ataupata lini kwa sababu ni kitu kinacho *fluctuate*, leo amepata

tarehe 2, kesho tarehe 5, mwezi huu tarehe 30, basi. Kwa hiyo, ni kama vile mtu hana uhakika wa kupata mshahara wake wakati ni haki yake kama mtumishi wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ningeomba pia nichukue nafasi hii kuikumbusha Serikali kwamba wafanyakazi hawa wanatoa mchango mkubwa kwa Serikali. Kwa hiyo, ingekuwa ni wakati muafaka sasa Serikali katika mafao ya wafanyakazi kwa maana ya upandishwaji wa vyeo, pia wapandishwe vyeo vyao kwa muda muafaka ili wapate hamasa ya kuweza kulihudumia taifa pamoja na wananchi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nichukue nafasi hii pia, pamoja na suala hilo, waweze pia kupatiwa masomo ili waweze kuwa na ujuzi wa kutosha kwa ajili ya kutekeleza majukumu yao ya kila mara. Kwa hiyo, kwa sababu tayari leo tunapitisha au tunajadili Muswada huu wa Pensheni ya wafanyakazi, kwa hiyo pensheni hii nafikiri ingekuwa wakati muafaka sasa waweze hata ikiwezekana wakopeshwe wafanyakazi hawa ili waweze kupata elimu ya kutosha kwa faida ya nchi na wao wenyewe ili watakapopata elimu kama alivyozungumza mzungumzaji aliyepita kwamba watakapokuwa na elimu kubwa, maanake na mafao yao pia yanaongezeka. Lakini si kukopeshwa kwa ajili ya elimu tu, lakini pia wanatakiwa pia wakopeshwe ili waweze kujiendesha kiuchumi kwa maana ya aidha kwa kupata uwezo wa kulima au kujenga hata nyumba kwa ajili ya maisha yao ya baadae wakati watakapostaafu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la Mheshimiwa Waziri kusimamia Bodi hii ya Mfuko wa Pensheni, mimi sina tatizo, naunga mkono kwa asilimia mia moja kwa sababu Bodi ni watu, lakini Waziri ni mtu mwenye dhamana kubwa na ambaye tunamtegemea kwa kufanya maamuzi. Kwa hiyo, inawezekana kwenye Bodi kukawa na tatizo ambalo Waziri anaweza akalirekebisha kwa kutegemea majukumu aliyokuwa nayo na ujuzi aliokuwa nao. Kwa hiyo, ningependa suala la Waziri kusimamia Bodi libaki pale pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kitu kinachonisikitisha katika Muswada huu ni kwamba, inavyoonekana katika *reform* iliyofanyika katika Serikali za Mitaa, imejali zaidi masuala ya watumishi kwa maana ya watendaji. Lakini halizungumzii kabisa wasimamizi wao au waajiri wao wakuu ambao ni Waheshimiwa Madiwani. Sasa ningefikiri wakati umefika kwa Serikali za Mitaa au Wizara husika izungumzie mafao ya Waheshimiwa Madiwani ambao wao ndio wasimamizi wakuu wa watendaji hawa katika Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Madiwani ni watu ambao wanafanya kazi katika mazingira magumu lakini kwa kipato kidogo sana. Lakini tukubali wazi kwamba Madiwani hawa ndio Wabunge wadogo. Diwani ni Mbunge mdogo na katika majukumu yetu ya kuwahudumia wananchi, sisi Wabunge tunawategemea sana Madiwani katika kuboresha kazi zetu ili wananchi waweze kupata huduma ya kufaa. Lakini hatuliangalii suala hili. Utakuta Madiwani wanapata posho ndogo, kwa mfano shilingi 30,000/=, shilingi 30,000/= mtu atafanyia nini! Huwezi kununua hata shati la kisasa!

Kwa hiyo, nafikiri ingekuwa wakati muafaka sasa tuangalie hata posho za hawa wasimamizi wakuu wa watendaji katika Serikali za Mitaa ambao ni Waheshimiwa Madiwani na wao tuwaboreshee maslahi yao. Mimi ningependekeza kwa wakati tulionao, nafikiri kama basi posho zao isifike laki moja, basi angalau isiwe chini ya shilingi 50,000/= ili na wao angalau waweze kutekeleza majukumu yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa Madiwani kama tulivyo sisi Wabunge, kwenye majumba yao kila siku wanafuatwa na wananchi kwa ajili ya kuwaomba msaada kwa sababu wananchi wanafikiri Diwani ni mtu mwenye kipato kikubwa ambaye anaweza akawasaidia kwa jambo lolote, kumbe Diwani hana mshahara na posho yake ni ndogo ambayo haiwezi kukidhi haja hata kwa maisha yake yeye na watoto wake. Lakini, bado pia wananchi wanategemea msaada wa Diwani. Kwa hiyo, nafikiri tungeangalia suala hili kwa undani zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini wakati wa kuangalia Madiwani, pia tungeangalia na wadau wakuu ambao ni Wenyeviti wa Serikali za Mitaa. Hawa nao ni Madiwani wadogo katika nafasi zao. Wenyeviti hawa wa Serikali za Mitaa wana majukumu makubwa mno katika kutekeleza au kusimamia kuboresha utendaji kwa wananchi wanaoishi kwenye *Council* hizi kwa sababu itakumbukwa kwamba kwa hivi sasa Serikali ime-*introduce* utaratibu wa kuwapata Watendaji wa Mitaa. Watendaji wa Mitaa hawa kwa bahati nzuri wanalipwa mishahara. Lakini Watendaji wa Mitaa hawa wako chini ya hawa Wenyeviti wa Mitaa na wakati mwingine Wenyeviti wa Mitaa, nyumba zao ndio zinatumika kama ofisi za Watendaji wa Mitaa. Sasa utakuta anayesimamiwa anapata mshahara, lakini yule anayesimamia hata hawezi kupata hata posho, kwa hiyo, inamkatisha tamaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jambo hili, kwa hiyo, nilifikiri wakati umefika kwa Serikali hasa Waziri mwenye dhamana kwa vile ananisikiliza, ni kwamba na wao Wenyeviti wa Mitaa ni wakati muafaka sasa angalau tuwape posho, hasa ningependekeza labda hii posho ambayo walikuwa wanapata Madiwani shilingi 30,000/=, sasa tuwape Wenyeviti wa Mitaa ili Madiwani tuboreshe zaidi posho zao ili tuweze kufanya kazi kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii sasa, liko jambo ambalo linanikera, jambo hili ni kwamba katika utaratibu wa Serikali za Mitaa au kanuni inasema kwamba asilimia kumi ya mapato katika Serikali za Mitaa, ni kwamba yaende kwa makundi au yasaidie makundi ya akina mama na vijana ili tuweze kuboresha maisha yao na katika sera yetu ya nchi, tumesema kwamba kila mtanzania aweze kupata maisha bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini katika utaratibu huu wa makusanyo ya asilimia kumi katika Manispaa zetu au katika *Council* zetu, ni kwamba utekelezaji haufanyiki! Hii nafikiri inatokana na Wakurugenzi kulimbikiza makusanyo, kwa sababu unapolimbikiza makusanyo, utakujakushitukia kwamba deni ni kubwa ambalo ungeweza kukata kwa ajili ya kuboresha ili akina mama na vijana waweze kupata mikopo ya kuwasaidia. Sasa, kwa sababu wanalimbikiza, wanashindwa kutekeleza kwa sababu hela zitakuwa ni nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, pendekezo langu ningefikiria kwamba makusanyo ya kila mwezi zitolewe zile asilimia kumi kwa maana ya asilimia tano kwa vijana na asilimia tano kwa akinamama ili ziende kwenye akaunti maalum ili ziweze kuwasaidia, kwa sababu bila kufanya hivyo, wananchi wetu hawawezi kupata maisha bora kwa maana ya kwamba hata hizi bilioni moja zilizotolewa na Serikali kwa kila mkoa, haziwezi kumfikia mwananchi kwa sababu hazitoshi.

Kwa hiyo, nafikiri hizi hela za makusanyo za Manispaa zingekuwa muafaka kabisa kuwasaidia wananchi wetu ili hatimaye wawe na maisha bora kwa njia ya kuwapatia mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi nilikuwa naomba kwa leo nizungumze kidogo tu ili kabla kengele ya pili haijanigongea, huo ndio mchango wangu katika kuchangia hii *agenda* ya Mfuko wa Pensheni wa *Local Government*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nasema kwamba naunga mkono hoja asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA - MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Dr. Omar Nibuka kwa mchango wako. Sasa, naomba nimwite Mheshimiwa Ezekiel Maige na Mheshimiwa Lekule Laizer, naye ajiandae.

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie Muswada wa Sheria wa Mfuko wa *Pension* wa *Local Government*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko huu wa *Pension* ya *Local Government* kwa ujumla wake uko katika mfumo mzima wa *pension* katika nchi na pia unagusa mfumo mzima wa hifadhi ya jamii katika nchi yetu. Kwa hiyo, nitapenda kuchangia kwa kuangalia maeneo yote mawili. Kwanza, nitapenda nizungumzie mapungufu ambayo nafikiri yako katika mfumo mzima wa *pension* katika nchi au tuseme hifadhi ya jamii katika nchi yetu kabla ya kuangalia hasa mapungufu ambayo mimi nafikiri yapo katika Muswada huu ulioletwa hapa mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda ku-*approach* suala hili kwa njia hiyo kwa sababu mbili.

Kwanza, kwa jinsi hali ya sasa ilivyo kwamba tuna mifuko mingi, kila mfuko umeundwa kwa sheria yake. Kila mfuko una taratibu zake na mifuko yote inakuwa inamhusu mfanyakazi, kunapotokea matatizo anayekuwa anaathirika zaidi ni mfanyakazi. Kwa sababu hiyo, nilifikiri ni vizuri nikajaribu ku-*highlight* mambo fulani fulani ambayo nafikiri ni vizuri Serikali ikayaangalia mapema na pengine ingefaa zaidi kuangalia suala la *National Social Security Policy* mapema kabla hata ya kuzungumzia mfuko mmoja mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko wa Hifadhi ya Jamii, katika nchi yetu una mapungufu mengi. Kama nilivyosema tuna mifuko mingi kila mfuko una utaratibu wake wa uchangiaji kwa mfano kuna mifuko ambayo mwajiri anachangia asilimia 10 na mwajiriwa anachangia asilimia 10. Kuna mifuko kama huu ambao sasa tuna Muswada wake tunaupendekeza hapa ambao baadaye tutaupitisha, mwajiri anachanga asilimia 15 na mwajiriwa anachanga asilimia 5.

Lakini vile vile kuna tofauti ya mafao katika mifuko mbalimbali. Kuna mifuko mingine kwa mfano inatoa *education benefit* kama hapa tulivyoona kwenye Muswada huu tunaoujadili, mifuko mingine haina. Sasa kwa ujumla wake kunakuwepo na matatizo hasa linapokuja kutokea suala la mfanyakazi kubadili mwajiri. Lakini pia kwa ujumla mifuko hii inapokuwa mingi inapunguza uhuru wa mfanyakazi kuchagua ni mfuko upo ajiunge nao. Kwa mfuko huu ambao tunauzungumzia kwa sura yake unaonekana kama unataka kuweka ukiritimba kwa wafanyakazi wa *Local Government* kwamba ni lazima wajiunge na mfumo huu. Lakini pia miaka michache iliyopita Mfumo wa *Social Security* katika nchi ulikuwa *liberalized in which case* wafanyakazi wanaruhusiwa kujiunga na mifuko mbalimbali wanayokuwa wanaipenda. Sasa kwa mazingira haya naona kama kuna *contradiction* kwa kuwa huu mfuko unasema kwamba wafanyakazi wa sehemu fulani wote waingie kwenye mfuko huu wakati kuna mifuko mingine ambayo sheria yake iko tofauti, maana yake kutakuwepo na tatizo la kuingiliana kwa hawa ambao ni wachangiaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sura ya mifumo hii tuliyonayo, mfanyakazi anakuwa hana uhuru wa kuchagua. Kwa mfano, katika mapendekezo haya tuliyonayo, kifungu kimojawapo kinasema kwamba, mfanyakazi kama anafanyakazi kwenye *Local Government* akitoka michango yake, kule anakoenda kuajiriwa sehemu ya pili, yule mwajiri wake aendelee kuwa *contributing employer* wa hii ambayo hii sasa baadaye itakuwa nafikiri *Local Authority Pension Fund (LAPF).*

Kwa sura hiyo, maana yake ni kwamba kama yule mwajiri kwa mfano alikuwa anachangia kwenye mfuko ambao unachangia 10%, tuseme mwajiri yule anachangia tuseme *NSSF* akaja mfanyakazi ambaye alikuwa ameajiriwa kwenye Halmashauri fulani, labda tuseme kwenye Hospitali ya Wilaya, akaja akaajiriwa na hiyo *private hospital* au huyo mwajiri, maana yake kutakuwepo na *staff* mmoja ambaye *employer* atalazimika kuchangia asilimia 15 kwenye ule mfuko wake wa *Local Authority in this case* itakuwa *pension fund*. Lakini pia wale *staff* wake wengine watakuwa wanawachangia kwenye mfuko mwingine. Katika mazingira hayo kutakuwepo *complication* kwa mwajiri. Mwajiri ukimpa *choice* kwamba achague anajiunga na mfuko upi ni dhahiri atapenda kuchanga kwenye mfuko ambao mzigo kwake utakuwa ni mdogo. Kwa mazingira hayo nilifikiri jambo hili kwa ujumla wake ni vizuri tukaomba Serikali ikajaribu kuboresha mfuko mzima wa hifadhi ya jamii katika nchi ili kusiwepo matatizo katika waajiri kama huo mfano niliutoa.

Lakini vile vile hata uhuru wa kuhama kwa wafanyakazi kwa mfano pia katika suala zima la kuhama kwa wafanyakazi kuna tatizo la *portability* ya *contributions* ya *employee* kama *employeee* alikuwa anafanyakazi kwa mwajiri ambaye ni *contributing*

*employer* wa mfuko fulani akahama akaenda kwingine, michango yake iliyokuwepo kule ni vigumu kusema kwamba itatambulika kwenye mfuko mwingine ambako anahamia.

Kwenye huu Muswada tunazungumzia hapa kwenye kifungu namba 39 kimezungumzia suala la *back purchase* kwamba eti huu mfuko tunaozungumzia utaweza kununua *contributions* au *benefits* kutoka kwenye ule mfuko wa awali. Sasa hapo kutakuwepo na matatizo kununua *contribution* ya mfanyakazi aliyekuwa kwenye mfuko mwingine ili uje kwenye huu mfuko ambao tunauzungumzia halafu tuweze kum-*include* huyu mfanyakazi kwenye *scheme* ninaona kutakuwepo na matatizo na hili litatusumbua.

Kwa hiyo, ni vizuri jambo hili tukaliangalia mapema kabla halijaanza kuleta matatizo na kama ambavyo sasa hivi linaleta matatizo na anayekuja kuumia zaidi ni mfanyakazi. Kwa sababu *option* inayokuwa imebaki kwa mfanyakazi, mara zote ni ku-*withdraw* kitu ambacho naamini si malengo hasa ya *pension*. Kama neno lenyewe *pension* lilivyo ni kwamba linalenga kumsaidia mfanyakazi pale ambapo atakuwa amekosa uwezo wake wa kufanyakazi aidha kwa kuzeeka au kwa kupata janga fulani katika kazi yake. *(Makofi)*

Sasa kwa sababu mifuko hii inakuwa haiingiliani kimafao yaani hayafanani, lakini pia michango haitambuliwi na kuhamia kwenye mfuko mwingine, matokeo yake ni kwamba wafanyakazi wanalazimika ku-*withdraw,* anapo-*withdraw* anakwenda kuanza upya, maana yake na umri unazidi kwenda, *chances* za kujikuta kwamba anakuwa *pensioner* kwenye mfuko fulani zinapungua *at the end of the day* anakuja kulipa *gratuity* tu kwa sababu aidha ana-*retire* baada ya kuwa alikuwa anahama hama kwenye mifuko iliyo mingi. Kwa hiyo, nilikuwa nataka kuomba tu kwamba Serikali kwa ujumla ijaribu kuangalia tatizo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nijaribu kupitia mapungufu yaliyoko kwenye sheria hii ambao tunaipendekeza hii ya sheria ya Mfuko wa *Pension* ya wafanyakazi *wa Local Government.* Eneo la kwanza nilikuwa naona lina matatizo ni kwenye uwakilishi katika Bodi ya Wafanyakazi. Nimejaribu kupitia kifungu namba 10 (1) na jedwali la kwanza, ukiangalia bodi jumla inaleta kama watu 10, hawa watu 10 ni 3 tu ambao wanatoka kwa mwajiriwa *(employees).* Wako wawili *Permanent Secretaries*, halafu mwingine *Attorney General,* halafu pia wanakuwepo wengine wawili kutoka *ALAT* ambao pia ni sehemu ya mwajiri kwa sababu *ALAT* inajumuisha wajumbe ambao ni Madiwani na Mkurugenzi. Halafu pia wengine ni wajumbe wawili wanaokuwa *appointed* kwa *paragraph* 1(1)(g) kinasema kwamba watachaguliwa wawili kutoka wenye *private sector* kwenye uzoefu na mambo ya *social security*.

Katika mazingira hayo yawezekana kutokana na *discretion* ya Waziri wakawa ni waajiriwa *fine* lakini *chances* za kwamba wakawa ni waajiriwa ambao wanachangia kwenye mfuko ule ni ndogo. Kwa mazingira hayo ni kwamba wafanyakazi wanakuwa wamewakilishwa na wajumbe watatu katika bodi. Sasa hili linawanyima nafasi ya kujadili mambo yao na mwisho wa siku watajikuta tunakuwa kwenye malalamiko kama ambayo tunayo kwenye mifuko mingine kwamba wafanyakazi hatusikilizwi, fedha zinakuwa *invested* lakini hatufaidiki na hicho kinachojitokeza huko.

Kwa hiyo, nilipenda ni vizuri kabisa nimwombe Mheshimiwa Waziri kwamba mapema iwezekanavyo kabla na yeye hajaingia kwenye mtego huo wa malalamiko basi ni vizuri akalikumbuka kulirekebisha hilo ule mfumo mzima wa bodi.

Lakini ni uhuru wa bodi katika kuamua, kifungu namba 49 wachangiaji wengine wamekizungumzia. Kinampa nafasi Waziri kuweka mkono wake katika majadiliano ya bodi katika uwekezaji. Bahati mbaya kifungu hicho hakijasema ni wakati gani bodi ifanye *consultation* kwa Waziri. Hata wakitaka kuwekeza kwenye nyumba ya milioni 15 kwa jinsi kifungu kilivyo maana yake lazima Waziri awe *consulted*. Kwanza, *process* yenyewe inakuwa ni *complicated*, lakini lingine la pili ni kwamba kukija kutokea tatizo kunakuwa hakuna *independence* kwa sababu katika hali ya kawaida nilikuwa nategemea kunapotokea *external auditor* akachungua *(deeds)* shughuli za mfuko ule ambayo ni maamuzi yatakuwa yamefanywa na bodi atayapeleka kwa Waziri husika ambaye ndiyo mwenye uwezo hata wa kuivunja bodi. Sasa katika mazingira hayo kama Waziri mwenyewe kulikuwa na mkono wake maana yake ni kwamba uamuzi wa kusema ni nini kifanyike pale ambapo maamuzi yale yalikuwa siyo sahihi inakuwa ni tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu kingine ambacho nilitaka nizungumzie ni mfumo mzima wa mafao. Haya mafao nina wasiwasi kama ni *demand driven*. Tumekuwa na kasumba ya ku-*import* au kuchukua mafao kwa ujumla, *maternity, invalidity,* sijui na nini, lakini sidhani kama mafao tuliyoya-*stipulate* hapa ni yale ambayo kweli wafanyakazi wangeweza kuyapenda. Nina wasiwasi kuna mafao mengine kwa mfano sijui mafao yanayohusu maziko na nini pengine wafanyakazi wangeweza kupenda mafao ya aina nyingine tofauti. Sasa hilo pia nilikuwa nafikiri ni tatizo ambalo ni vizuri tukaliangalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mfuko wa mafao huo huo nafikiri Mwanasheria wakati anatengeneza *draft* hii kidogo alikuwa amejikita sana kwenye historia kwa sababu lugha iliyotumika haijazingatia suala la *gender*. Ukiangalia kifungu namba 29(1)(a) kinazungumzia pale mwanaume anapokuwa amekufa na jinsi ambavyo *maintenance* itaweza kulipwa kwa mke. Sasa haijaeleza kwamba mume anapokufa ambaye mume ni *dependant* halafu akafa yule mama ambaye ndiyo mwajiriwa ambaye ndiyo *contributing employee* kwamba *the same should apply* kwa mwanaume. Kwa hiyo, nilifikiri ni vizuri tu tukawa *gender sensitive* kama ambavyo uelekeo wa dunia ya sasa ulivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda kwa kumalizia nilipenda kuzungumzia suala la ukokotoaji wa *pension*. Kifungu namba 36 kimependekeza kwamba *pension* ikokotolewe kwa kuangalia *contribution* ya mwaka wa mwisho yaani miezi 12 ya yule *contributing employee*. Katika mazingira ya sasa ambayo wafanyakazi wanabadili waajiri mara kwa mara na mishahara ya waajiri inabadilika nilifikiri ni vizuri tukichukua wastani wa kipindi kirefu zaidi ili kuangalia *the best period* ambacho mfanyakazi alikuwa analipwa mshahara mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yawezekana tunaweza tukasema tukaangalia wastani au tukaangalia *the best salary in the past five years* au *the best salary in the past four*

*years* kuliko kuangalia mwaka mmoja wa mwisho kwa sababu inawezekana mtu alikuwa anafanyakazi sehemu halafu akajikuta anakwenda kwa mwajiri mwingine kama nilivyosema *Local Government* inasema kwamba itakuwa inaangalia *contribution*. Kwa kuangalia kifungu nilikisema kifungu namba 15(3) kwa mazingira hayo ni kwamba kama yule mwajiri wa mwisho atakuwa anatoa mshahara mdogo na tukaangalia mshahara ule wa mwisho *at the end of day pension* ya yule *employee* itakuwa ni kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia muda nilikuwa naomba kwanza niseme tu kwamba kwa ujumla nina *support* hii *bill*. Lakini ningefurahi sana kwamba haya marekebisho ya msingi yakizingatiwa ili walau kupunguza matatizo ambayo *ready* tuna *experience* katika mifuko mingine ili mfuko huu uende vizuri na uwe na *good lessons* ambazo tumejifunza toka sehemu nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi hii naomba kuishia hapo. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakupongeza kwa kunipa nafasi ili na mimi nichangie Muswada huu ulioletwa na Waziri wa Nchi, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Lakini ningependa kwanza na mimi nitoe rambirambi kwa famili ya marehemu Peter Siyovelwa, kwa kweli alikuwa mtaalamu sana katika mambo ya Halmashauri, ametoa semina mbalimbali kwenye ngazi mbalimbali mpaka hata Serikali za Mitaa karibu kila Halmashauri wanamfahamu kwa sababu alitoa elimu katika karibu Halmashauri zote na sio Halmashauri tu hata sisi Chama cha Mapinduzi kwa kweli alikuwa mwalimu wetu ambaye ametoa mchango mkubwa sana katika chama, ametoa semina mbalimbali alikuwa anazunguka kutoa elimu katika Chama cha Mapinduzi, kwa hiyo alikuwa ni *asset* kubwa katika Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ningependa kuunga mkono Muswada huu. Ni Muswada mzuri sana, tunampongeza Waziri kwa kuleta Muswada huu hapa Bungeni. Kwa kweli mfuko huu ni mifuko ambayo inawasaidia sana wadau hasa baada ya ku-*retire,* unajua unapokuwa kazini, bado huoni ugumu sana kwa sababu una mapato, lakini siku ukiondoka, hapo ndiyo utaanza kuona shida nyingi zaidi. Kwa hiyo, mfuko huu ukiimarika utasaidia sana watumishi wa ngazi mbalimbali, kwa hiyo, tunakupongeza sana Mheshimiwa Waziri, pamoja na Kamati iliyojadili na kuleta mapendekezo hapa Bungeni tujadili na nadhani tutaupitisha.

Ningependa na mimi niboreshe baadhi ya sehemu, unajua mfuko huu mimi ningependa kusema kwamba mfuko huu, uwe ni mfuko ambao utakuwa wazi kwa wadau. Kwa sababu wadau wasipopata taarifa ya mapato na matumizi watakuwa na wasiwasi hata na kuchangia itakuwa ni kazi ngumu, au malalamiko yatakuwa makubwa sana.

Kwa hiyo, inafaa mfuko huu kila mara uwe wazi. Inafaa itolewe taarifa, tunakumbuka nadhani wengi mko katika mifuko mbalimbali ya *shares,* kama *TBL*, *Tanga Cement,* wanajaribu kila wakati kutoa taarifa kuwapa wadau taarifa na mfuko huu inafaa wadau nao wapate taarifa wajue kwamba imekuwaje. Kwa hiyo, uwazi wa mapato na matumizi uwe bayana ujulikane kwa wadau wa mfuko huu.

Jambo lingine ni ukaguzi wa mahesabu, huu ukaguzi wa mahesabu mimi ningeomba iwe tofauti na ukaguzi wa Halmashauri zetu, ukaguzi wa Halmashauri zetu, ni ukaguzi wa maajabu, ajabu sana, kwa sababu mwaka huu ukaguzi unaokaguliwa ni hesabu za mwaka 2004/2005, bado za mwaka huu 2006 zitakwenda kukaguliwa mwakani. Hii inaleta shida sana, hata wale watu ambao wametumia vibaya hizo fedha utampata mwingine amehamishwa amekwenda kula fedha hizo hizo, katika Halmashauri zingine, yaani ameibia Halmashauri tatu, kabla hesabu zake hazijagundulika.

Kwa hiyo, naomba mfuko huu uwe mahesabu yawe yanaendana mwaka hadi mwaka isichelewe kama zile Halmashauri zinavyofanya. Unakuta mwingine ametumia fedha ya mfuko, hesabu hazijakaguliwa, mwakani kukaguliwa hayuko tena, amefukuzwa kazi au amefariki itakuwa ni kuleta kila siku mahesabu ya kufuta kama zile za Halmashauri.

Jambo lingine ni bodi ya wadhamini, bodi hii ingefaa iwe ni bodi ambayo inabuni miradi, hizi fedha sio fedha za kuweka kwenye akaunti, ni fedha za kuweka kwenye miradi, uzalishaji, uwe mfuko endelevu na bila kuwa na watu ambao ni wabunifu kwa kweli mfuko huu utalegea sana hautakuwa mfuko ambao unaweza baadaye ukawa na faida kwa wadau.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kama niseme tu kwamba wadau wanapokatwa au wanapolipia mfuko huu, kwa kweli naona kwamba makato ni makubwa kwa sababu anapanga mahitaji yake. Lakini baadaye wakati wa kulipwa, kupokea unapolipwa, mafao yako hapo ndiyo utaona faida ya mfuko, lakini tatizo linakuja siku hiyo inapofika wakati wa kudai mafao yao, yaani kukatwa kudaiwa ni haraka sana unakatwa kila mwezi. Lakini siku ya kupewa haki yako inakuwa ni nongwa, unazungushwa, unazungushwa, nenda rudi, nenda rudi. Sasa Waziri hapa mmejiwekea utaratibu wa kumshitaki mtu ambaye halipii mfuko au mtu ambaye halipi ule mchango.

Lakini sikuona utaratibu namna huyu mdau yeye anapokosa haki yeye afanye nini, kwa sababu hizi fedha hazina tofauti na akaunti yako uliyoweka fedha zako zilizoko kwenye akaunti. Hivyo unapokatwa kila siku, hizo fedha mdau anahesabu kwamba ziko kwenye akaunti yake, ukienda siku yoyote kwenye akaunti kama kuna fedha, sidhani kuna usumbufu wowote na nasema kwamba na hawa ikifika siku ya kulipwa asizungushwe.

Kama wanavyofanya *Insurance*, hasa kwa kweli ukiangalia fedha zinazolipwa kwenye, wanaolipia magari hasa *comprehensive insurance* unapolipa milioni, kila mwaka milioni tatu, milioni mbili lakini ukifika siku ya kudai, gari imepata ajali unaweza kuzungushwa miaka miwili. *(Makofi)*

Lakini ukihesabu milioni mbili mbili ulizolipa kwa miaka unakuta ni pesa zaidi ya manunuzi ya gari. Lakini kupata hizo fedha ni shida, mimi nahesabu kwamba hiyo ni dhuruma na ni wizi wa hali ya juu, na mfuko huu usije ukawa kama hizo za *insurance* ambayo mtu anazungushwa nenda rudi, nenda rudi, lakini siku moja ikipita mwezi

hujalipa *insurance* gari inakamatwa, usumbufu mkubwa sana. Kwa hiyo, naomba huu mfuko uwe ni mfuko ambao unawasaidia wananchi.

Ningependa kuungana na Kamati, walisema tuwaangalie Madiwani, waaingizwe katika mfuko huu, kwa kweli nakubaliana mia kwa mia. Kazi ya Madiwani ni kazi kubwa sana. Lakini wanachopata utashangaa, unajua wananchi hawajui kwamba madiwani wanalipwa 30,000, hawajui kabisa.

Sasa Madiwani wanatumiwa kama shoka. Ukitumia shoka haidai chochote ndivyo Madiwani walivyo. Madiwani ni wasimamizi wa fedha za Halmashauri. Ukisema tu Halmashauri unakumbuka Madiwani. Huo mfuko lazima Madiwani nao watashiriki kuwa ni sehemu ya kulinda huu mfuko. Kwa hiyo, Madiwani wawekwe mfuko huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hiyo tu, sidhani hata hiyo 30,000 utakata nini, kwanza hiyo posho yao ikifikishwe 100,000 ndiyo uweze ukaangalia kwamba atakatwa nini? Kwa hiyo, ningesema hatuwezi kabisa ukachukua sehemu ya watendaji kwenye Halmashauri, ukawaweka kwenye mfuko ukawaacha watu wengine ambao ni muhimu sana. Madiwani ni muhimu kwenye Mfuko huu wasitengwa kabisa na watendaji wengine. *(Makofi)*

La mwisho ningependa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri na kudumu katika Wizara hii. Mimi nimefurahi kabisa yale mabadiliko ya juzi yalivyokukwepa kwa kweli unafaa katika Wizara hii. Umefanya makubwa katika Wizara hii ulipokuwa Naibu ndiyo maana ukapandishwa ukawa *full Minister. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA - MWENYEKITI:** Nakushukuru Mheshimiwa Lekule Laizer na hasa kwa hizo pongezi zako. Wote tunajua umahiri wa Mheshimiwa Pinda kwenye Wizara hii. Kwa hiyo, tunamtakia kila la kheri. Sasa naomba nimuite Mheshimiwa Siraju Kaboyonga na kama nilivyosema yeye ndiyo atakuwa msemaji wetu wa mwisho kwenye shughuli ya asubuhi hii. *(Makofi)*

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie mawazo yangu kidogo kwenye Muswada ulio mbele yetu wa *Local Authority Pension Fund*. Awali ya yote na mimi niungane na wenzangu wengine kutoa salaam za rambirambi kwa familia ya marehemu Peter Siyovelwa na baada ya rambirambi hizo, sasa niende moja kwa moja katika mjadala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mjadala huu kama walivyosema baadhi ya waliotangulia kuzungumza umekuja wakati ambapo Serikali ilikwishapitisha sera ya ustawi ya hifadhi ya jamii hapa nchini, sera ambayo iliweka msingi wa baadaye kuwe na sheria ya hifadhi ya jamii kinchi. Lakini kwa sababu ambazo hatuzijui mpaka leo sheria ya ujumla kinchi inayoshughulikia suala zima la hifadhi jamii haijaja mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na hali hiyo, ndiyo maana sasa tunaendelea kujadili mifuko ya *pension* ya *institutions* au ya *specific areas* peke yake. Basi na mimi nitaujadili mfuko huu kwa mtiririko huo huo. Lakini nilidhani niseme kwamba ingelikuwa vizuri sasa tungekuwa tunazungumzia Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Kitaifa kwa ujumla.

Katika mapendekezo yaliyoko mbele yetu katika Muswada huu nimeangalia mafao ambayo yatatolewa na mfuko huu. Kwa kiasi kikubwa yanafanana sana na mafao ambayo yanakubalika kimataifa na Shirika la *International Labour Organization* ili mfuko unaotoa mafao yanayofanana na hayo uweze kujulikana kama mfuko wa Hifadhi ya Jamii. Kwa maana hiyo, nilikuwa napendekeza hata jina la mfuko huu libadilike liwe ni *Local Authority Social Security Fund.* Kwa sababu kwa kweli *it is not Pension Fund persay.* Ni *Social Security Fund,* lakini *specifically* ya *Local Authorities.*

Mapendekezo mengine ni kama ifuatavyo:-

*Section* ya nane, kifungu cha tatu kidogo pale, panasema kwamba *the Board may appoint other Officers* na inaendelea. Sasa inatoa tatizo kidogo kwamba Bodi ita-*appoint other Officers,* wepi? Ni vizuri basi katika hili Sheria ikawa wazi ikijua kwamba kuna *appointments* nyingine ni za *management* na *appointment* nyingine ni za Bodi.

Kwa hiyo, niseme tu kwamba *appointments* kuanzia *level* fulani mpaka huko juu zitakuwa ni za Bodi. Sheria iseme hivyo ili ijulikane wajibu wa Bodi kwenye masuala ya *appointment* na wajibu wa menejimenti kwenye masuala ya *appointments.*

*Section 13(b)* inazungumzia kwamba likitokea tatizo na hii *fund* kuwa *under funded, then the Board may recomend to the Minister a revision of the rates* za *contribution.* Sasa hivi kwa mujibu wa Sheria hii tunayoizungumzia, Muswada tunaouzungumzia *level* ya *contributin* ni *20% in total.* Mfanyakazi anatoa *5%* na mwajiri anatoa *15%.* Sasa *level* hii imefikiwa. Nataka niamini imefikiwa kitaalam na maana ya utaalam ni katika masuala haya ni kwamba bila shaka atakuwa ameitwa Mtaalam anaitwa *Actuarial,* wakati tunau-*transform* mfuko wetu huu *Provident Fund* kuupeleka kwenye *Pensio Fund.*

Nataka niamini kwamba, moja ya kazi kubwa ambayo imefanyika ni kumwajiri mtaalam *wa Actuarial* ambaye amekuja na kuutathmini na kuupa muda karibu miaka 10 au 20 mbele kuona kwamba unaweza kuhimili malipo ya *benefits* ambazo zinatajwa katika mfuko. Lakini mara tu tunapofanya mabadiliko haya imeonekana kwamba mfuko utakuwa na tatizo la fedha kiuwezo.

Kwa hiyo, Serikali itatoa *contribution* kuuwezesha mfuko kuweza kuwa endelevu. Kwa mantiki hiyo, nisingependa kukubaliana na wazo la kusema kwamba *rate* ije iwe *revised upwards* kwa sababu kumetokea na matatizo ya *sustanability.* Matatizo ya *sustanability* yakitokea *guaranter* iwe ni wajibu wake kulipa ile sehemu ambayo itakuwa imepungua na *guarantor* katika hili namwona mimi ni Serikali. Kwa sababu

*rate* ya *20%* ni kubwa kuanza kuizungumzia kuipandisha ni kuwatia wafanyakazi katika lindi la kupungukiwa na *take home* yao katika misingi ambayo nadhani sio ya lazima.

*Section 15* (2) inazungumzia *members* wengine *other than* wale ambao sasa hivi wako kwenye ajira. Sasa unapoanza kuzungumzia *members* wengine na wakati mfuko umeuita *Local Authorities* maana yake sasa una-*transend* kwenye maeneo mengine ya mashirika mengine. Kutaanza *competition* na *over lapping* na kunyang'anyana wale wanachama. Mimi nadhani tuendelee tu *as a specialized fund* kwa ajili ya *Local Authorities employees.* Lakini wakati huo huo napenda nitumie fursa hii kwamba kwa hao wengine ambao tunataka tuwaongeze, basi ni nafasi nzuri sana hapa ya kuwaongeza Madiwani ili na wao wawe *members. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema ingekuwa vizuri kama tungekuwa tunazungumzia mambo haya kwa ujumla wa kitaifa kwa sababu sasa nataka kuligusa suala linalohusu Sera kinchi. Nalo ni la *retirement age.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko unapendekeza kwamba *voluntary retirement age* iwe miaka 55 na *mandatory* miaka 60. Wakati *life expectancce* ya Mtanzania sasa kutokana na matatizo ya *AIDS* na kadhalika ni miaka 43. Je, mwanachama atafika hiyo miaka 55 na 60 ili aweze ku-*enjoy benefits* za mfuko huu? Tuwe *relialistic,* siyo wengi watakaofika. Kwa hiyo, ndio maana nilisema sasa tukiliweka kwenye hili sijui kama rafiki yangu Bwana Pinda atalikubali au vipi. Lakini ndiyo hali halisi, *retirement age* naomba iwe hivi: *voluntary 50* na *compasory 55,* ili angalau wafanyakazi hawa waweze ku-*benefit* matunda ya huu mfuko hasa kwenye *pension.* Kwa sababu mtu halipwi pensheni mpaka ame-*retire.*

*Section 48(c)* inazungumzia kwamba pesa zitakazokusanywa zitatumika kwa *administration.* Lakini sijaona kama *administrative expenses* za mfuko huu zina kiwango maalum. Yaani *sky is the limit?* Ni vizuri tukawekwa *limit* kwamba tukitengeneza bajeti kila mwaka ijulikane mfuko huu kwa upande wa *administration* utatumia kiasi gani? Iwe *in relation to the income* ambayo mfuko utakuwa una-*generate. Income* maana yake siyo *contribution*, *income* ukitaka kupima utendaji wa wafanyakazi, ni vizuri *income* iwe ni matokeo ya *investments* nzuri zinazofanywa na waendeshaji wa mfuko.

*Section 49* kuhusu *investiments* imezungumzwa na karibu kila msemaji aliyenitangulia na mimi naafikiana na hilo kwamba haiwezekani *(it is in-practical).* Kwanza turudie kwenye *section* inayozungumzia kumpata *DG* wa mfuko huu na tumempa kazi gani. *DG* wa mfuko huu kwa kifupi amepewa kazi pamoja na nyingine kwenye *section 2(a) carrying out and over seeing the carrying out of the day to day management of the business operations and affairs of the fund.*

Sasa *business operations* ni pamoja na ku-*invest funds* ambazo zinakuja kwenye *fund* kwenye mfuko. Kama tunataka asimamiwe tuhakikishe basi kwamba kunatengenezwa *investiment policy,* ambayo kama ni lazima aione Waziri, aipitishe iwe ndiyo mwongozo. Lakini kusema kila tunapotaka ku-*invest* twende kwa Waziri tumpelekee haiwezekani, *it will not work.* Isitoshe ukiwa na mapesa mengi kama mifuko

hii ndiyo inakuwa wanayo maeneo ya ku-*invest* ni mengi ikiwa ni pamoja na maeneo ya kununua hisa kwenye soko la mitaji *capital market* na *stock echange. Transactions* za kule ni *transparent.*

Hata Waziri au mtu mwingine yeyote hawezi kukataa kama bei ya *stock* ya *TBL* (Kiwanda cha Bia) katika *stock exchange* ni nzuri, sasa hakuna haja tena ya Waziri kuiafiki bei ya soko. Tuwape nafasi tumewapa kazi, tuwape miongozo, wafanye, Waziri awe ni mtu wa kusimamia *policies* tu siyo mtendaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipindi cha mpito, tunabadilisha mfuko huu tukiwa na wafanyakazi ambao wamezoea, *Provident Fund.* Wanajua wakimaliza kazi watapata pesa zao mara moja. Sasa unamwambia mfanyakazi ukimaliza pesa zako hatukupi usubiri tutakuwa tukikulipa kidogo kidogo. Kuna suala la mazoea, kumeneji mazoea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutengeneze kipindi cha mpito tutoe *option* wale watakaokuwa wanadhani bado tuko kwenye *Provident Fund* tuwape *benefit* hiyo. Angalau kwa kipindi kifupi labda kati ya mwaka mmoja na miaka miwili na tuwaambie tunawatayarisha kwamba baada ya kipindi hiki ukiacha kazi sasa utaratibu ni *pension fund* na mambo mengine siyo yale ya kulipana kwa mkupuo kwa mara moja. *Let us manage a transion period.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya kwa uchache ndiyo mapendekezo yangu ya haraka haraka, lakini nataka nimalizie kwa kusisitiza suala la kuwa na sera ya Hifadhi ya Jamii na kuwa na Sheria mama ya Hifadhi ya Jamii kinchi. Vinginevyo, mifuko hii itaendelea kunyang'anyana wateja wale wale na wanachama wale wale basi itakuwa ni vurugu.

Kabla sijakaa nataka vile vile niungane na wenzangu waliozungumzia kuhusu muundo wa Bodi. Bodi ya Mfuko kama huu inahitaji watendaji wenye uzoefu wa kibiashara na wenye muda wa kufanya hizo kazi. *Principal Secretary*, *Attonery General* hawa ni watu wana kazi zao nyingine nzito. Tutaitisha mkutano hauna *quoram* kwa sababu hawapatikani. Tubadilishe, kwani watu wapo! Sasa utang'ang'ania tu hawa *Principal Secretaries* wana kazi zao tayari. Tutafute watu wenye *qualifications* ili mradi tuseme tu ili tukuweke kwenye Bodi hii uwe na *qualificatins* hizi uwe na uzoefu huu, basi! Tuwape watu wafanye kazi! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kaboyonga kwa mchango wako mzuri.

Waheshimiwa Wabunge, kabla sijasitisha kikao chetu cha leo asubuhi, ninaomba nisome tangazo. Taarifa ya Kikao kitakachofanyika siku ya Jumamosi, yaani tarehe 4 Novemba 2006. Tangazo hili limeletwa na Kaimu Katibu wa Kamati ya Wabunge wa Chama Cha Mapinduzi. Anasema anawaomba Waheshimiwa Wabunge wote wa Kamati

ya Wabunge wa CCM katika Kikao siku ya Jumamosi saa 4.00 asubuhi katika Ukumbi wa zamani ambao unaitwa Pius Msekwa. Kikao hicho ni muhimu kwa kila mjumbe kuhudhuria na anategemea kwamba Wabunge wote wa Chama Cha Mapinduzi watahudhuria kikao hicho siku hiyo ya kesho.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya tangazo hilo, tumekamilisha mjadala wa pamoja wa hoja iliyopo mbele yetu na sasa ili kuweza kumpa nafasi Mheshimiwa Waziri na timu yake waweze kupitia yale yote ambayo yamechangiwa na Waheshimiwa Wabunge. Kwa hiyo, ninasitisha Kikao cha Bunge sasa hivi ili hatua zote za kupitisha Muswada ziweze kufanyika tutakapokutana hapo saa 11 jioni. Kwa hiyo, sasa nasitisha kikao cha Bunge mpaka saa 11 jioni.

*(Saa 06.42 mchana Bunge liliahirishwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11:00 jioni Bunge lilirudia)*

*Mwenyekiti (Mhe. Jenista J. Mhagama)Alikalia Kiti*

**MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

*(Majadiliano yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Baada ya mjadala wa jumla sasa naomba nimkaribishe Mheshimiwa Waziri. Naona ataanza Mheshimiwa Naibu Waziri kutoa maelezo ya hoja mbalimbali ambazo zimechangiwa na Waheshimiwa Wabunge na baada ya hapo tutaendelea na hatua nyingine.

**NAIBU WAZIRI, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali yote kwanza niwashukuru sana wachangiaji wote ambao wamechangia Muswada huu. Kwa kweli mengi tulishayaingiza kwenye *amendment* yetu ambayo tuliitoa asubuhi ambayo walitoa Kamati ya Katiba na Sheria mapendekezo tulishayatolea maelezo na tumeya-*include* kwenye Muswada mzima. Machache ambayo tunataka kuyaingiza yako tayari na Mheshimiwa Waziri kuya-*elaborate* zaidi.

Mimi nichukue tu nafasi hii kuwashukuru wote waliochangia kwa njia moja au nyingine, kwa kweli ni mazuri na yalikuwa ni ya kuboresha Muswada huu. Kwa hayo, machache nawashukuru naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kutoa ufafanuzi katika maeneo ambayo yalikuwa yamechangiwa asubuhi hii. Lakini kabla sijafanya hivyo, naomba kwanza niwatambue wale wote ambao wametusaidia sana katika kuboresha Muswada wetu.

Kwa hiyo, kwanza ni Mheshimiwa Charles Keenja, ambaye aliwasilisha kwa niaba ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa -

Mbunge wa Karatu ambaye aliwasilisha maelezo hapo kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Philemon Ndesamburo - Mbunge wa Moshi Vijijini, Mheshimiwa William Shellukindo - Mbunge wa Bumbuli, Mheshimiwa Dr. Omari Mzeru Nibuka - Mbunge wa Morogoro Mjini, Mheshimiwa Ezekiel Maige - Mbunge wa Msalala, Mheshimiwa Lekule Laizer - Mbunge wa Longido na Mheshimiwa Siraju Juma Kaboyonga Mbunge wa Tabora Mjini. Hawa walichangia moja kwa moja hapa Bungeni. *(Makofi)*

Lakini tumepata vile vile michango kutoka kwa Wabunge kwa maandishi. Michango hiyo imetoka kwa Mheshimiwa Dr. Harrisson Mwakyembe Kyela, Mheshimiwa Dr. Guido Sigonda - Mbunge wa Songwe, Mheshimiwa Mwanawetu Zarafi - Viti Maalum Lindi, Mheshimiwa Victor Mwambalaswa kutoka Lupa na Mheshimiwa Fatma Mikidadi wa Viti Maalum. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuwatambua Waheshimiwa Wabunge waliotoa mchango huo, basi naomba nijaribu kutoa ufafanuzi kwa maeneo mbalimbali yaliyokuwa yametolewa hoja hapa leo asubuhi. Naomba nianze na yale yaliyojitokeza kupitia kwa Mheshimiwa Keenja. Kwanza Mheshimiwa Keenja, alitaka nafasi muhimu waliyonayo Madiwani katika Serikali za Mitaa, iwe ni sehemu ya utaratibu wa mafao haya ambayo sasa tunazungumzia chini ya Mfuko huu.

Kwa hiyo, maelezo kwa kifupi tunaweza tukasema tu kwamba ilimradi katika mapendekezo yaliyomo katika Muswada nafasi hiyo imetolewa kwa watu wengine ambao hawamo kabisa katika utumishi, hili hatukuona kwamba lina tatizo, lakini litawekwa katika Kanuni ili tuweze kuweka utaratibu mzuri zaidi wa namna ya kuwahusisha Madiwani hasa kwa sababu vipindi vyao ni vya miaka mitano ya uhakika kwa sababu ni watu wa kuchaguliwa. Lakini chanzo chao siyo lazima zikawa posho inaweza vile vile ikawa ni pamoja njia nyingine zinazowawezesha kuwa na fedha kwa ajili ya kuchangia. Lakini kimsingi linakubalika na tunafikiri tutaliweka katika utaratibu. *(Makofi)*

Yako mambo mengi ambayo yalielezwa na Mheshimiwa Dr. Slaa na mimi naomba kwa kweli niyapitie moja moja kwa uangalifu kama ifuatavyo:-

Kwanza, amesema Muswada huu haukuwa shirikishi kwa kiasi cha kutosha na hasa katika Mfumo wa sasa wa *public hearing*. Utaratibu ulivyo ni kwamba ukishawasilisha Muswada na ukishausambaza kwa wahusika Bunge kwa kawaida ndiyo linachukua jukumu la kutoa taarifa kwa wale ambao wanaonekana kwamba ni wadau muhimu katika kuboresha Muswada. Kwa hiyo, katika hali ya Muswada huu Ofisi ya Bunge, inasema ilitoa taarifa kwa makundi mbalimbali. Lakini inaonekana Muswada wenyewe haukuwa pengine na matatizo makubwa na hivyo hakuna aliyeweza kujitokeza kutaka kushiriki katika zoezi hili.

Pili, Mheshimiwa Slaa anasema Waziri alieleze Bunge hili ni wapi yatakuwa Makao Makuu ya Mfuko huu unaotungiwa sheria mpya na hakuishia hapo, akataka hasa ikiwezekana Makao Makuu yawe Dar es Salaam. Sina tatizo kabisa na kupeleka Makao Makuu huko Dar es Salaam ya Mfuko huu. Lakini kwa kweli katika azma yetu ya kujaribu kujenga Dodoma kama Makao Makuu, kidogo nilishangazwa na kauli hiyo kwa

sababu haiendani hasa na azma yetu ya kutaka kuimarisha Dodoma kama Makao Makuu ya nchi. Kuwepo kwa chombo hiki ni sehemu tu ya uimarishaji huo na ofisi yetu maadam iko hapa Dodoma tulidhani ni namna bora na mfano mzuri zaidi wa kuigwa na vyombo vingine.

Safari alizosema kwamba zinachangia, tunaloweza kusema ni kwamba katika mazingira tuliyonayo safari hizi ziko, lakini haziko za Dar es Salaam tu, inategemea na jukumu ambalo liko mbele yako. Wakati mwingine ni Arusha, wakati mwingine ni Dar es Salaam, lakini wakati mwingine. Inaweza ikawa sehemu nyingine yoyote kama Morogoro. Kwa hiyo, kwa kweli ni safari, lakini *functional* sio safari tu kwa sababu unaibuka tu kutaka kwenda eneo lile kwa kupenda kwako.

Kwa hiyo, tunaamini rai aliyoitoa kujaribu kudhibiti safari zipungue, hilo tutazingatia. Lakini mimi nimepata taabu kidogo kusema Makao Makuu yaende huko kwa sababu mfuko huu tofauti pengine na vyombo vingine. Ni mfuko ambao unatunza fedha za watumishi Dodoma kwa msingi tulioutumia ni katikati ya nchi kwa sehemu kubwa. Kwa hiyo, Halmashauri zinaweza zikafika hapa kwa urahisi zaidi, kuliko ukiamua kupeleka pembezoni ambako ni Dar es Salaam.

Jambo la tatu ambalo Mheshimiwa Dr. Slaa alitaka kujua ni kwamba kifungu cha 81 hakuna kipengele katika Muswada ambacho kinaelezea jinsi ya kutoa huduma utakavyoratibiwa. Hilo tunalikubali na tumesema tutalizingatia kwenye kanuni ili tuweze kuboresha ni namna gani tutahakikisha kwamba watumishi hawasumbuliwi ,kunakuwepo na huduma ambazo zinatolewa kwa ufanisi mkubwa.

Nne, anasema mtindo wa kutunga sheria kuwalazimisha watu kuwa wananchi wa mfuko anaona umepitwa na wakati na tungeiachia mifuko hii ikafanya kila mmoja kwa namna wanavyoona. Ni rai nzuri kwa maana ya ushindani. Lakini kwa mfumo ulivyo hivi sasa wa Hifadhi ya Jamii ndivyo tulivyo. Kwa hiyo, *LAPF* ilikuwa na kundi lake, *NSSF* ina kundi lake, Mfuko ule wa Serikali nao ni kundi la watumishi wa Serikali na huu ulikuwa ni mahususi kwa ajili ya kundi hili la watumishi wa Serikali za Mitaa.

Hata hivyo, kwa mujibu wa sera, lakini zaidi hasa katika mapendekezo yatakayoletwa Bungeni hivi karibuni kuhusiana na utungaji wa sheria inayotekeleza hiyo sera tunaamini jambo hili litajitokeza vizuri zaidi na linaweza pengine likapata maelekezo mahususi juu ya namna ya kuendesha jambo hili bila kuleta migongano katika utendaji wa vyombo hivi.

Sehemu ya tano rai yake ilikuwa ni kuhusu idadi ya wanawake akataka itajwe wazi katika kifungu kile cha 10 (1). Ushauri huo kwa kweli tumeuzingatia, hatuoni kwamba una tatizo.

Sehemu ya sita, anazungumzia kifungu 10 (2) juu ya mamlaka ya Waziri kuwa ni makubwa mno ya kufuta kipengele kilichoko kwenye jedwali. Jedwali analolizungumza ni lile linalounda Bodi ya Mfuko huu. Sasa tunachosema tu hapa ni kwamba katika utekelezaji wa jambo hili ziko *consultations* za kutosha zinazofanyika ndani ya ofisi

yenyewe ya Waziri kabla hawajafikia uamuzi wowote. Lakini kubwa tulililoliingiza sasa ambalo halikuwepo hapo mwanzoni ni kufanya mawasiliano na Bodi yenyewe kabla ya kufanya *changes* zozote. Kwa hiyo, tulidhani hili linatosheleza kabisa lakini bado tunajenga hali ya kuaminiana kwa kiasi kikubwa kabisa kati ya nafasi ya Bunge na nafasi ya Serikali.

Sehemu ya saba inazungumzia kifungu 41 mamlaka ya Rais kuamua mafao ya mtumishi aliyestaafishwa kwa manufaa ya umma. Mheshimiwa Dr. Slaa kidogo alikuwa na *reservations* katika eneo hili na hakuona kwamba pengine ni busara kufanya hivyo. Lakini kipengele hiki utakikuta karibu katika sheria zote za mifuko na sababu ipo, Rais kama kiongozi wa nchi, ndiye vilevile Mkuu kwa kweli wa Utumishi wa Umma wote hapa nchini na kwa maana hiyo, yako maeneo ambayo hayawezi kufanywa na mtu mwingine, kwa kuwa sisi kama Waziri, ndio tunashughulika na watumishi hawa kwa karibu sana.

Kwa hiyo, ziko *cases* ambazo unakuta mtumishi kafukuzwa kazi au kweli kastaafishwa kwa manufaa ya umma na kwa mujibu wa taratibu, hastahili kabisa kurejeshewa fedha yoyote, iwe ile ya kuchangia yeye mwenyewe au ile ambayo imetokana na mchango wa aina nyingine. Sasa katika mazingira haya, ubinadamu unatutaka mwingine tufikirie *case by case* na mtu ambaye anaweza akaifanya kazi hiyo vizuri tulidhani ni Rais. Kwa hiyo, akiombwa anaweza pengine akasaidia vizuri sana.

Pengine nitoe mfano halisi ambao bado unanisumbua ofisini kwangu pale. Ninaye Mkurugenzi ambaye alikuwa kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara Vijijini. Kwa bahati mbaya, huyu bwana asili yake ni mmakonde. Baba yake alikuja siku nyingi, babu ndiye alikuwa siku nyingi zaidi. Kwa hiyo, amezaliwa hapa, amekuwa hapa, amesoma hapa na akaajiriwa katika utumishi wa Umma. Alikuwa ni Mkurugenzi wetu, lakini ikagundulika dakika hizi za karibu kwamba yeye ni mmakonde wa Msumbiji na kwa hiyo, sio raia.

Kwa hiyo, sheria ilipochukua mkondo wake amefukuzwa na kwa hiyo, hakustahili kupata hata senti moja. Sasa unapopata *case* kama hii inahuzunisha ni ya kusikitisha na ni kesi aina hii ndio tunafikiria kwamba pengine ukimpelekea Rais angalau huyu mtu alipwe hicho alichokuwa anachangia, mtu mwingine sio rahisi kufikiria jambo kama hilo, ndio hasa *essence* ya kipengele hiki. *(Makofi)*

Sehemu ya saba, Mheshimiwa Slaa anasema kusubiri maamuzi ya Waziri kuhusiana na uwekezaji litafanya shirika lisiwe shindani, tumelikubali kabisa, wakati nawasirisha maelezo hapa, nilieleza nimeondoa kipengele E, bahati mbaya Mheshimiwa Slaa, alidhani nimesema A, lakini nilikuwa nazungumzia E, ambayo ndio inahusiana na uwekezaji. Tulishalitambua hilo na tukasema kwa kweli ni urasimu ambao sio wa lazima sana. Kwamba Waziri amepewa mamlaka makubwa isivyo lazima kifungu cha 10(2) au kuongeza viwango vya michango kifungu cha 24 na 26 na kwamba pengine ingekuwa vizuri mamlaka haya ikabakia kwenye Bodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu nimwombe Mheshimiwa Slaa katika hili kwamba sababu kubwa kwa kweli ambayo inatufanya tusite kufanya hivyo, ni kwa sababu tungalipenda Serikali ambayo ndio tunasimamia shughuli zote kwa ujumla, tuwe na uhakika jambo hili linapofanyika limefanyika kwa misingi gani, maana ni kweli kabisa Bodi inaweza ikaamua kuongeza leo michango kutoka asilimia 20 ya sasa wakaamua asilimia labda 30 au 40 na kwa sababu wamepewa mamlaka hayo basi linaweza likaonekana kwamba ni jambo liko ndani ya uwezo wao. Lakini hofu yetu ni kwamba kwa mambo mazito kama haya ni vizuri, Waziri mwenye dhamana angalau basi akapata misingi ya jinsi gani kulifikia maamuzi mazito kama haya kwa sababu mwisho wa safari watakaoathirika ni watumishi katika chombo hicho.

Naomba niseme kidogo kuhusiana na maeneo ambayo Mheshimiwa Ndesamburo alichangia katika kusaidia kuboresha Muswada huu. Alisema kifungu kiongozwe kuhusu Mfuko kutoa mikopo ya elimu kwa wanachama. Tumelitazama hili kimsingi tunalikubali na tumeona tutatengeneza kanuni ambazo zitazingatia jambo hili kwa kuwa yako mambo yaliyokwisha kuzingatia kwamba mikopo ya nyumba hatuoni kwa nini eneo hili liwe na kigugumizi kikubwa. Tutaangalia ni namna gani zitalipwa na kuweka utaratibu mzuri zaidi. *(Makofi)*

Kifungu cha 49 ambacho kinahusiana na uwekezaji kilisemwa vile vile na Mheshimiwa Ndesamburo, lakini kama nilivyosema kwa jibu nililompa Mheshimiwa Dr. Slaa, jibu ni lile lile, tumeshaondoa tunakubali hakuna haja ya kuingiza ukiritimba mkubwa katika masuala haya ya uwekezaji. Ingawa kulikuwa na rai nzito kidogo kwamba maeneo yale mazito uwekezaji ule mkubwa hilo linafaa. Lakini yako maeneo mengine ambayo unakuta kama alivyosema Mheshimiwa Dr. Slaa ni fedha ya kawaida hii ya Serikali ambayo tunaipata kutumia utaratibu wa kawaida, lakini sisi tumedhani wacha eneo lote libaki huru ili waweze kutimiza wajibu wao vizuri, sisi tutaangalia mambo ya msingi ambayo yatasimamiwa vizuri na ofisi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa William Ezekiel Shellukindo amesema sheria iwe kali kiasi kwamba Wakurugenzi ambao hawawasilishi michango wafungwe kabisa. Tumejitahidi katika Muswada tumeeleza pale kwamba huyu mtu atatozwa faini ya Shilingi laki tano ama kifungo cha miaka miwili. Sasa inawezekana Mheshimiwa Shellukindo alikuwa anaona laki tano wanao uwezo wa kuzilipa. Lakini tulidhani hata ukizilipa kwa jambo kama hili nayo inaweza vile vile ikawa ni fundisho kwa sababu tunaamini halitaishia hapo, bado tunaweza tukachukua hatua nyingine za kinidhamu kama zitakuwa zimesababisha uzembe ambao tunaona haukuwa *justified*. Lakini akishindwa ni kweli atakwenda miaka miwili. Lakini tuko radhi kwa siku zijazo pengine tunaweza tukalitazama vizuri zaidi kwa sababu ni eneo ambalo linataka kuangaliwa kwa uangalifu sana.

Taarifa za vitega uchumi zitolewa kwa wadau. Ushauri tumeuzingatia muda wa Wajumbe wa Bodi uongezwe ili wapate muda wa kuelewa vizuri shirika linavyoendeshwa na kuendesha mambo yake. Kwa utaratibu ulivyo, sasa hata katika mapendekezo ya Muswada huu sheria tumependekeza Mjumbe huyo aweze kufanya kazi kama *Board Member* kwa miaka mitatu. Lakini tukaweka kipengele cha kuweza kuteuliwa tena kutegemea *of course* na utendaji wake ulikuwa mzuri kiasi gani. Hili

tumeliweka makusudi. Vyombo hivi vinahitaji *continuously* kuwa *monitored.* Ukiwapa Bodi hawa *Members* miaka mitano wakati mwingine mambo pale yakiharibika inaweza ikawa shida kidogo kujua ufanye nini katika mazingira tuliyonayo. Kwa hiyo, imewekwa makusudi ili *checks and balances* atakayefanya vizuri ndiyo ambaye tutaondoka naye na kumpa nafasi ya kuendelea.

Mheshimiwa Dr. Mzeru Nibuka naye ameeleza mambo mengi, wadau washirikishwe katika maandalizi ya sheria kama hii, mazingira magumu kwa watumishi yaangaliwe namna gani yataweza kudhibitiwa, tatizo la kutopandishwa cheo, kupatiwa mikopo ya masomo, *reform* haikujali mafao ya Madiwani, Posho za Madiwani ziongezwe, utaratibu wa asilimia kumi za vijana na wanawake nao uzingatiwe. Yako mambo kweli yanaigusa *LAPF* kidogo katika Muswada huu, lakini mengine ni ya kwangu moja kwa moja.

Kwa hiyo, suala la kuwashirikisha wadau tumekubali, juhudi zilifanyika lakini inawezekana kwa mazingira ya sheria au Muswada wenyewe ulivyo pengine haikuwa attractive sana kwa walio wengi. Lakini mazingira magumu ya watumishi hilo tumelikubali, tutajaribu kulizingatia kwenye kanuni. Suala la kupandishwa vyeo nalo liko ndani ya uwezo wangu kama Waziri mwenye dhamana katika eneo hili, kwa hiyo, hilo linashughulikiwa na sisi.

Suala la kupatiwa mikopo nimeshalieleza. Suala la Madiwani ni kweli kabisa lakini kama nilivyosema tutawaangalia katika Mfumo huu tuliouweka ni namna gani tunaweza tukasaidia katika kuboresha mafao yao kidogo.

Mheshimiwa Ezekiel Maige alitupa hoja nzuri tu kwamba Serikali iangalie mfumo mzima wa hifadhi ya jamii nchini ili kuondoa uwezekano. Hili kama nilivyosema iko sheria inaandaliwa chini ya Wizara ya Kazi ambao ndio wamepewa jukumu la kutazama ni namna gani tunaweza tukasimamia Hifadhi ya Jamii kwa upana wake kitaifa. Kwa hiyo, tukishakamilisha zoezi hilo tutawasilisha Muswada huo hapa Bungeni. Ukokotoaji wa mafao uzingatie wastani wa mishahara kwa kipindi fulani badala ya kuzingatia mshahara wa mwisho.

Rai ni nzuri, lakini inataka kazi ifanyike kubwa kwa sababu usipokuwa mwangalifu unaweza ukakuta shirika linafilisika kwa kutumia vigezo ambavyo pengine havikuzingatiwa vizuri sana. Rai ni nzuri na tunamwelewa lakini kwa mfumo ulivyo sasa miezi 12 mshahara wako wa mwisho unapo-*retire* kwa mifumo iliyoko sasa ndiyo inayotumika kama kigezo ulikuwa na mshahara gani hiyo ndiyo inatumika kusaidia kutengeneza mafao yako. Lakini hoja yake siyo mbaya lakini nadhani inahitaji stadi kubwa kidogo ili tuweze kuwa na uhakika kwamba tunatenda haki kwa pande zote mbili.

Pia, Mheshimiwa Lekule Laizer alisema Mfuko uweke utaratibu ambao wadau watakuwa wanapata taarifa za matumizi ya shirika. Tumelizingatia tutajitahidi kuliweka vizuri kwenye kanuni ambazo baadaye *of course* zitaletwa Bungeni kwa utaratibu wa kawaida wa kuwekwa mezani. Lakini vile vile alitaka ukaguzi wa hesabu za mfuko ufanyike mwaka hadi mwaka bila kuchelewa. Hilo tumekubali na utazingatiwa katika taratibu zitakazoandaliwa kwa ajili ya jambo hili. Madiwani waingizwe kwenye utaratibu

wa *pension* ya Mfuko, kama nilivyosema tumeshalichukua tutaangalia namna ya kuwatengenezea utaratibu utakaotuwezesha kuingiza humo. Bodi ya wadhamini iwe ni Bodi yenye uwezo wa kubuni miradi. Hilo litazingatiwa sana katika uteuzi hasa kwa vile vikundi ambavyo havikuwa *stipulated* moja kwa moja chini ya sheria.

Lakini nataka niwahakikishie kidogo kwa kweli, ukishazungumza Katibu Mkuu wa Fedha yumo, wa TAMISEMI yumo, *Attorney General* pale yupo, mwenyekiti wa *ALART* unaona kwa sehemu kubwa suala la uwezo wa kufikiri na kujaribu kubuni miradi au uwekezaji katika maeneo ambayo yanaweza kuleta manufaa ni *impliedly* kwa kweli katika namna ambavyo watumishi wenyewe wamepangwa. Lakini bado tunadhani ni jambo ambalo tunadhani ni jambo ambalo linaweza likatazamwa likaboreshwa zaidi.

Suala kwamba sheria haijaweka utaratibu ambapo endapo mdau atasumbuliwa katika kutoa mafao yake achukue hatua gani, tumelipokea. Hata sisi ni kero kwa sababu Wizara ndio inasumbuka zaidi mwishowe kwa sababu ya mapungufu ambayo yanatokana na tatizo hili la watu kucheleweshewa mafao yao. Kwa hiyo, tutalizingatia katika upangaji wa kanuni nzuri zitakazowabana kuhakikisha kwamba hilo jambo linadhibitiwa kwa kiasi kikubwa.

Lakini vile vile tulipata rai nzuri kwamba posho ya Madiwani iongezeke kufikia angalau 100,000 ili waweze kuchangia kwenye mfuko. Naomba niseme tu kwa kifupi kwamba bado tunaendelea sana kuishukuru Kamati ya Lubeleje, walimaliza kazi yao vizuri. Yako mapendekezo mazuri sana kuhusiana na Madiwani. Lakini kwa mzigo ulivyo mkubwa, tulidhani Halmashauri zenyewe haziwezi, tumelazimika sasa kuiomba Serikali ijaribu kufanya maamuzi juu ya jambo hili. Kwa hiyo, tumeandaa waraka wa Baraza, umekwenda *Cabinet Secretariat*, umekwenda kwenye *IMTC* na sasa unakamilishwa ili uende kwenye Baraza tuweze kupata mwongozo na maelekezo ya Rais na Baraza lake. Tunaamini kwa kiasi kikubwa yatakuwa *accommodated*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Siraju Kaboyonga, alikuwa na mchango mzuri tu. Kwa hiyo, kipengele cha *The Board may appoint other officers* aliuliza hawa ni wa kina nani? Sisi tumelikubali, tutajitahidi kuliweka vizuri ili tuweze kutenganisha watumishi wa menejimenti, watumishi wa Bodi ili iweze kuwa *clearly* zaidi. Hivyo hilo hatukuwa na matatizo nalo. Kiwango cha kuchangia ni asilimia 20, kwa ujumla imefikiwa kitaalamu. Alikuwa anatuhoji anasema *I hope* mmefikia kitaalamu, matatizo ya *sustainability* yakitoeka, basi mjue atakayebeba mzingo ni yule mdhamini ambaye *in this case* ni Serikali kupitia Wizara ya Fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kumhakikishia kabisa Mheshimiwa Kaboyonga, kwamba, tuliteua *consultant* ambaye ndio alifanya *study* hiyo kwa kina akatufikisha hapo unapoona tumefika na tukachukua sasa tuka-*adopt* mapendekezo yake ndiyo tukayatengenezea utaratibu wa kutengeneza sheria ambayo sasa Muswada wake ndio umefikishwa mbele yenu leo.

Kwa hiyo, hilo lilizingatiwa na kimsingi bado tunadhani mambo yakiharibika, kwa vile Serikali ni mdhamini, ndiye aliyetuwekea dhamana, kwa kutegemea na tatizo

limeibuka namna gani, bado tunadhani Serikali itakuwa sikivu kwa jambo ambalo linaweza likapelekea kuathiri watumishi katika mafao yao. Lakini na sisi kama wasimamizi wa chombo hiki tutajitahidi kusimamia karibu kuhakikisha hayo hayatokei.

Suala la kuongeza wanachama litaongeza washindani, hivyo ni vyema kulenga watumishi wa Serikali za Mitaa na sheria zifikirie kuwaingiza Madiwani hilo tumelipokea tumesema tutalizingatia kwa kiasi kikubwa, ingawa kifungu cha 24 kifungu kidogo kile cha tatu kimewekwa pale kujaribu kutoa hiyo tahadhari, *precisely* unavyolisema na sisi tunajaribu kulitazama kwa njia hiyo hiyo. Umri wa kustaafu miaka 55 mpaka 60 ndivyo ilivyo sasa, sasa iko rai kwamba tushuke 50 mpaka 55.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili ni la kisera kama mnavyojua sera ya sasa ndivyo inaweka hivyo, kwa hiyo karibu katika utumishi wetu wote wa umma hivyo ndivyo ilivyo na waliamua hivyo wakati ule ilionekana pengine tatizo la UKIMWI ambalo sasa hivi ni kubwa, halikuwa pengine na eneo kubwa la uathiri wa miaka ya kuishi katika utumishi wa Umma. Lakini inahitaji nayo ifanyiwe *thoroughly study* ili tuweze kuwa na uhakika chochote kitakachoamriwa kwamba hakitaturudisha katika *sustainability* ya mfuko wenyewe.

Suala la bajeti, ni vyema shughuli za kiutawala zitumie fedha zinazotokana na uwekezaji na sio michango, tumelikubali, lakini tunachosema tu ni kwamba kwa sera ilivyo sasa mifuko yote bahati mbaya au nzuri fedha yote pale inahesabika hivyo. Lakini nadhani rai aliyoitoa tumesema tutai-*adopt* kwenye kanuni ile ya kuwa na kiwango mahususi cha kiasi gani unataka tutumie kwa ajili ya uendeshaji wa shirika ili tubakize kiwango cha kutosha kwenye shughuli hasa za maendeleo ya mfuko huo. Kwa hiyo, nadhani hili ni jambo jema na tutaliangalia.

Serikali ifikirie kuwapo kwa sera ya hifadhi ya jamii na kuwa sheria mama ya mfuko, sera ipo kwa sasa, lakini kinachokosekana ni sheria na ndiyo hiyo nimesema kwa sasa iko chini ya Wizara ya Kazi, wanakamilisha zoezi hilo. Katika kuteua Bodi watendaji wenye uzoefu wa kibiashara ndio tujaribu kuwazingatia zaidi na sisi tumesema tutajitahidi ingawa kwa mfumo ulivyo utaona tumepata taabu kidogo kwa sababu tumeshaweka makundi hivi ya Kiserikali ambayo nawaona moja kwa moja *assumption* iliyopo kwamba Katibu Mkuu Fedha, Katibu Mkuu wa TAMISEMI na *Attorney General,* kwa hiyo tutakuwa na mchango mkubwa katika eneo hilo kwa uzoefu na uwelewa wa mambo ya Serikali.

Lakini kuna kipengele kile cha mwisho ambacho kinaturuhusu kujaribu kutazama sasa *sectors* nyingine za binafsi tuone tutafanya nini, litazingatiwa kwa kiasi kikubwa sana, tuone kama angalau tunaweza tukapata *input* ya mtu mmoja, wawili ili tuweze kuboresha jambo hilo zuri vizuri na labda kwa haya niseme tu *in conclusion* kwa haya iliyojitokeza Bunge moja kwa moja kuhusiana na kipengele hiki, kwa kweli tatizo tunalolipata pale tulikuwa tunajaribu kuweka uwiano kati ya waajiri, mtumishi lakini na Serikali kwa upande mwingine kwa maana ya *roll* yake kama wasimamizi wa chombo hiki.

Ndio maana utaona kwa upande wa wawafanyakazi, tunao watatu, waajiri pale tumekuwa tumeweka wawili kwa maana ya *ALART* makundi yale mawili, lakini Serikali kama mdhamini tukaweka watatu, eneo lile la mwisho la jumla ndio tukaweka wawili. Kwa hiyo, unapata kumi lakini kwa uwiano ambao tulidhani *tripartite situation* inaweza pengine ikatusaidia zaidi kuimarisha jambo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, haya ni baadhi ya maelezo ambayo tumeyatoa kwa wale waliotusaidia kwa kutoa mchango moja kwa moja hapa. Naomba nigusie kidogo hoja za maandishi kwa sababu bado naona nina muda.

Mheshimiwa Mikidadi, Fatuma Makidadi anasema, wastaafu kulipwa pesheni ambayo yeye anaona ingefaa iwe inalipwa kila mwezi badala ya miezi mitatu mitatu, sasa mimi sina hakika miezi mitatu mitatu imetoka wapi, lakini sisi Serikali Kuu ni miezi sita, inawezekana *PPF* na *NSSF* pengine mmojawapo anatumia hivyo, lakini kwa mapendekezo yaliyomo kwenye Muswada, *exactly* anachokisema Mama Fatuma ndicho tumeshauri, ndicho tumependekeza, mafao *under* mfuko huu yatakuwa ni ya kila mwezi na siyo ile ya miezi mitatu wala sita. Kwa hiyo, hilo tumelizingatia vizuri.

Amejaribu vilevile kusema, basi Bodi zizingatie jinsia na kama nilivyosema tumejitahidi katika mlolongo ule wa *Members* wa *Board*, kujaribu kuhakikisha angalau tunatamka kwamba mama mmoja atakuwepo hapa na sehemu nyingine kama tulikuwa tumejaribu kueleza katika sheria na ile *schedule*. Lakini Mama Fatuma bado alisema mtakapokuwa mnafikiria jinsia hiyo, basi mniangalie na mimi maana nami natafuta kweli, tutaliangalia Bi. Mkubwa wakati ukifika. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwanawetu Said Zarafi alisema kwamba Wizara iweke wazi Sheria kuhusu muda wa mstaafu aliyeachishwa itamchukua muda gani hadi kupata mafao yake. Hilo tutaliweka katika Kanuni na kwa ujumla tunakubali kabisa lazima tujaribu kudhibiti hali yoyote inayoweza kumsababishia mtumishi adha bila sababu za msingi.

Vile kulikuwa na hoja kutoka kwake kwamba *pension* ya wadau huwekezwa lakini walengwa wanafahamu ni jinsi gani watafaidika na vitega uchumi hivyo, alikuwa anahoji kwa kweli anatushauri kwamba tuwe na utaratibu utakaowawezesha ni namna gani watafaidika na tumekubaliana na wenzetu wa *LAPF* kwamba kwenye Kanuni zinazotungwa kuhusiana na uwekezaji. Hilo tutajitahidi kuliweka bayana zaidi na tutawaomba tukishaweka hapa mezani mjaribu kuona ni namna gani tume – *accommodate* jambo hili.

Ni jinsi gani walengwa wameshirikishwa katika marekebisho ya Sheria kama nilivyoeleza jitihada zilifanywa na Ofisi ya Bunge lakini inawezekana kwa sababu fulani fulani pengine haikuwa *attractive* sana haiku-*draw attention* kubwa sana.

Sheria ianishe wazi kwa watumishi wanaobadilisha mwajiri mfano mtumishi wa Serikali Kuu kuingia Serikali za Mitaa kusiwe na usumbufu. Bahati nzuri kwa mfuko huu hilo limezingatiwa kwa sababu michango inafanana tano kwa kumi na tano, tano kwa kumi na tano mtu akitoka Serikali Kuu anaweza kwenda Serikali za Mitaa bila matatizo

makubwa kwa sababu hakuna *change* ya michango ambayo inaweza ikaleta tatizo kidogo.

Kwa hiyo, kwa haya nadhani kwa Mheshimiwa Siraju Juma Kaboyonga na Mheshimiwa Mama Fatma Abdallah Mikidadi tutakuwa tumejaribu kueleza kwa njia hiyo.

Lakini kwa Mheshimiwa Dr. Harrison George Mwakyembe uwekezaji wa fedha za mfuko uwe wa ushirikishaji wa wadau ili kuleta uwajibikaji na kujenga imani kwa wanachama. Hoja yake hasa ni ushirikishwaji wa wafanyakazi wenyewe kupitia mfumo mahususi juu ya utaratibu wa uwekezaji ili waweze kuona kwamba chombo hiki kweli kinafanya kazi kwa manufaa yao. Ni rai nzuri na tutaona namna tutakavyoliweka katika Kanuni Ushirikishwaji wa Wafanyakazi ambao ni walengwa wakubwa katika maamuzi haya ambayo ni ya msingi sana.

Lakini pili alikuwa na rai nyingine ya Ushirikishaji wa Wadau uwe kwa kiwango fulani ambacho kitamkwe kwa Sheria. Nadhani ni katika kuimarisha hoja ile ile, tutaangalia wakati tunatengeneza Kanuni kama tunaweza tukaangalia ni kiasi gani cha uwakilishi wakati wa kupitisha mambo mazito kama hayo hasa kwenye vile vikao vya wafanyakazi wote ambapo ndio bajeti zinatazamwa na mpango mzima wa chombo kama hiki tungeweza tukajihakikishia kwamba tunashirikisha ama wote au sehemu kubwa katika kujua kinachoendelea ni nini.

Mheshimiwa Dr. Guido Gorogolio Sigonda alisema kwamba Madiwani na Watendaji wa Kata, Ma-*VEO* pia waingizwe katika mpango wa *Pension* wa Serikali za Mitaa. Kama nilivyosema, chini ya mfumo wa Mfuko huu hata mtu wa kawaida anaruhusiwa. Kwa hiyo, tumekubaliana kimsingi kwamba tutaangalia hawa wote walio chini ya Serikali tuone ni namna gani tunaweza kwa kutumia utaratibu uliopo kuwaingiza katika mfumo huu. Kwa watendaji au Ma-*VEO* au Ma-*WEO* ni rahisi zaidi kwa sababu ni watumishi ambao wanalipwa kutoka Serikali Kuu. Kwa hiyo, ni suala tu la kuwaingiza katika utaratibu ili na wao waweze kunufaika mwisho wa safari.

Lakini vile vile ameeleza kukosekana kwa uhakika wa ajira za Watendaji Kata na Vijiji wahakikishiwe uhalali wa ajira. Mimi nafikiri kwa upande wa Serikali Kuu tumejitahidi Watendaji wote wa Kata sasa hivi ni Waajiriwa wa uhakika na wanalipwa na Serikali na Ma-*VEO* nao kwa uamuzi na *support* tuliyoipata hapa kwenu Bungeni nao sasa ni Waajiriwa na wanalipwa na Serikali Kuu. Kwa hiyo, tuna hakika kwa maana ya ajira yao hili nalo limekuwa *taken aboard*.

Watendaji Kata na Vijiji kutothibitishwa na Ofisi za Wakurugenzi wa Wilaya wanapohitaji kukopa Benki au Taasisi nyingine za fedha. Hili ni la kiutendaji, kwa hiyo mimi nimekubali kwamba tutajaribu kuliangalia na Katibu Mkuu kwa sababu kimsingi halina tatizo, fedha ile inalipwa kutoka Serikalini, ni rahisi kabisa kumwezesha mtu kukopa na sisi tukahakikisha amekatwa fedha zake kupeleka kwenye chombo alichokopa. Serikali kuwalipa angalau posho Wenyeviti wa Vijiji na Watendaji wa Vitongoji ili

kuwaongezea miradi na kuwaongezea ari ya kufanya kazi na kuondoa kuingilia mapato kwa kujilipa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili lina ugumu wake, lakini naomba nilieleze tu kwa urahisi kidogo, tumekwishaelekeza Halmashauri na ninaomba nilirudie nimeshaeleza hili jambo mara mbili au tatu hapa Bungeni kuzitaka Halmashauri kutokana na fedha hii ya ruzuku ambayo sasa inarejeshwa kwao badala ya Vijiji kukusanywa sasa inarejeshwa kwao na Serikali Kuu waendeleze ule utaratibu waliokuwa nao wa asilimia 20 sehemu ya fedha hiyo kwa ajili ya maendeleo ya pale Kijijini na pesa inayobaki kidogo kwa asilimia ileile ziwaendee Wenyeviti hawa wa Vitongoji pamoja na Vijiji.

Mimi nimezunguka katika Halmashauri nyingine na ninazipongeza sana Halmashauri ambazo tayari wamekwishaanza kufanya kazi hiyo, wamejitengea asilimia 20 kutokana na ruzuku na katika Halmashauri moja nilikuta wastani ni kama Shilingi laki tatu kwa kila Kijiji na kwa kila mwezi. Kwa hiyo, ni fedha ya kutosha ambayo ingeweza kabisa ikakidhi tatizo hili, lakini kama hapana budi, basi tutaliongezea nguvu ili liweze kufanyika kwa namna ambayo ni nzuri zaidi.

Naomba niseme kidogo kuhusu mchango wa Mheshimiwa Victor Kilasile Mwambalaswa Mfuko ufanye majadiliano na kuungana na mifuko mingine iliyopo ili mifuko yote iombe Serikali kuunda chombo cha kusimamia mifuko. Nimesema hilo linakuja, Waziri wa Kazi katika muda sio mrefu naamini kwa sababu wapo mahali pazuri wataleta jambo hili hapa kwa ajili uamuzi wa Bunge.

Kuhusu kwmaba Mfuko uwekeze katika biashara ambazo zinalenga madhumuni ya kuundwa kwake na sio vinginevyo. Hili nalo tumelikubali, litazingatiwa sana kwenye Kanuni tutakazoziweka, lakini kama nilivyosema, Waziri tumeona tuachie Bodi kwa sababu ina utaalamu wa kutosha waamue uwekezaji utafanyikaje bila kuwaingilia sana isipokuwa pale tu itakapobainika kwamba kuna tatizo la msingi na tukalazimika kuingilia kati.

Mfuko kufanya utafiti na kutambua Asasi au Chombo cha Fedha mtandao mkubwa hapa nchini ili kiweze kusaidia katika kuwasaidia watumishi, nao ni ushauri mzuri utaangaliwa kwa sababu tunavyo vyombo kama *NMB* wana mtandao mkubwa, *CRDB* katika baadhi ya maeneo wanaweza kupatikana vilevile.

Kwa hiyo, nadhani kuna uwezekano wa kuzungumza nao, tunaweza tukaona mikopo hiyo mingine kupitia mabenki inavyoweza kufanyika na sisi tukawa kazi yetu ni kuwarejeshea wale waliokopwa.

Mheshimiwa Dr. Omari Mzeru Nibuka ameeleza kwamba Muswada huu ni muhimu sana kwa wafanyakazi wa Serikali za Mitaa, lakini wameshirikishwa kiasi gani nimekwishaeleza. Lakini kwa maana ya mfuko wenyewe huu ushirikishwaji ulikuwepo wa kutosha kupitia *TALGU* walishirikishwa, *ALAT* wenyewe wameshirikishwa lakini tuliomba hata msaada wa mawazo kutoka kwenye Vyombo vya Hifadhi ya Jamii ili tusije

tukafanya kitu ambacho hakiendani na matarajio na matakwa ya wananchi. Lakini vilevile Serikali tumekuwa *very close* na jambo hili.

Kwa hiyo, tuna hakika michango iliyopatikana pale ni ya kusaidia kuboresha chombo hiki vizuri zaidi.

Elimu kuhusu utaratibu huu wa *pension*, hilo tunalikubali na ni kazi ambayo itabidi ifanyike ili wananchi na watumishi *in particular* waweze kufahamu chombo chao sasa kimeanza, manufaa yake ni nini, mafao yenyewe hasa yatahusisha maeneo yapi ili kama walivyosema Waheshimiwa Wabunge wengine wangeweza hata ku-*opt* kuingia katika baadhi ya mafao na mengine wakasema hayahitajiki sana.

Kwa hiyo, niliona nimalizie kwa hili kwa sababu nilikuwa nimeshaligusia, lakini baadaye nikagundua kwamba hatukuwa tumeliweka vizuri sana.

Kwa hiyo, kwa hayo machache, naomba kusema kwamba tumejitahidi kutoa maelezo kwa kadri inavyowezekana, ni matarajio yangu sasa kwamba tutamalizana vizuri.

Nawashukuru sana kwa kazi nzuri mliyotusaidia. *(Makofi)*

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA - MWENYEKITI:** Samahani Mheshimiwa Waziri tunaomba utoe hoja.

**WAZIRI WA NCHI, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani. Naomba kutoa hoja.

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Pili)*

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA - MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imetolewa na imeungwa mkono.

## KAMATI YA BUNGE ZIMA

### Muswada wa Sheria ya Mfuko wa Pensheni wa Serikali za Mitaa wa Mwaka 2006
### *(The Local Authorities Pension Fund Bill, 2006)*

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA - MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, sasa tunaingia katika hatua inayofuata ambayo inahusu upitishaji wa Muswada uliopo mbele yetu.

Katika hatua hii, ninaomba tukifuata Kanuni Namba 72 inaturuhusu kupitisha Muswada huu kwa vifungu. Kwa hiyo, nitamwomba Katibu atuongoze katika hatua hii.

Kifungu cha 1

*(Kifungu Kilichotajwa hapo juu Kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima Bila Mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 2
Kifungu cha 3

*(Vifungu Vilivyotajwa hapo vilipitisnwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Mabadiliko yake)*

Kifungu cha 4
Kifungu cha 5
Kifungu cha 6
Kifungu cha 7
Kifungu cha 8

*(Vifungu Vilivyotajwa hapo Vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima Bila Mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 9

*(Kifungu Kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima Bila Mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 10

*(Kifungu Kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima Pamoja na Ma badiliko yake)*

Kifungu cha 11
Kifungu cha 12

*(Vifungu Vilichotajwa hapo juu Vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila Mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 13

*(Kifungu Kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima Pamoja na Mabadiliko yake)*

Kifungu cha 14

*(Vifungu Kilichotajwa hapo juu Kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila Mabadiliko yoyote)*

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kifungu cha 10 (2) mimi nina neno hapo lakini kabla ya kusema hivyo ninaomba nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri sana na kwa mabadiliko mengi ambayo ameyapokea kama alivyoeleza katika majibu.

Katika Kifungu cha 10 ninaomba tu anihakikishie katika hii sehemu ya pili, kwanza nilipeleka *Schedule of Amendment* na yeye pia amekuja na *Schedule of Amendment* yake, sijaona *Schedule of Amendment* yangu ambayo niliiwasilisha kwa Mujibu wa Ibara ya 70(4).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa iko kwenye ofisi yako, mimi nitaendelea tu na hoja yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi hoja yangu ilikuwa kwamba katika kifungu hiki kinazungumzia kifungu cha pili kwamba Waziri ana uwezo kwa kuchapa kwenye gazeti kubadilisha *composition* yote kama ilivyoonyeshwa katika *schedule* ya kwanza na Waziri siyo tu atapunguza mmoja au wawili au watatu lakini anaweza kufuta yote. Sasa ameeleza katika *schedule* aliyoleta kwamba ni *in consultation* na *Board* lakini mimi nikaona hapa bado kuna tatizo kwa sababu kama Bunge limetengeneza Board kwa mfumo fulani na Waziri anapata bado mamlaka ya kufuta yote nikadhani kuna tatizo.

Sasa kwa kuwa sijapata maelezo kama *schedule* niliyoleta imepokelewa au vipi na kwa bahati mbaya sijajibiwa kwa maandishi, naomba maelekezo kwanza ya ofisi yako ili niweze kuendelea kama *schedule* hiyo inaendelea au vipi kwa sababu Kifungu cha 70 kinataka kwamba *schedule* ikiwasilishwa na Mbunge iunganishwe pamoja na *Order Paper* ya siku. Sasa hiyo naona haikufanyika, labda ni kwa bahati mbaya au sijui, lakini ili nisiendelee, basi naomba nipate maelekezo ili niweze kuendelea kutoa hoja yangu.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA - MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dr. Wilbrod P. Slaa kabla sijampa nafasi Mheshimiwa Waziri aweze kutoa maelezo ambayo ameyatumia Mheshimiwa Dr. Wilbroad P. Slaa anatumia kifungu namba 70(4) kujenga hoja ambayo anaiwasilisha mbele yetu, yeye anatumia kifungu kile namba 70 (4) lakini ninaomba asome pamoja na Kanuni Na. 47 yenye kifungu a, b, c, kifungu cha 2, 3 na 4. Wakati akisoma hayo basi namwomba Mheshimiwa Waziri kwanza aendelee na maelezo yake.

**WAZIRI WA NCHI, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu labda niseme pengine ilikuwa ni bahati mbaya kwamba ilikuwa *skipped* lakini aliwasilisha kweli pendekezo lake, lakini nadhani wataalamu wangu katika kusambaza ile orodha, *schedule* yake haikuwa imezingatiwa na inawezekana ni kwa kutokujua tu. Kwa hiyo, sasa baada ya maelezo hayo, basi unaweza ukatoa maelekezo ili niweze kujibu sasa ambayo alikuwa anataka tujibu.

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri na ninaomba radhi na mimi kwamba pia hoja haiko mikononi mwa Wabunge kwa hilo lililotokea. Sasa sijui nitalisoma lilivyo! Lakini kwa kuwa Wabunge hawatakuwa wameliona sijui kama linaweza likafanya kazi. Lakini hoja inasema hili …

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA - MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dr. Wilbrod P. Slaa naomba utulie kidogo.

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo!

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA - MWENYEKITI:** Kanuni Na. 47 (3) inasema kwamba kila badiliko litakalopendekezwa sharti liwiane na hoja iliyokusudiwa kufanyiwa badiliko na sharti badiliko hilo liungwe mkono na lisiingize jambo lolote ambalo kwa maoni ya Spika laweza tu kuwasilishwa kwa hoja maalum baada ya kutolewa taarifa.

Kwa hali hiyo, kwa kuwa Waheshimiwa Wabunge hawana karatasi ambayo inaonyesha *amendment* yako na kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amekubali kwamba yeye anayo na itaingizwa katika kufanyiwa utaratibu, basi mimi naomba tumwachie Mheshimiwa Waziri kusudi aweze kuyafanyia maunganisho na anaweza kuitolea maelezo katika kipindi cha sasa.

**WAZIRI WA NCHI, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na eneo hili ambalo Mheshimiwa Wilbrod P. Slaa anaulizia kifungu hicho ni kifungu kinachompa Waziri uwezo wa kuweza kurekebisha *schedule* ambayo ndiyo imeweka mfumo wa Wajumbe wa Bodi katika mfuko huu tunaopendekeza kupitia Muswada huu.

Nilieleza wakati natoa maelezo hapa kwamba ni kweli hapo mwanzoni hatukuwa tumefikiria kwamba kuna ulazima wa *consultations*, lakini baada ya kulitazama tukarekebisha na tukaweka kwenye *Schedule of Amendment* tuliyoigawa hapa kukubali kwamba ipo haja ya ku – *consult* na *Board* yenyewe pale inapoonekana kuna haja pengine ya kufanya *variation* ya jambo linalohusiana na Mfumo wa *Board*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maadam Board hii ndiyo imepewa jukumu la kulea chombo hiki na Waziri analazimika kufanya *consultation,* kama itaonekana kuna haja ya kufanya hivyo, mimi nilidhani maelezo haya yanajibu kwa kiasi cha kuridhisha kabisa hoja na rai ya Mheshimiwa Dr. Slaa kwa sababu vinginevyo pendekezo alilokuwa amelitoa la kutaka *variation* hiyo iletwe Bungeni ithibitishwe na Bunge kwa njia ya azimio, mimi nikasema katika mifumo ya uendeshaji wa vyombo hivi maana yake ni kwamba hata jambo dogo la kutaka kurekebisha kitu kidogo litasubiri mpaka Bunge linalokuja, nitoe azimio baadaye ndiyo tuje tukae, nikasema pengine tufike tu mahali tukubali kwamba tumeiamini *Board*. Mimi nadhani ni chombo ambacho hakiwezi kupuuza jambo ambalo ni zito na linagusa watumishi wake.

**MHE. DR. WILBROD PETER SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Nadhani sina tatizo sana na Mheshimiwa Waziri kwani nia yetu ni kuboresha tu lakini kama nilivyosema hoja yetu haikuwa kumzuia Waziri pamoja na *consultation* ya *Board* kufanya *amendment* kuhusu baadhi ya wajumbe. Hoja yetu ilikuwa ni kufutilia mbali *Board,* maana yake hii ina kipengele kikubwa. Nilichokuwa napendekeza ni kwamba kile kipengele tu cha kufutilia mbali kihitaji azimio la Bunge na sababu ya kufanya hivyo ni nini?

Sababu ya kufanya hivi ni kwamba, kwenye *Board* ile ni wajumbe wawili tu wanaotoka kwa kundi la wafanyakazi wenyewe, sasa iwapo hawa wataonekana *stubborn,* wakorofi hata kwenye *Board* ile ikapigwa kura wao wakashindwa Waziri *in consultation* na hiyo *Board* ambayo imepiga kura bado wakawaondoa wale wakaonekana wakorofi ambao ni wale wenyewe wenye kitu chao wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi nikapendekeza kwamba ili haya mengine yaendelee ile *schedule* yetu ibaki kwa Waziri sina tatizo na *schedule,* lakini *composition* ya *Board* ambayo leo sisi tunaipitisha kwamba kati ya hao ni lazima mmoja awe ni Mwenyekiti wa *ALAT*, kati ya hao mmoja ni lazima awe mwanamke, kati ya hao ni lazima watoke wawili kutoka kwa waajiri yaani *ALAT*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hii *composition* Waziri asiwe na mamlaka isipokuwa iwe inahitaji Azimio la Bunge na Azimio kwa kawaida sio gumu kwa sababu ni Azimio tu ni *composition* tu siyo *schedule* nzima na hii ni kwa sababu ya kulinda kwa kweli uamuzi mzito, *Board* uliofanya kwamba Mwenyekiti wa *ALAT* ni lazima awe ndani, ni lazima wajumbe wawili watoke kwa wananchi kupitia kwa vyombo vyao na wa tatu ni wale wanawake tuliowataja lazima na wale pia nao walindwe. Lakini Waziri katika hii *composition* asiwe na uhuru wa kubadilisha chochote katika hilo isipokuwa kwa Azimio la Bunge.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA - MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dr. Slaa labda katika lingine, lakini kwa maelezo yangu wakati ninamfuatilia Mheshimiwa Waziri, nafikiri ametoa maelezo hayo yote ambayo unayazungumza. Ametoa maelezo ya kina, lakini labda Mheshimiwa Waziri kwa faida yake tena labda kwa dakika chache lakini kwa kweli maelezo ya kina yalishatolewa kwa kiasi cha kutosha.

Ninaomba kusema kwamba Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa Kanuni hiyo hiyo Na. 47(4) kinasema: “Badiliko lolote halitaruhusiwa kama kwa maoni ya Spika linapingana moja kwa moja na hoja ya msingi ambayo imekwisha kutolewa.” Kwa hiyo naona maelezo ya kina yalishatolewa hapa mbele yetu ambayo yanaeleza kuzingatia kwa hayo unayozungumza.

Mheshimiwa Waziri sijui kama una neno lingine la kuongeza. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba niseme tu kwa kifupi kwamba ofisi yangu ndiyo imeleta pendekezo hili mbele ya Bunge hili. Hiyo *schedule* yenyewe tunayoizungumza ni mawazo ambayo yamechangiwa na ofisi yangu, *LAPF* na wadau wengine. Tumeliweka hivyo linavyoonekana kwa nia safi kabisa tukiamini kwamba ni utaratibu ambao unaweza ukasadia kujenga chombo.

Rai ya Mheshimiwa Wilbrod Slaa mimi nachelea kutokuipokea harakaharaka kwa sababu inajenga hali ya kutokuiamini Serikali kwa kiasi ambacho mimi kidogo nashtuka, sioni kabisa kwamba Waziri ambaye anaweza akafika akaamua tu kufutilia mbali *schedule* ambayo yeye mwenyewe aliitengeneza, wale amewateua kwa sehemu kubwa ni yeye mwenyewe halafu aje tu kama mtu ambaye hakujua wajibu wake akafanya hilo jambo. Hata hivyo kuna *consultations* nyingi sana ndani ya Wizara yenyewe na vyombo vingine mpaka mnapofikia hatua hiyo itakuwa ni kitu *critical* kwelikweli na mimi sitegemei katika mazingira tuliyonayo kwamba tunaweza tukafikishana hapo.

Imewekwa kama tahadhari tu kama itaonekana kwamba iko haja, lakini hata ikiwepo hiyo haja bado utaratibu utazingatiwa mkubwa na wala usije ukashangaa kwamba tunalazimika kwenda mpaka kwa Waziri Mkuu atupe ushauri na maelekezo sidhani kama ni kitu tu tutakurupuka hivi hivi kwa wadhifa tulionao na dhamana tuliyopewa.

Kwa hiyo, mimi nilikuwa nataka nimwombe Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa aone nia nzuri ya Serikali katika jambo hili badala ya kuingiza utaratibu ambao pengine utakuwa ni wa usumbufu. *(Makofi)*

Kifungu cha 15
Kifungu cha 16
Kifungu cha 17
Kifungu cha 18
Kifungu cha 20
Kifungu cha 21
Kifungu cha 22
Kifungu cha 23
Kifungu cha 24
Kifungu cha 25
Kifungu cha 26
Kifungu cha 27
Kifungu cha 28
Kifungu cha 29
Kifungu cha 30
Kifungu cha 31
Kifungu cha 32
Kifungu cha 33
Kifungu cha 34

Kifungu cha 35
Kifungu cha 36
Kifungu cha 37
Kifungu cha 38
Kifungu cha 39
Kifungu cha 40
Kifungu cha 41
Kifungu cha 42
Kifungu cha 43
Kifungu cha 44
Kifungu cha 45
Kifungu cha 46
Kifungu cha 47
Kifungu cha 48

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila Mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 49

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Mabadiliko yake)*

Kifungu cha 50
Kifungu cha 51
Kifungu cha 52
Kifungu cha 53
Kifungu cha 54
Kifungu cha 55
Kifungu cha 56
Kifungu cha 57
Kifungu cha 58
Kifungu cha 59
Kifungu cha 60
Kifungu cha 61
Kifungu cha 62
Kifungu cha 63
Kifungu cha 64
Kifungu cha 65
Kifungu cha 66
Kifungu cha 67
Kifungu cha 68
Kifungu cha 69
Kifungu cha 70
Kifungu cha 71
Kifungu cha 72

Kifungu cha 73
Kifungu cha 74
Kifungu cha 75
Kifungu cha 76
Kifungu cha 77
Kifungu cha 78
Kifungu cha 79
Kifungu cha 80
Kifungu cha 81
Kifungu cha 82

*(Vifungu vilichotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila Mabadiliko yoyote)*

Jedwali la 1

*(Jedwali la kwanza la Muswada lilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Jedwali la 2

*(Jedwali la Pili la Muswada lilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**Muswada wa Sheria ya Mfuko wa Pensheni wa Serikali za Mitaa wa Mwaka 2006** ***(The Local Authorities Pensions Funds Bill 2006)***

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**WAZIRI WA NCHI, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imeupitia Muswada wa Sheria ya Mfuko wa Pensheni wa Serikali za Mitaa wa Mwaka 2006, *The Local Authorities Pensions Funds Bill 2006*, Kifungu kwa Kifungu na kuukubali pamoja na marekebisho yaliyofanywa.

Hivyo naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria wa Mfuko wa Pensheni wa Serikali za Mitaa wa mwaka 2006 *(The Local Authorities Pensions Fund Bill, 2006)* sasa ukubaliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa na Kuamuliwa)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Tatu na Kupitishwa)*

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA - MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, baada ya kupitia hatua zote ambazo zilikuwa mbele yetu na kupitisha Muswada huo kwa kadri ya taratibu zote zinazotakiwa, ninaomba sasa nimwite Waziri wa Nchi aweze kutoa hoja ya Kuahirisha Bunge kabla ya muda uliopangwa. Waziri Nchi, karibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. JUMA J. AKUKWETI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kwanza kabla sijatoa hoja hiyo, niseme tu, kwa kawaida wewe mwenyewe unaruhusiwa kuahirisha Bunge bila mtu yeyote kutoa hoja mpaka pale ambapo kama kuna mtu ana hoja maalum. *(Makofi)*

Sasa naomba tu ufafanuzi hapo, nitoe hoja kwa sababu kuna mtu ana hoja maalum ama namna gani?

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA - MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, kwa kuwa leo tuna hoja binafsi ya Mbunge ambayo tayari imeshawekwa mezani kwa Spika na upande wa Serikali, Waziri mwenye dhamana ya kupokea hoja hiyo anayo taarifa pia. Basi nakuomba utoe hoja hiyo ili iweze kusomwa na Waziri mhusika aweze kuitolea taarifa kama ilivyoletwa Mezani kwa Spika.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU – (MHE. JUMA J. AKUKWETI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa tunaangalia hapa upande wa Serikali, ni Waziri yupi ambaye amepewa hiyo hoja? Kama yupo au Mezani mnamfahamu, tunaomba mseme Waziri fulani anayo ingawa hiyo kwenye Kanuni hailazimishi. Lakini inalazimisha tuione hapo Mezani. Sasa tunataka kujua ipo hapo Mezani ama haipo? Ama ziko maofisini huko maeneo mbalimbali? Sasa tunataka kujua hilo kwanza, Waziri ambaye amekabidhiwa ili tumjue na kama yeye hakupewa ni vizuri kama hapo Mezani ipo.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA – MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, hoja hiyo imeshawasilishwa na ipo Mezani kwa Spika baada ya kuwasilishwa hapa Mezani kwangu leo hii mchana. Mimi niliiwasilisha kwenye Meza ya Spika ofisini. Baada ya kuzungumza na mtoa hoja, jioni hii baada ya kuingia ndani amenihakikishia kwamba Naibu Waziri, Habari, Utamaduni na Michezo tayari ana taarifa hiyo na yuko tayari kutoa maelezo ya hoja hiyo. Kwa hiyo, nilikuwa nakuomba utoe hoja ya Kuahirisha Bunge mapema ili tuendelee na utaratibu huo. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU – (MHE. JUMA J. AKUKWETI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya ufafanuzi huo, kwa niaba ya

Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kutoa hoja kwa mujibu wa kifungu cha 21 kwamba Bunge sasa liahirishwe hadi kesho saa tatu. Naomba kutoa hoja.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA – MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, tunaomba utuahirishie Bunge mpaka Jumatatu saa tatu asubuhi na sio kesho kwa kuwa ni Jumamosi. *(Kicheko/Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU – (MHE. JUMA J. AKUKWETI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri kabisa kwamba sasa badala ya kukutana kesho, likutane Jumatatu saa tatu asubuhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Kicheko/Makofi)*

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA - MWENYEKITI:** Mheshimiwa Wabunge, hoja hiyo imetolewa na Waziri wa Nchi na imeungwa mkono. Kanuni Na.40 ya Bunge letu inasema, sasa Mbunge yeyote aweza kwa kibali cha Spika kutoa maelezo yake binafsi Bungeni chini ya kanuni hii. Lakini Mbunge anayekusudia kufanya hivyo atapaswa kuwasilisha maelezo yake hayo mapema kwa Spika. Spika akiridhika kwamba maelezo hayo hayakiuki kanuni yoyote ya Bunge ataruhusu yatolewe kwa kusomwa Bungeni. Muda wa kusema utakuwa ni dakika zisizozidi kumi na tano.

Naomba nimwite Mheshimiwa Esther Nyawazwa, ili aweze kutoa hiyo hoja yake binafsi.

## HOJA BINAFSI KUHUSU KARATA ZENYE PICHA ZA WANAWAKE WALIO UCHI KUUZWA MADUKANI HAPA NCHINI

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ufafanuzi wako. Nisemee hapa au nije mbele?

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA – MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, unasemea hapo hapo ulipo.

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa mujibu wa kanuni Na. 40 ikisomwa pamoja na fasili ya kifungu cha 9 cha kanuni ya 21 ya kanuni za Bunge, toleo la mwaka 2004, naomba niwasilishe mbele ya Bunge lako Tukufu maelezo binafsi kuhusu karata zenye picha za wanawake walio uchi zikiuzwa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ziara yangu ya kutembelea Wilaya nane za Mkoa wa Mwanza niliyoifanya kuanzia tarehe 24 Agosti, 2006 hadi tarehe 24 Septemba,

2006 nilielezwa na baadhi ya wananchi kuwa kuna karata zenye picha za wanawake walio uchi zinauzwa kiholela madukani.

Katika ziara hiyo, nilipokea malalamiko kutoka kwa wananchi mbalimbali kuwa karata zenye picha hizo zilikuwa zinauzwa kiholela madukani na vijana hata wale wadogo wamekuwa wakizinunua na kuzicheza na kwamba kutokana na picha hizo zilizopo kwenye karata hizo, maadili ya vijana wengi yamekuwa yakimomonyoka kwa kasi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kujulishwa na wananchi kuhusu suala hilo, nilifanya utafiti binafsi na kuthibitisha kuwa ni kweli karata hizo zinauzwa kiholela madukani Mijini na hata Vijijini na vijana wengi wamekuwa wakizununua na kuzicheza. Ili kupata ushahidi wa maelezo yangu, nilizununua na kuja nazo ili niweze kuonyesha Bungeni kama kielelezo. Ninazo hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, picha zilizomo kwenye karata hizo, zinawadhalilisha wanawake kwa ujumla na hususani wanawake wa Kitanzania ambao hawana maadili kama yanayoonyeshwa na picha hizo yaani kukaa uchi na kuvaa vichupi tu. Hizi hapa.

*(Hapa Mhe. Esther K. Nyawazwa alionyesha kwa Waheshimiwa Wabunge karata zenye picha za wanawake walio uchi)*

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, picha zilizomo kwenye karata hizo pia zimekuwa ni kichocheo na kishawishi kikubwa kwa vijana wengi wanaozinunua na kuzicheza, cha kufanya vitendo vya ngono visivyo salama ambazo matokeo yake ni kupata maambukizo ya UKIMWI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na athari nyingi ambazo zimetokea kwa vijana wetu wengi wa Kitanzania kutokana na kuzinunua na kuzicheza karata hizo, kama vile kupata vishawishi vya kufanya ngono zisizo salama na kupata maambukizo ya UKIMWI, kuondokana na maadili ya Kitanzania au ya Kiafrika na kuiga maadili na mambo mabaya ya tamaduni za Wazungu na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi hawaelewi ni kwa nini Serikali na vyombo vyake imeachia na kuruhusu karata kama hizi kuingizwa nchini na kuuzwa kiholela Mijini hadi Vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, kwa kuruhusu karata hizi ziingizwe na kuuzwa nchini, Serikali haioni kuwa haitimizi wajibu wake kwa kulinda na kuwajengea maadili mema vijana wetu ambao ndio nguzo ya Taifa letu la baadaye?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa picha zilizomo kwenye karata hizi zinaonyesha kuwa zinaleta athari kubwa kwa maadili ya vijana na kwa nchi yetu, nawasilisha maelezo haya ili Serikali itoe ufafanuzi ni kwa nini karata zenye picha hizo zinazowadhalilisha wanawake, kuharibu maadili na kuchochea vitendo vya ngono kwa vijana, zinaachwa ziingizwe nchini na kuuzwa kiholela karibu nchi nzima? Aidha,

nawasilisha maelezo haya ili Serikali ijibu na kutoa ufafanuzi ni kwa nini karata za aina hiyo zisipigwe marufuku kuingizwa na kuuzwa nchini kwetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii na nawashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU – (MHE. JUMA J. AKUKWETI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba nitoe maelezo yafuatayo:-

Kama wewe mwenyewe ulivyoshuhudia na Bunge hili kushuhudia hivi punde kumekuwa na maulizano na majadiliano ya haraka haraka kuhusu kuijua au kutoijua taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kanuni ya 40 ya kanuni zetu za Bunge ambayo imetoa namna ya kuendesha shughuli katika eneo hili haisemi kwamba lazima nakala ile iletwe Serikalini, lakini inasema iletwe kwa Mheshimiwa Spika. Kwa utamaduni wa Bunge hili, ili mambo yaende vizuri, tuweze kujibu vizuri kwa faida ya Watanzania, imekuwa ni utamaduni kwa ofisi yako kuleta Serikalini ili itafutiwe majibu na tuendeshe shughuli hii vizuri. Kwa bahati mbaya katika hili, hiyo nakala ilikuwa bado njiani haijatufikia. Sasa naomba kusema yafuatayo.

Maelezo ya Mheshimiwa Mbunge ni maelezo mazuri, ya kina na ya fasaha na kwa kweli mimi kwa niaba ya Serikali napenda kumpongeza sana kwa maelezo hayo. *(Makofi)*

Napenda kumwahidi yeye, wewe na Bunge zima hili, kwamba Waziri anayehusika na eneo hili atatoa maelezo kuhusiana na jambo lenyewe, lakini hayatakuwa sasa hivi kwa sababu kama nilivyosema, ndio kwanza tunasikia hoja yenyewe. Basi tutatizama na zitatafutwa na hizo karata na maelezo yanayohusika na hatimaye tutatoa maelezo hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niishie hapo na nakushukuru kwa kunipa nafasi.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA - MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naomba kuishukuru Serikali kupitia Waziri wa Nchi, kwa kuona umuhimu wa hoja yenyewe. Kama alivyotoa maelezo hayo, kwa mujibu wa kanuni, ninakubaliana naye na tunaomba Serikali ipate nafasi ya kuyapatia maelezo hayo kwa kina na kuona nini inaweza kusema juu ya suala hilo.

Baada ya kupokea maelezo hayo na kupitisha hoja ya Kuahirisha Bunge mapema kabla ya wakati. Sasa naomba nichukue nafasi hii kuahirisha Bunge mpaka siku ya Jumatatu, saa tatu asubuhi ndani ya ukumbi huu huu.

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Saa 12.10 jioni Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumatatu,
Tarehe 6 Novemba Saa Tatu Asubuhi*)